ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini - Tarehe 29 Juni, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya SUZA na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, vile vile naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na nayo, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa naomba kumwita Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naye aje.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia ya mwaka 2016, naomba kuwasilisha.

Mhe.Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Naomba sasa nimwite Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, naye aje.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani hati ya Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ya 2016

(*Majadiliano yanaendelea*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru kwa kuniruhusu kuweka utaratibu kifungu cha 63.

Kwa masikitiko na kwa huruma kubwa leo katika *order paper*, serikali iliji-*commit* kupitia *Hansard* ya Mhe. Mohammed Aboud. "Mhe. Jaku, kabla ya kufunga Baraza hili tutaleta taarifa" na leo ninaona siku ya mwisho katika *order paper*, sijui kama pana miwani hapa niazimwe naona haimo hiyo hoja.

Kwa hiyo naomba muongozo wa kiti chako kwa heshima na taadhima ya hali ya juu Mhe.Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Jaku. Ni kweli serikali ilikuwa imeji-*commit* kwa ajili ya kuja kutoa maelezo hapa Barazani, lakini taarifa ambayo niliipata kutoka serikalini ni kwamba walikuwa wanahitaji muda zaidi kwa ajili ya kuja kutoa maelezo kuhusiana na suala hilo na pamoja na hivyo, serikali kupitia Wakuu wa Mikoa wamekuwa wakifafanua hilo suala ambalo lilihitajika kutolewa maelezo humu Barazani.

Kwa vile mimi kama Spika, niliridhika, kwa hiyo nimewaruhusu wajiandae na hatimaye baadaye watafute njia ambazo watakuja kutufahamisha. Kwa hiyo suala hilo ndio kama hivyo lilivyo, kwa hiyo naomba tuendelee. (*Makofi*)

Waheshimiwa, leo ni siku ya kuchangiwa ule mswada, kwa hiyo nitamwita mchangiaji wa mwanzo Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza hili tukufu na kuchangia mswada wa sheria ya kuanzishwa Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote na wataalamu mbali mbali walioona kwamba pana haja hivi sasa katika nchi yetu kuwa na Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Spika, tunaamini sisi Wazanzibari tumechelewa sana, lakini kama tunavyosema ukichelewa siku nyengine na wewe utapata mazuri, baada ya kuona kwa wenzetu katika Tanzania Bara mfano mikoa mbali mbali Hospitali za Rufaa zimo na sisi tunategemea yatakuwa hayo.

Mhe. Spika, Hospitali ya Rufaa ni jambo muhimu sana katika nchi, lakini umuhimu wake zaidi unategemea vitendea kazi na wataalamu mbali mbali ili liendane na jina lake kuwa ni rufaa.

Mhe. Spika, kwanza linalohitajika tuwe na madaktari wa fani mbali mbali. Hospitali ya Rufaa iwe na wafanyakazi wakarimu yaani wana huruma na wananchi. Hospitali hii masaa 24 pawe na madaktari wanafanya kazi bila ya kuchoka, maana rufaa wakati wowote inapotokea inategemewa hiyo.

Mhe. Spika, mimi ombi langu kwa wizara, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuliangalia hili na kuwa kweli jina linafaa la Hospitali ya Rufaa basi la kwanza tuwe na wataalamu, yaani madaktari wa fani mbali mbali katika nyanja zote. Lakini pia vipindi vyote vya masaa 24 pawe na huduma. Kwa mfano hivi sasa hivi Mhe. Spika, hivi sasa hivi tulipo, tunategemea wazanzibari wote hospitali kuu ni hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini wanatokea wagonjwa wanakwenda pale kuanzia asubuhi mpaka jioni daktari hawamuoni, hiyo ni hatari.

Kwa hiyo niseme tu kwamba, je, hili tunamwambia Mhe. Waziri kweli tutafikia lengo hilo tunalolitegemea kwa rufaa. Bila ya kuwa na mkakati wa kuwapata madaktari waadilifu na waaminifu kwa nchi hii tutakuwa na jina la rufaa ambalo halina tija ndani yake.

Mhe. Spika, jambo jengine kubwa ili hii hospitali iwe nzuri na ifanye kazi kwa ufanisi ni vitendea kazi. Leo tunafika wakati hospitali yetu unakwenda unataka vipimo mbali mbali si vikubwa sana Mnazi Mmoja hamna. Namuomba sana Mhe. Waziri hili kwanza liangaliwe kwa macho mawili.

Mhe. Spika, mimi nimempa mifano mingi Mhe. Waziri, mtu anakutwa na matatizo anakwenda hospitali daktari anatafutwa masaa manane haonekani; mgonjwa yupo kitandani au yupo kwenye kiti kakaa kitako hajitambui, lakini sijui. Mimi ninarudia tena kauli yangu nzuri tu, unapokuwa mwanajeshi uko *recruit* unakula kiapo cha uaminifu au askari yeyote kiapo cha uaminifu ndio

kazi yake, kuwa atafanya kazi saa 24 kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Na madaktari au wauguzi nafikiri wanaposoma katika vyuo vyetu kwanza hula kiapo cha uaminifu, cha kuwa yeye muadilifu, atakuwa na huruma, atakuwa na kila kitu, lakini kwa upande wetu wa Zanzibar sio wote, sio madaktari wote au wauguzi wote, haya mengi yamekosekana. Namuomba sana Mhe. Waziri, hii rufaa ni nzuri lakini rufaa iwe na vitendea kazi.

Mhe. Spika, hapa tutategemea kuwa na magari ya kutosha, tutakuwa na madaktari wa kutosha, tutakuwa na kila stahiki ya vifaa vya kutosha ili wananchi wetu wanakwenda pale wanaambiwa leo *CT Scan* haifanyi kazi, lakini nenda *Global* hapo utapata, sijui kuna mchezo gani unaochezwa ambao haufahamiki kwa wananchi wetu.

Mimi naiomba serikali hili suala kwa jina kubwa sana, rufaa ni kitu cha mwisho maana yake, kashindikana huko kapelekwa hapo kuwa ndio atapata huduma za kutosha. Kwa hiyo jina la rufaa lieleweke kwamba ni hatua ya mwisho kwa mgonjwa au aliyepatwa na maafa yoyote kwenda kupata huduma ya mara moja katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi tumeyaona. Mimi nitamuomba sana Mhe. Waziri. Jana katika kipindi cha maswali na majibu, liliulizwa swali hapa mambo ya hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini mimi nikauliza, nataka akija hapa Mhe. Waziri, atupe kauli thabiti, tuna madaktari wangapi bingwa kwa hospitali yetu hii ya Mnazi Mmoja, na kweli mimi ninai-*confirm*. Lakini pili madaktari hao wana fani gani katika nchi yetu.

Sisi tulikuwa na madaktari mbali mbali; palikuwa na mwalimu wangu Dkt. Jidawi, tulikuwa na daktari bahati mbaya mwenzetu yule kapata maradhi Dkt. Malik, mpaka leo Mungu hatujui kampeleka wapi. Hawa ilikuwa kidogo unaamini pale hospitali ukienda na wengine wapo wazuri lakini hawa ilikuwa saa 24 mtu anajua wajibu wake na anafanya kazi yake kidhati kabisa.

Mhe. Spika, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, hospitali ya rufaa inafaa lakini rufaa ndiyo huwa ya mwisho. Maana mtu anaposhtakiwa huko Mahakama ndogo ndogo mwisho anaishia rufaa, inavyomalizika huko ndio hivyo hivyo. Kwa hivyo namuomba sana Mheshimiwa hili jina tulichukulie la uaminifu na la mwisho katika wananchi ili kupata huduma zao kwa usalama wa maisha yao.

Mhe. Spika, jambo jengine. Hospitali ya Rufaa bado nakuja hapa hapa, si majengo tu ya kulaza wagonjwa au huduma ndogo ndogo za kutoa dawa, lakini pawe na muelekeo pa kujengwa banda la kungojea wagonjwa saa 24. Maana

Muuguzi au mgonjwa ana wazee wake au ana watu wake wanaomuhudumia hospitali pale, lakini leo Mheshimiwa jambo la aibu Mnazi Mmoja naichukulia ndio hii rufaa yenyewe tunaitegemea baadaye pa kusubiri mgonjwa, kwa sababu kuna wagonjwa wa aina tafauti, kuna wagonjwa wanategemea misaada mbali mbali, lakini kuna wagonjwa kama waja wazito ndugu zetu watoto au mama zetu au dada zetu, mzazi hakubali kuondoka akawa mbali, kwa sababu tunaomba salama ajifungue salama lakini lisimtokee baya akaathirika maisha yake, lakini leo pa kukaa kusubiri hana.

Mhe. Spika, kwa hivyo namuomba sana hili ndio hivyo vitendea kazi vyenyewe. Vitendea kazi, madaktari wazuri, wauguzi wazuri, wanaojali watu pamoja na huduma za jamii wanaosubiri wagonjwa wao.

Mhe. Spika, najua unaniangalia kutokana na muda, mimi baada ya hayo machache namuomba sana Mhe. Waziri, naiomba serikali hili suala la rufaa tulipe jina linalofaa kwa kutekeleza wajibu wetu kwa wananchi wetu naunga mkono mswada huu. *(Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shihata na hasa kwa namna ulivyozingatia muda, kwa sababu umekwenda kwenye mambo yenyewe yanayohitajika, umechangia *issues* zinazohusu mswada, hukutoka sana nje ya mada, kwa hivyo na hata hawa wengine wanaochangia tusiende sana nje ya mada, twende kwenye mada inayohusu hospitali hii ya Mnazi Mmoja.

Sasa ninaomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar, atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii asubuhi hii kuweza kuchangia katika mswada ulio mbele yetu.

Mhe. Spika, sina budi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijaalia uhai na afya njema, namuomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe kufanya niliyokusudia.

Mhe. Spika, kwanza sina budi Mwenyezi Mungu nimshukuru kwa kuniwezesha hapa lakini pia kunipa uono wa mambo haya machache ambayo niliyaona katika waraka huu na mimi naomba nipate kuchangia kidogo.

Kwanza naipongeza serikali kwa maamuzi haya yaliyoona kwamba kwa nchi yetu ni vizuri kuyaleta mbele yetu na kuweza kuyafanyia kazi ili nchi yetu

kuweza kupata mambo mazuri tuliyoyakusudia katika kujenga maendeleo na afya za watu wetu.

Mhe. Spika, siku zote lakini kuna maneno yanasemwa kwamba *nia inashindwa na matokeo*. Kwa hivyo nia ni nzuri lakini matokeo yasije yakawa mabaya mbele yetu na hatupendi iwe hivyo. Kwa maana kwamba hii nia tuliyoianzisha iende sambamba na matokeo yatakayokuja, kwamba lengo ni kwamba watu wetu wa nchi yetu wazanzibari wasipate matatizo, yapungue matatizo ya afya ambayo yanaikabili nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi katika waraka huu naomba kwanza katika kifungu nambari nane cha waraka huu uliopo mbele yetu hilo neno linalotumika kwa sababu ni kitu cha sheria hii, neno moja linamaanisha maana nyengine, kwa hivyo linapotumika mwahali ambamo halikukamilika mtu anaweza akaja akalitumia vyengine, kwa vile mnasema hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Taifa basi litumike pale isitajwe neno hospitali tu. Tunapendekeza sana litumike neno hospitali ya taifa ya Mnazi Mmoja badala ya kuwa hospitali tu, hospitali inaweza ikakamatwa yote ile lakini tunasema hospitali ya taifa ya Mnazi Mmoja. Naomba hapo tuliangalie sana hilo.

Mhe. Spika, lakini pia vile vile niende kwenye kifungu cha 17 namba 1 kifungu (c) na (f). Hii nina wasi wasi kuhusu hii Idara ya Utawala na Rasilimali Watu na Fedha.

Mhe. Spika, hii Idara kwa kweli ni Idara muhimu sana. Namuomba sana Mhe. Waziri, katika kupanga kwake Idara hii iangalie na watu walio na uzalendo wa nchi hii, isije ikawa kama vile zamani awamu zilizopita wizara hii tukawapa watu kuikamata Wizara hii ya Afya na wao ndio ambao waliokuwa wakidai kwamba hakuna afya hakuna kitu gani, lakini serikali ikawakabidhi majukumu haya matokeo yake ikawa ni vile vile.

Kwa hiyo mabadiliko yapatikane safari hii serikali yote ni ya Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo na hawa ambao hawatutakii mema serikali hii na nchi hii basi wasiweze kupewa nafasi katika Idara hii muhimu ya utawala na rasilimali watu na fedha. Kuendelea kuwapa watu ambao hawana imani na nchi hii, kwa kweli tutakuwa hatujapiga hatua, ile nia yetu ndio yale yale matokeo yatakuwa ni mabaya. Kwa hiyo naomba sana waziri atakapofika wakati kuunda Idara hii ya utawala na rasilimali watu na fedha awe muangalifu sana, ushauri wangu ni huo.

Mhe. Spika, pia katika kifungu (f) cha kifungu nambari 17 kifungu kidogo (f), Idara ya Huduma ya Uchunguzi wa Afya. Kifungu hichi nacho ni muhimu sana kwa sababu kama tunavyojua kwamba hakuna matibabu yatakayofanyikana bila ya uchunguzi, uchunguzi ni vifaa, hivyo ni vyema kwamba serikali kwa kuanzisha wizara hii katika Hospitali ya Rufaa ni muhimu sana kuwa na vifaa vinavyostahiki, lakini pia na wataalamu.

Mhe. Spika, ni juzi tu tulipata semina hiyo iliyopita nyuma yetu kwamba wataalamu ni kidogo sana na wengine wanarudi masomoni, wataalamu hawa elimu yao inabaki kwenye vichwa vyao na madaftari yao. Kwa hivyo tunapoanzisha hospitali kama hii tujipange vizuri. Na mimi ilikuwa nia yangu kwamba tusianzishe hospitali hii kuifanya ya rufaa, lakini baada ya kupata maelezo miongoni mwa hao wataalamu wakasema jamani ikubalini kuanzishwa kwa hospitali hii hayo matatizo mengine ndio yatatuka, kwa hiyo yapewe kipaumbele ni vifaa, madaktari ambao wamepoteza muda wao mwingi sana wa kuchukua elimu hiyo, kwa hiyo wakija wapate waifanyie kazi, vifaa vitumike isiwe vimebaki kwenye maghala ni kama kuwa hatuna vifaa.

Mhe. Spika, kwa hivyo ni suala muhimu sana hili tulipe kipaumbele katika kuhakikisha wataalamu wetu wanapata vile vifaa vya uchunguzi badala ya kila jambo moja unasikia uende Bara, uende India, hii itatupunguzia matatizo wananchi wetu ambao wengi wetu ni masikini, hawana uwezo, leo mkipata mgonjwa mmoja tu katika familia ishakuwa ni fadhaa kubwa sana. Namuomba sana Mhe. Waziri hili alipe kipaumbele katika huduma ya uchunguzi wa afya, lakini katika huduma hiyo ya uchunguzi wa afya isiishie katika hospitali tu, ule mtindo wa zamani wa kuchunguza afya za wanafunzi, watoto wetu katika skuli uendelee, kwani tukilianza jambo bado dogo tunaziba ufa kabla ya kujenga ukuta.

Kwa hivyo, huduma hii naomba sana na pia katika huduma hii iangaliwe kwamba zile kamati za huduma za afya za shehia zifanye kazi, zikiwa zitaweza kufanya kazi mambo mengine yatatuepuka kama haya ya kipindupindu kutokana na usafi; bado mitaani huko tunakufa ovyo kabisa, lakini itakapokuwepo huduma hii ya kamati za afya zitasaidia sana zikiwezeshwa na wao wenyewe wakilikubali jambo hili.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Afya kupitia wizara zake zilizoenea katika nchi nzima hili naomba lifanyiwe kazi.

Sasa niende katika kifungu cha 25 kuhusu kinga. Hapa kuna neno mimi naona sijalielewa vizuri katika *paper* hii naomba nikinukuu.

Kifungu cha 25 kinasema kwamba:

"Mjumbe wa Bodi, mfanyakazi au mtu mwengine yeyote ambaye anatoa huduma Hospitali, hatoweza kuwajibisha binafsi...".

Mhe. Spika, hapa ndipo ninapotaka kujua, hatoweza kuwajibisha au hatoweza kuwajibishwa kwa kitendo, jambo au chochote alichokifanya. Mimi katika kusoma kwangu naomba ufafanuzi atapokuja Mhe. Waziri hili neno ni kuwajibisha au kuwajibishwa.

Halafu niende katika kifungu cha 27. Kifungu hiki kinasema itatoa huduma bila ya malipo. Ni sawa, lakini huku nyuma alishaeleza kwamba kutakuwa na malipo ya ada. Sasa malipo haya vipi? Ufafanuzi naona sijapata na hili pia naomba atapokuja Mhe. Waziri anipe au atupe ufafanuzi ili tuweze kuelewa, ndio hilo hilo kasema itakuwa huduma bila ya malipo lakini huku kuna kifungu kutakuwa na ada, michangio, michangio ni fedha si kwamba mtu anakuja na kuni au kitu gani, ni fedha, na ada ni fedha halafu huku anazungumza huduma bila ya malipo. Hili naomba liwekwe wazi na wananchi walielewe nini makusudio yetu.

Mhe. Spika, ahsante sana naomba niishie hapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nami nikushukuru nisipoteze muda pengine muda wenyewe hautotosha na nianze na utangulizi tu Mhe. Spika. Naomba nimnukuu Mhe. Spika kama ifuatavyo:

"Lakini kabla ya kuwahoji nataka niseme maneno yafuatayo. Waheshimiwa Wajumbe nataka niwasihi sana, kwamba chombo hiki ndicho kinachotoa uongozi wa nchi. Baraza la Wawakilishi ni chombo cha wananchi, wananchi tunawawakilisha na sisi tunafanya shughuli kwa ajili yao, mamlaka hasa ni yao..."

Mhe. Spika: Mheshimiwa nakuomba uchangie Mswada tafadhali, usiende nje ya hapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: *Hewallah* Mhe. Spika. Nianze na Mswada tuliopewa huu wa Sheria ya Kuanzisha Hospitali ya Taifa. Mhe. Waziri watendaji wake naomba wanisikilize kwa makini hapa, na mimi naomba kuweka *hansard* sawa kama tunaupitisha Mswada huu hii wizara tutawapa miaka mitatu, vyenginevyo huko mbele tutakuja na hoja binafsi kuuvunja huu kama tutakuwa hai. Tunatoa miaka mitatu kujaribu, tukishindwa huko tutakuja

na hoja binafsi kuuvunja, Waswahili wanasema, *mtoto akililia wembe mpe*, lakini una mambo mazuri na mambo mabaya, tuwe wakweli.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka huu mswada ilikuwa angalau tukae na wadau, haya ni maisha ya watu tunayoyapitisha hapa, ndio yale niliyosema tunakwenda kuulizwa hii dhamana na uzoefu unaonesha huko maji yalikuwa hayalipiwi, elimu bure, tunakuja huku tumeshajipanga kwa hili? Una mambo mazuri, una mambo mabaya, tutayaona Mheshimiwa.

Mhe. Spika, nianze na uwakala kifungu cha 3(1). Dkt. Jamala Adam anisikilize vizuri ili wakasaidiane katika majibu. Mimi nataka kufahamu uwakala kifungu hiki kitakuwa nusu nusu au kizima. Mnazi Mmoja chanzo cha kupatia fedha kiko wapi, kutegemea *first track*, ku-*park* zile baiskeli ndani na vipimo vyenyewe havipo. Lakini jengine uzuri wake likifanywa hili tukienda vizuri mambo ya Bima hapa unafikiri Mnazi Mmoja ukipata shilingi 1,000,000 kwa mwaka au 2,000, 000 ukiitizama Al-Rahma alikuwa akipata karibu shilingi bilioni moja kwa mwaka. Ni jambo zuri hili litasaidia pesa hizi kwa kujengwa vizuri, ubaya kuwa wale bila wakija pale pesa hizi zikapatikana wakawa na vipimo watu hawawezi kwenda Bara, ndio lengo tunalokwenda.

Kwa hivi sasa tunapata shilingi 2,000,000 kwa mwaka, ikija ikipatikana shilingi bilioni moja kwa mwaka ni jambo zuri na makampuni mengine yangeweza kuja kuwekeza hapa kwenye suala hili. Hicho ni kifungu cha 3(1).

Sasa nije kifungu cha 4(2), kutekeleza majukumu ya udhibiti na usimamizi wa Hospitali nyengine yoyote kama ilivyo sheria au sheria nyengine'.

Mhe. Spika, hoja yangu hospitaji yenyewe kuingia mkataba, lakini haikueleza wazi hapa kama itapata mkopo benki, ilikuwa ieleze wazi kama itapata mkopo benki. Kwa mkataba unaweza kuingia tu na *MoU* ni mkataba tu, lakini ilikuwa ieleze kifungu hiki kama hospitali inaweza kupata mkopo benki ili kwenda kununua vitu kama vile vitu vya *CT-Scan, X-Ray Machine*, ilikuwa ieleze katika kifungu hiki na vile vile serikali iwe dhamana, iwe nyuma yake, serikali iwe dhamana yake katika kufuatilia suala la mikopo.

Mhe. Spika, nije kifungu cha 5. Mhe. Waziri, Waheshimiwa Watendaji huko tusikilizane na kidogo katika hili kuna neno lirekebishwe kazi za hospitali (j). Mashirika na kwa watu binafsi kwa msingi wa "maedeleo" ingewekwa "maendeleo" badala ya maedeleo ingerekebishwa hiyo.

Kifungu cha 5(e) Wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi, iangaliwe vizuri. Sekta binafsi au sekta ya afya ilikuwa itaje kuna kinga, tiba, afya ya jamii na ni *specific* aliyetajwa hapa, ilikuwa kielezwe wazi kifungu hiki.

Mhe. Spika, nije kifungu cha 7(b), 'ametenda kosa kinyume na maadili au kuwa na tabia isiyokubalika na jamii".

Mheshimiwa maadili suala hili liko kwenye sheria tulipitisha hapa ya Maadili ya Viongozi Nam. 14 Mwaka 2015. Mjumbe wa Bodi anaweza kuwajibika na sheria hii tumepitisha hapa. Iangaliwe vizuri Mheshimiwa, mimi narudia tena nimezaliwa shamba, nimesoma shamba, nimekulia shamba, naishi shamba wakati mwengine, elimu yangu ni ndogo.

Mhe. Spika, hapa naomba Waheshimiwa Wajumbe wanisikilize kwa makini sana, kifungu cha 17 naomba tusikilizane kwa makini na hapa nizungumze kwa lugha kidogo inayoweza kuwa nyepesi. Hapa pana mtihani, naiomba wizara ikaongeza kifungu (g) ingeweka *customer care*. Nini maana ya *customer care*? Unapofika pale daktari hukumkuta ukalalamike na kiwe *24 hours* hiki, lakini hapa tusije tukakipitisha. Wapiga kura wetu, wazee wetu, watakwenda kuteseka, ukienda pale daktari humuoni huku tumeshapitisha tujue pa kulalamika, utamtafuta daktari humpati watakuwa hawatekelezi majukumu yao.

Kifungu hiki Wajumbe tufahamiane vizuri tukizungumza, lazima kuwe na *customer care*, umefika daktari hayupo huwezi kumpata Mkurugenzi kwenda kumgongea mlango utaambiwa wewe nani, hiki tuwe makini tusije tukakipitisha kwa upande wangu mimi naomba, kama tumekifahamu lazima tuwe na *customer care* pale, malalamiko yetu tupeleke. Daktari wa mifupa hayupo, *X-ray* hayupo, huwezi kumpata Mkurugenzi, *customer care* lazima iwepo daktari hatekelezi wajibu wake ni mtihani tunakwenda kumlalamikia nani? Nafikiri Waheshimiwa Wajumbe tumefahamiana katika kifungu hiki ni muhimu sana tukija kukipitisha kama hatukupata *customer care* kwenye malalamiko yetu tutakuja kupata mtihani. Mkurugenzi huwezi kumuona mpiga kura, tutakwenda sisi kama Wawakilishi kwenda kugonga mlango kwa waziri au naibu waziri watakuja kuumia watu wetu wa chini.

Mhe. Spika, nije kifungu cha 19. Hapa pana kifungu cha 17, 14 na 19 naomba niunganishe. Wakurugenzi wa Bodi imetiwa Wakurugenzi wa Idara ya 18 au 19. Hoja yangu kwamba, Wakurugenzi wa Idara wawe na wataalamu wanaoweza kufanya shughuli hizi, na hapa wataalamu watakuja kukimbia wanakwenda kwenye sekta binafsi watu wanalipwa kwa dola kule. Kuna Dkt.

Jamala, Dkt. Marijani Msafiri anafanya kazi peke yake, juzi katupa semina tumeiona yule peke yake kwa siku anaweza kufanya operesheni 20 au 30 mwisho atakimbia.

Sasa hapa wataalamu waje wakafanye hizi kazi tusiwape vyeo vya ukurugenzi, tuna wataalamu kidogo hiki kitengo atakaa mtu mwengine yeyote, Dkt. Jamala ateremke chini, kina Dkt. Naufal Kassim wateremke chini, Dkt. Marijani, wakafanye hizi kazi za operesheni hapa ni kuboresha maslahi yao; maslahi ndio kitu muhimu ndio utakuta hao wengine wanatoka kwenda katika mashirika mengine huko wanalipwa kwa dola. Bado hatujafika kuwa kigezo cha Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Ali Suleiman Ali kazungumza hapa na tumepata darasa, *specialist* hamna, hatujafikia bado, hii *oxygen* yenyewe kwa tabu, *X-ray Machine* haipo, ni mtihani, *generator* lenyewe linakofanya kazi ni sehemu mbili tu, kwenye *maternity* na ukitokea operesheni *theatre*. Kwa hiyo, bado hapa kuna mtihani kidogo, sio mdogo, tutafute madaktari mabingwa ndio kitu cha mwanzo na maslahi yao yatengenezwe watafutiwe gari, viwanja, wapate kujenga, maslahi ndio kitu muhimu. Hapa nakusudia kuwalinda ma-*specialist* ndio lengo langu, hawezi kukaa mtu mmoja kufanya kazi zote hizi utakuta wataalamu wanakimbia wanakwenda vitengo vyengine kwenye dola.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 21 kutakuwa na fedha za hospitali zitajumuishwa. Hapa ndipo penye mtihani Mheshimiwa, kwamba hapa pamoja na wafanyakazi wa hospitali tuna tabia mbaya kuhusu wana siasa. Tusikilizane vizuri, hapa kutakuwa na siasa ya *CUF*, CHADEMA, *NCCR Mageuzi*. Wataalamu wasiingiliwe katika mambo ya siasa, tutafika kuibomoa nchi hii, tusiajiri mtu kwa sababu ya siasa hiki kitengo ni muhimu tusiyaingilie hayo hapa. Watu wanaacha kazi kutafuta maslahi mengine, hiki ni kitengo muhimu tusikae kuchambua watu hapo, tuwaboreshe na tuwape vifaa ili wakafanye kazi, suala la siasa halihusu hapa, tusije tukafika huyu kala ng'ombe, huyu kala mbuzi aa, tusije tukafika huko.Tuwaajiri lakini isiwe huyu yuko upande huu, huyu upande huu, tutakuja kuharibikiwa, sisi tunataka kuokoa maisha ya watu.

Mhe. Spika, nikija kutoka katika kifungu hicho nije tena hapo hapo suala la kuongeza wataalamu. Hapa wataalamu wanavunjika moyo wanakwenda kukopa katika Mfuko wa Elimu ya Juu shilingi 300,000 anakatwa shilingi 200,000 anabaki na shilingi 100,000 ataishi vipi, atasoma vipi ajisomeshe mwenyewe, hili suala liangaliwe maslahi yao.

Nikitoka hapo nije kifungu cha 22(b) Michango na Malipo. Hapa ndipo penye huo mtihani wenyewe hasa Mhe. Spika, ruzuku na mishahara ya *OC* nataka kupendekeza ruzuku nijue kiasi gani inaweza kupatikana, mahitaji ya msingi ya hospitali ikiwemo dawa, vifaa, tiba na maslahi ya wafanyakazi, kwa kutegemea *OC* tu na serikali kutia pesa ielezwe ni shilingi ngapi itaongeza serikali kwa pesa hizi. Kwa ruzuku ya mishahara hapa nataka ufafanuzi wa *OC* au tunarudia kule kule nyuma, ijulikane ni shilingi ngapi zitahitajika. Dkt. Jamala Adam nafikiri ananifahamu huko juu aliko.

Mhe. Spika, nije tena katika kifungu cha 22(b) chanzo chengine kilichotajwa hapa ni michango, ada, malipo na mikopo kutoka kwa watu na taasisi. Hapa swali tuna sera ya malipo bure. Je, hatuna uwezo? Kuna kifungu mbele cha 27 nitakigusia kidogo tu *which is which*, huduma. Hapa tusitake kuwadanganya wananchi wetu, haujaelezwa wazi huu waraka tulioletewa, pana mtego na itabidi tuelezwe kama wanataka kuwalipisha wananchi au vipi, hapa mtego kifungu cha 22(b), waeleze nini sera yao kuwachangisha watu ili wafahamu vipi mnyonge atapata matibabu.

Sasa nije kifungu cha 23 kubakiza fedha. Kifungu hiki ndicho wanacholilia wao sana wizara. Waziri wa Fedha nimuombe sana ni msikivu, lakini kwa suala hili hiki kinakwenda sambamba na kifungu cha 22(b) kinachozungumzia malipo, na maana hiyo ndio inayosema mwanzo wa huduma kuwa ni malipo, tunaamini tusiogope ikiwemo wazi michango ya malipo. Fedha hizi kwa nini kiwango hicho hakikubakisha fedha ya waziri? Waziri wa Fedha na Mipango hapa asije akaingilia, namuomba sana ndugu yangu, kuna taa (*bulb)* hazimo mle ndani, huu ndio msaada wao waliokuwa wanautafuta, maamuzi yao pesa zibaki pale. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha hiki awaachie, hili ndio lengo lao kubwa pesa watumie wenyewe pale, madhali patakuwa pana *auditor*, muhimu kifanyiwe *auditing* ndio kitu cha muhimu, lakini pesa zile ukija ukizichukua, shilingi ngapi wanazopata? Halafu leo ukachukue ubaki nazo uwapangie matumizi. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha, hili kwa heshima kabisa awaachie wenyewe awepo *auditor* wazikague ndio lengo lao kuleta mswada huu.

Mimi nilikuwa Mjumbe wa kamati hiyo, pesa zikifika kule Mhe. Omar Yussuf Mzee pesa zile zinakwama, hili ndio lengo lao na pesa hizi Mhe. Waziri wa Fedha asije akazigusa. Waheshimiwa Wajumbe hapa kidogo tufahamiane, waachiwe mamlaka Wizara ya Afya wakusanye hizi pesa watumie lakini kuwe na *auditor* ni kitu muhimu, isije ikafika kama wale waliozuiwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 27 huduma bila ya malipo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub una dakika mbili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, huu Mswada ni mkubwa lakini unataka kuchambuliwa ungeniongeza na tatu kama itawezekana.

Kifungu cha 27 Huduma ya Malipo ya Sera ya Kimapinduzi. Ninashauri Serikali ya Mapinduzi, hapa naomba nisikilizwe Sera ya Mapinduzi ya mwaka 1964 elimu ilikuwa bure, maji bure, matibabu bure, lakini tuangalie kwamba 1964 na 2016 tafauti yake ikoje, tumefahamiana Waheshimiwa Wajumbe? Mwaka 1964 watu walikuwa kidogo, matibabu yalikuwa kiasi kidogo, *population* ilikuwa ni ndogo, uchumi ulikuwa mdogo, lakini tuangalie hivi tunavyokwenda sasa hivi.

Vile vile uwezo wa serikali mwaka 1964 sio uwezo wa 2016 hivi sasa, tukubali hayo mambo, tuyapime idadi ya watu imeongezeka kutoka mwaka 1964 mpaka sasa hivi 2016 kweli tutahudumia watu hivi? Bajeti ya mwaka 1964 sio bajeti ya sasa hivi mwaka 2016, *two things are different,* tukifanya mambo tukae tuyafikiri.

Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba serikali ikafikiri sera ya matibabu bure ijibebeshe mzigo wakati uwezo haupo, huu ni mtihani ambapo jambo hili serikali ikae ilizingatie. Nimerudia waamue kama matibabu bure kweli au watu wachangie na watu hawana shida kuchangia, huduma tu iwepo.

Wewe ukiikata tiketi ya boti kwenda Dar es Salaam kufuata huduma au waweke vitengo viwili huku pata sote, huku hohe hahe, huku watu wa kati kati na watu wa juu.

Mhe. Spika, narudia tena Wizara ya Afya huu mkataba kama nitakuwa hai mimi kwa binafsi yangu kama serikali itanikubalia au itanikatalia kama mswada wa ng'ombe nilioulеta humu ikanikatalia, natoa miaka mitatu, vyenginevyo nitakuja na hoja binafsi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda wako wa kuchangia umekwisha, nakushukuru. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said atafuatiwa na Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Nadir Abdul-lafit Yussuf ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia mswada wetu huu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nipende tuungane nanyi tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuamka salama usalimini na kuendelea na kazi zetu kama kawaida.

Mimi kwanza nianze kwa kumshukuru sana Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake na mbinu zake za kila aina kwa wananchi wake kuwasaidia katika hali na mali na afya bora pamoja na maisha bora.

Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu katika masuala yote ya Mnazi Mmoja. Mimi ninachosema ni kwamba naipa pongezi serikali kwa madhumuni makubwa ya kuliangalia jambo hili ambalo ni moyo wa binadamu au ndio moyo wa nchi kutokana na hali za afya za wananchi wetu.

Mimi ninachotaka kuchangia ni kwamba nakubaliana na maneno ya waziri jana, alipozungumza kuhusu habari ya kwamba huu mswada ni wa haraka haraka.

Nakubaliana na masuala aliyosema katika nchi za Afrika Mashariki kwamba lazima tuungane na hayo masuala mengine, lakini hata kama tumechelewa tunatakiwa na sisi tuharakishe mambo ambayo yametucheleweshe ili tukimbilie pale ambapo tumechelewa tupawahi. Kwa sababu Mheshimiwa wenzetu wamejipanga kuhusu masuala haya. Sisi tumechelewa, kwa hivyo uchelewaji wetu usifikirie kwamba ndio uwe sababu ya mambo yetu kuchelewa hivyo hivyo. Ni lazima tujikaze kwa mbinu zozote ili tuweze. Lakini ninachotaka kusema kwamba kwanza tutizame malengo na madhumuni ya huu Mswada.

Malengo tunayafahamu maana yake ndio tumeletewa katika miswada mingi, na malengo makubwa ni kuboresha afya mara, nyingi tunapiga kelele sana kuhusu madaktari bingwa kuhusu matatizo tunakwenda India, tunakwenda Bara na maeneo chungu nzima kutafuta matibabu.

Sasa ikiwa madhumuni makubwa ni hayo na malengo makubwa ni hayo na ndio yaliyokusudiwa. Mimi nayaombea dua Mwenyezi Mungu ayatie baraka ili tufanikiwe. Lakini tuangalie sana Mhe. Spika, mimi nikiangalia Mnazi Mmoja nimepata historia yake kidogo nimeangalia. Lakini jengo lenyewe haidhuru ndio tumeambiwa kwamba litafanyiwa ukarabati. Lakini nilikuwa nasikia kwenye hotuba hapa kwamba Mhe. Spika, jengo lenyewe lina vitanda 400 naviangalia sana.

Wakati huo huo jengo lile litakuwa la rufaa litakuwa la maradhi ya aina yote; ya mripuko yatakayokuja, ya kila kitu na watu wa kawaida waingizwe humo humo. Hapo kidogo napata utata Mhe. Spika.

Kama ingekuwa tumejenga jengo la kisasa ambalo lina eneo tofauti Mnazi Mmoja tukaiacha kama hospitali kubwa tu ambayo inahudumikia wananchi wetu kwa viwango vikubwa vya bure kama malengo ya serikali yalivyo, basi lingekuwa jambo la maana sana. Lakini kwa sababu ndio zilitolewa kwamba ndio tunakimbilia muda wa kujenga hospitali kubwa mpya hatuna tunaikamata ile ile.

Je, serikali nayo imejipangaje kuhusu wananchi wake ambao wanatumia Hospitali za Wilaya na Mkoa. Hizi hospitali zitakuwa na viwango gani ambavyo vitaifikia Hospitali ya Mnazi Mmoja kipindi kile sio kipindi hichi ambacho kitakuwa cha taifa kipindi kile.

Sasa Mhe. Spika, lazima tuangalie kwamba kitu kikishaongezeka *rank* nina uhakika kwamba yale maradhi madogo madogo ya watu yatakuwa hayatizamwi. Itakuwa lazima tunaangalia mfumo mkubwa.

Mimi nimeangalia mambo mengi humu; watu,vyuo, mambo gani yatakayokuwa tunaangalia Muhimbili Mhe. Spika, iangalie Muhimbili na uiangalie Mnazi Mmoja, Mnazi Mmoja dakika tatu unaitembea, Muhimbili kama hujatembea kwa gari hufiki, eneo lenyewe la kupanua hakuna.

Sasa tunakuja kuangalia tunaingia Hospitali ya Taifa au ya Rufaa lakini na jengo lenyewe bado halijawa la kukidhi, pale hapana hata *parking*, ile *parking* ya magari hapana, mimi siioni mule ndani. Sasa tunatakiwa tujipange, tulikuwa tunaongea mambo mengi hapa baadhi ya *theatre* leo hapo tunaangalia jenereta hatuna. Hospitali kama ile kama ni ya Rufaa chini ya jenereta mbili tatu lazima ziwepo, *theatre* na mambo mengine *laboratory* za uhakika ambazo kwa kweli ni za vitu vya gharama kubwa sana. Nikiangalia huku bado tuna tatizo la kusema kwamba tunatoa huduma bure.

Hii hali inanipa matata, lakini kwa sababu waliokuwa wametangulia kuangalia wana uwezo wa kuangalia upeo tutafanyaje, tutakwenda kidogo kidogo lakini sasa na huku nyuma tusisahau, wananchi wetu tumewazoesha na tumewaambia tutawapa huduma bure. Wakati huo huo tunataka kuingia katika Mswada huu huu ambao lazima ulipiwe kwa pesa, hiyo haiwezekani bure.

Sasa hapa mambo mawili nayachangia, tunataka kukopa pesa benki, tutakuja kulipa nini. Halafu humu naangalia kwamba bajeti bado itakuwa inatusubiri ya humu humu ya kuingia kwenye masuala haya haya ya Mnazi Mmoja, wakati hii ilikuwa ni msaada wa kuitoa moja kwa moja tukaitizama nguvu zake.

Sasa Mhe. Spika, hapa nataka liangaliwe vizuri sana hili suala, tusije kufika kwa malengo mengine, pale tulipofika ikawa tumepavuruga. Hilo nataka tuliangalie vya kutosha, kwa sababu tunaingia kwenye ushindani wa kibiashara.

Mhe. Spika, huduma bora ambazo kwa kweli ndio tunatakiwa kuzitoa na hii inatakiwa kama ushindani.

Mhe. Spika, sisi tukijipanga Mnazi Mmoja, ndio nilisema ingekuwa vyema tungebagua maradhi madogo madogo Hospitali za Mkoa kama kule Pemba. Mimi Pemba nashauri sana, kwa sababu kuna Hospitali za Mkoa kama hiyo inayoitwa *Abdalla Mzee Hospital,* basi na zile za Chake chake na Wete zipandishwe ziwe za Mkoa, na hapa Unguja kama itawekwa nyengine hapa ya Mkoa ikaondoka ile ya Mnazi Mmoja ikabakia ile ili angalau hii ya Mnazi Mmoja ikaachiwa vitengo vyake vilivyokusudiwa.

Ningeishauri sana serikali, kwa hivyo kama jengo lile tunalitoa kwa suala la kitaifa basi ingetengenezwa hospitali nyengine ya Mkoa ya kukidhi haja za wananchi wa kawaida.

Mhe. Spika, tumeshawaambia wananchi wetu tutawapa huduma bure ambazo zile ndogo ndogo ndizo zinazoanzisha maradhi makubwa wakaenda India. Kwa hivyo, tukifanya hivyo tutawasaidia wananchi wetu sana.

Mhe. Spika, nataka kutoa indhari moja, tunaanzisha kitengo tutaleta madaktari kwa bei mbaya, madaktari wale huduma zao hawazitoi vizuri wanaingia hospitali za *private*.

Namuomba sana Mhe. Waziri mikataba ya madaktari hawa mabingwa muiweke vizuri, vyenginevyo itakuwa nyinyi mumepita, watu wanapita juu kama wamekosha chupa na kukupaka mafuta ya nazi, wao watakuwa wanafanya kazi Mnazi Mmoja matibabu wanatoa Hospitali za *private*. Watu hao madaktari muwaangalie vya kutosha, mtachukua madaktari bingwa Hospitali za *private* mtazineemesha. Nyinyi mtakuwa pale pale chini ambako matatizo yatakuwa yapo, kwa sababu kutakuwa hakuna vigezo vya kumbana, madaktari bingwa hawa wa *UNDP* wanaokuja wanaambiwa usifanye kazi nyengine kazi tuliyokulipia ni hii.

Leo unamkuta daktari bingwa yuko kule na jioni anakwenda Alrahma, hapo nakwambia Hospitali ya Mnazi Mmoja inakwenda na maji.

Mhe. Spika, nasemea sana suala hilo ili lisiwe jambo ambalo tunakurupuka tu baadae tukalia. Maana yake madaktari mikataba miaka mitano kifungu huna cha kumfunga, hospitali haitoi huduma. Lazima tuangalie vitu vya kutosha.

Mhe. Spika, jambo jengine mimi nimefurahika nilipoiona hii hospitali mbinu zake zote lakini bado serikali haijaacha mkono wake, na hii Dkt. Ali Mohamed Shein lazima nimpongeze, hii inakuwa Mnazi Mmoja kama vile Mhe. John Pombe Magufuli anavyofanya Mheshimiwa ngoma ikishindwa Mhe. Rais anaingia mwenyewe. Hapa kidogo nafurahishwa na hili kwa kuachia tu mkondo wa watu ukasema uweze kuongoza hii *department,* hii hatari inaweza kuja kutokea.

Mhe. Spika, kila mmoja ana mawazo yake katika masuala kama haya, lakini serikali kama serikali kwa wananchi hasa Wazanzibari sera yake ni moja afya bure na hii ni malengo mazuri.

Mimi nimeupenda huu mswada, kwa sababu najua madaktari bingwa watakuwepo, yale niliyokuwa nazungumza kwamba madaktari tunawafuata India, Israel pengine asilimia hata 50 au 40 watakuwepo hapa, najua vitasaidia sana wale waliokuwa hawana uwezo Mwenyezi Mungu atawajaalia kupata matibabu hapa, lakini na vifaa, kwa hivyo Mhe. Waziri umelitaka jambo hili kwa nia njema, lakini ujue kwamba tegemeo la wananchi pamoja na sisi ambao wametuleta hapa tumeshaingiwa na hamu kwa suala hili, kwamba kwa kweli litakuja na muelekeo mzuri, na kila mmoja aliyekuwa na kidonda chake, ana mguu wake, anasubiri hospitali ifunguliwe akilete pale. Muhimbili kidogo nayo tutaipa nafuu.

Sasa yale madhumuni Mhe. Spika, tunayofikia hapa kwamba iwe ni Hospitali ya Rufaa ikishindikana hapa Mhe. Waziri itakuwa ni jambo kubwa sana, si jambo la Muhimbili, ni jambo la kwenda nje ya dunia. Kwa hivyo, hili lengo Mhe. Spika, ningeliomba sana litizamwe.

Lakini pia nizungumze mswada mzima wa mambo ambayo nilizungumza humu ndani mna mambo haya ya maradhi ya mripuko.

Kipindi cha nyuma nilizungumza kwamba haya mambo tafiti ni sawa. Lakini hiyo hospitali mbona tumeona uwezo wake na mambo tuliyoyatwika ni makubwa, hapa kutakuwa na Vyuo Vikuu kama vile Dar- es Salaam,

Muhimbili, najua lakini bado nazungumza kwamba jengo la Mnazi Mmoja kwa vitengo ambavyo vimezungumzwa humu na eneo naliona ni dogo, sijui llakini maana yake lazima tuangalie ukweli.

Bado eneo ni dogo, na bado sijui tunaichanganya na maradhi ya kawaida. Sasa hivi ukienda pale hospitali ya kawaida nafasi hupati watu wanakwenda siku mbili nafasi hazijapatikana. Leo tunachanganya na vitengo vipya pale pale hapa Mhe. Waziri paangalie kwa nguvu sana, itakujakuwa mseto huu sasa hapajulikani maradhi bingwa, hapatojulikana maradhi ya kawaida.

Mimi ningeshauri sana ukatafuta Hospitali ambayo itakuwa ya Mkoa itakupunguzia matatizo, hapa ningeshauri sana. Ingawa tunazo hospitali lakini bado watu wana imani na Mnazi Mmoja isingekuwa wanatoka Makunduchi wanakwenda Mnazi Mmoja, lazima pana *facility* zinakuwa zimeongezeka. Kwa hivyo, zile *facilities* zilizoongezeka ungetafuta hospitali ukaibagua na hii kwa niaba ya serikali ili kuleta, pale Mnazi Mmoja hapatoshi.

Kwa hivyo, ningeshauri sana malengo yawe ya ukweli na madhumuni yake tuliyoyakusudia yawe ya ukweli. Lakini na zile jitihada zako mwenyewe Mhe. Waziri mimi nakuaminia waziri una upeo mzuri, lakini sasa tukishafika vifaa tunashindwa havinunuliki bei mbaya itakuwa bado hatujakamilika, madaktari wana bei mbaya baadae tunawaacha wanakwenda kwenye *private* Mhe. Spika, bado hapo tutakuwa hatujakamilika.

Vifaa umeongeza unataka kuweka vitu vya uchambuzi maradhi ya mripuko na kila kitu, vyote vinataka vifaa na vyote vinataka maeneo na zote ni Mnazi Mmoja na Vyuo vikuu vyengine kuna wanafunzi pale watakuja *training*.

Mhe. Spika, ningeshauri sana bado Mnazi Mmoja ungeiweka kitengo cha peke yake, maradhi mengine madogo madogo ukatafuta eneo ambalo lina uhakika wa kupunguza maradhi haya. Mimi ningeshauri sana tusiitwike mzigo Mmazi Mmoja kwa matatizo haya.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Lengo ninachokwambia tena kama tumeamua kufanya ile Mnazi Mmoja biashara mimi nakubaliana na wewe, lakini hii tusiiweke kitengo cha bure. Mhe. Spika, bure hapa haitokwenda wala hospitali haitokuwa, hapa tunayo bure na bajeti tunaitilia na bado tuna malalamiko. Pamoja na kwamba kutakuwa na nafasi za kukopa, kutakuwa na nafasi za watu

wa nje kuja kujiunga na hospitali hii, mtu wa nje atayekuja kuwekeza hatokubali hospitali iwe bure na tumeshatangaza hospitali bure.

Kwa hivyo, ningeshauri Hospitali ya Mkoa ikawekwa mbali, Mnazi Mmoja kwa watu wale wanaokwenda India wanaokwenda kuchangishana itapata nafuu tu, usafiri na mambo mengine na mapunguzo, suala hili lingependeza zaidi.

Pale Mhe. Spika, mimi nimeshaona wakati wa kipindupindu tu miaka ile ya nyuma Mnazi Mmoja hupati nafasi kwa maradhi ya mripuko, na huku ndio tunasema kwamba ndio Hospitali ya Taifa.

Mimi nashauri sana Mhe. Spika, bado Hospitali ile ya Taifa iwekwe peke yake, tutafute eneo la Hospitali ya Mkoa hapa Zanzibar kusaidia Mnazi Mmoja.

Mimi ningeshauri sana Mhe. Spika, naishukuru sana na naiombea dua, hili suala Mwenyezi Mungu alitie sura alitie moyo lifanikiwe. Mategemeo ya kila mmoja, mategemeo ya Rais wetu, zote ni mbinu za kutafuta urahisi na ulaini wa maisha yetu hasa kwa suala la afya Mwenyezi Mungu alibariki.

Nashukuru sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nimetakiwa nikukumbusheni na Mwenyekiti wa Kamati ambaye anasimamia hii hospitali kwamba pamoja na miswada ambayo mumepewa pia mumesambaziwa marekebisho ya kamati ambayo sasa changieni kwa kuzingatia na hayo marekebisho ambayo yamependekezwa na kamati vile vile.

Halafu jambo jengine Waheshimiwa mnapochangia michango yenu ielekezeni kwangu Spika kwenye kiti, msimu-*address* Waziri wala watendaji wake iwe kwangu mimi tu. Ahsante tunaendelea.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri wake na uongozi wote wa Wizara ya Afya pamoja na viongozi wote waliohusika katika suala hili, na serikali kwa ujumla kwa kuleta mabadiliko ya mswada huu, ya Sheria ya Mswada unajulikana umetangazwa katika gazeti rasmi hili. Mswada wa Sheria wa kuanzishwa kwa Hospitali ya Taifa.

Pia nichukue nafasi hii kuitakia serikali kila la kheri katika mpango mzima baada ya kikao cha bajeti kumaliza.

Mhe. Spika, mwenzangu Mjumbe alipochangia hapa aliweka wasi wasi juu ya endapo baada ya miaka mitatu hapa endapo haya yote yalikuwa matarajio yake yeye mwenyewe binafsi kwa upande wake Mwakilishi kama hayatakuwa basi baada ya miaka mitatu basi na yeye pia atakuwa mkali.

Lakini na sisi binaadamu tumeumbwa kwa kuwapa wenzetu matumaini hasa kwa serikali na hasa kwa jinsi Chama chetu cha Mapinduzi kilivyoazimia katika ilani yake kwa mwaka 2015 kuelekea 2020 na ahadi alizotoa Mhe. Rais.

Kwa hiyo, niseme tu naamini serikali pamoja na wizara husika itaweza kuyafanya yale yote ambayo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wetu hasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyoyazungumza hapa atakuja hapa baada ya miaka mitatu kuja kuwasifia na kuwapongeza.

Mhe. Spika, na mimi niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Nitaanza kwenye kifungu cha 25 kwenye kinga kinapozungumza kwamba;

"Mjumbe wa Bodi, mfanyakazi au mtu mwengine yeyote ambaye anatoa huduma za hospitali, hatowezesha kuwajisha", nafikiri hapa ilikusudiwa kuwajibishwa.

Lakini pia jana Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri anatupa historia ya hii hospitali na nilifurahi sana kwamba kwa kweli sisi Zanzibar historia ya hospitali hii tunaijua, na alipotaja hasa katika historia ya familia ya Karimjee ni familia ambayo inatajikana na wana historia kubwa hapa Tanzania, na wana historia kubwa sana katika masuala la kilimo, wana historia kubwa sana katika masuala ya biashara, lakini pia wana historia kubwa sana kuwa ni watu ambao wenye roho ya imani, wenye roho ya kutaka kuwasaidia wenzao.

Ni familia ambayo ina mengi imeyakusudia, hata hivi sasa pia wana vitengo tafauti ndani ya familia na hukutana kila mwisho wa mwaka ndugu wote kwa jumla katika maeneo tofauti duniani, na nakumbuka katika familia ya Jivanjee walifanya mkutano wao mara ya mwisho Kenya Mombasa.

Sasa Mhe. Spika, katika kifungu ambacho nilichokiangalia katika kifungu namba 5 (1)

"Kuanzishwa Bodi inayojulikana kama Bodi ya Ushauri ya Hospitali"

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu na mawazo yangu baada ya kwisha kuusoma huu mswada, na kwa upeo ninavyofahamu nigependa sana katika

kifungu hicho hicho ambacho kinasema kitakuwa na Wajumbe wawili kutoka sekta binafsi. Ambayo hapa inasema kwamba Wawakilishi wawili kifungu namba 5 (e).

Mimi ningependa sana kumuomba Mhe. Rais kupitia kwa Mhe. Waziri kwamba katika maeneo ambayo tunapohitaji msaada na sisi wenyewe pia tunafahamu familia hii na uzoefu ambao tangu ilipoanzishwa historia yake. Hasa tukiangalia hii familia ya Karimjee hawako mbali na sisi, wako Tanzania Bara na wengine huwa wanakuja hapa tunawafahamu, sasa hivi wao pia ndio wanaohusika katika biashara ya Kampuni ya *Toyota* ni ma- *agent* Tanzania na serikali pia imekuwa inanunua magari mengi kwa ajili ya matumizi hapa Tanzania.

Mimi ningeomba sana na ningependa sana kumuomba Mhe. Rais kwa nia njema kabisa, katika kuisaidia hospitali yetu katika watu ambao nawathamini mimi kwa upande wangu ambao ni wafanyabiashara wakubwa na wengine pia katika fedha zao wanaozitoa katika jamii hupenda kuwasaidia wananchi.

Mimi namuomba sana Mhe. Rais katika utekelezaji wa nafasi ambazo atakuwa nazo kwenye bodi hii, namuomba sana kwa nia njema basi awaangalie bwana Hatim Karimjee sina nia mimi, mara nyingi kutaja majina basi namtaja jina mwenyekiti wa familia hii bwana Hatim Karimjee amualike azungumze naye katika historia ya hospitali hii inajulikana pia pamoja na ukumbi wa Dar- es Salaam wa Karimjee.

Lakini katika hiyo nia njema, mikutano yao wa familia ni katika hizo *funding* ambazo wanazitoa katika mfuko ambao uko Uingereza basi amualike bwana Hatim Karimjee na kama atapenda kuungana na sisi pia kwa pamoja katika safari hii ya kuanzisha hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kama itakuwa Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja basi aje azungumze naye na aangalie tunaweza kufanya kazi pamoja naye.

Pia katika nafasi hizo hizo za sekta binafsi ambazo zimetajwa mimi pia ningependa kumuomba sana, najua kuwa si utaratibu wangu mimi kumtajia Mhe. Rais lakini kwa nia njema nafanya hivi kabisa aangalie uwezekano wa kumwita Mzee Said Bakhressa muanzilishi ambaye pia yeye mwenyewe ni kiongozi wa kampuni ya *Bakhressa Group of Companies*, azungumze naye, tunamjua mzee Bakhressa ana tabia pia ya kutoa zakka katika mwezi mtukufu wa Ramadhani na siku nyingi, lakini ningemuomba sana amwite azungumzie naye katika safari hii ya kuisaidia Wizara ya Afya, katika safari hii ya kujenga umoja na kusaidia nchi yetu, kama atapenda kuungana na sisi kisheria ili aweze

kutoa mawazo yake kibiashara. Kwa sababu ninaamini kwamba katika uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenye manunuzi na mambo ambayo wanayokusudia, lazima katika mfumo mzima wa *triangle* kutoka juu, watahitaji kuwepo na akili ya kibiashara ili aweze kuingiza ndani kufanya mambo mengi ambao wao wameyakusudia.

Mhe. Spika, na katika haya kwenye uongozi ambao utakaouweka lazima kwenye hizo *strategies* za hospitali, lazima katika maeneo ambayo yatakuwa yanahusika moja kwa moja na masuala ya fedha kwa miaka ijayo, basi ninawasihi sana katika hilo waliangalie. Kwa hivyo kwa nia njema kabisa namuomba sana Mhe. Rais wakati anaendelea kabla ya kutaka kulifanya hili, basi hao watu wawili Mzee Hatim Karimjee (Mwenyekiti wa Familia ya Karimjee) pamoja na Mzee Bakhressa, *owner of group of Bakhressa Companies* basi awaite aonane nao.

Mhe. Spika, lakini pia nataka nitoe ushauri kwenye suala zima la Bima ambalo litakuwa linahusika katika mpango mzima wa hospitali.

Mhe. Spika, hapa tunao wapiganaji wetu ambao ni wapiganaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Idara Maalum za hapa Zanzibar. Na itakuwa ni vizuri kufahamu Bima ambayo Jeshi la Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanalipa kiasi gani, wapiganaji wetu wapo wangapi na katika zile huduma ambazo wanazohitaji kwa upande wa Zanzibar, basi tuhakikishe ile Bima ya afya kama zile huduma zitaweza kupatikana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na watajua ni fedha kiasi gani wanaweza kuzipata. Basi katika eneo hilo waliangalie ili zile fedha ambazo watakuwa wanalipa kila mwaka waweze kuboresha katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, kwa sababu itakuwa ni fedha ambayo wanaipata ya uhakika.

Mhe. Spika, lakini pia naweka angalizo katika huduma ambayo watakayokuwa wanaitoa iendane na wale ambao pia watakuwa na matarajio nao. Hatuwezi kuchukua fedha za watu ikiwa huduma yetu pia haiendani na kiwango, matarajio na ndoto za watu wetu. Hiyo ni tahadhari ambayo nimeitoa.

Mhe. Spika, lakini pia nilitaka kufahamu baada ya kuangalia sheria na ninafikiria Mhe. Mwanasheria Mkuu au Waziri atatusaidia atakapofanya majumuisho. Katika mfumo mzima wa sheria hii je, tukiamua kuanzisha hospitali ndogo ndogo au kuanzisha vitengo maalumu vya utafiti na hospitali kutoa huduma, kama ikiwa serikali pamoja na Hospitali ya Mnazi Mmoja itaamua kuanzisha katika maeneo ya Idara au Kitengo cha Mifupa Tanzania Bara, ikiwa Dar es Salaam au Mikoani. Je, sheria itakuwa inawaruhusu katika

kuboresha, na kama hiyo idara watafungua hizo hospitali je, wanaweza pia ikawa ni sehemu ambayo ya kuwapatia fedha kama itakuwa ni ya utafiti. Kama ikiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja wataamua kufungua Kitengo cha Mifupa au Kitengo cha *ENT* katika maeneo ya vijijini, Tanzania Bara au Wilayani ambapo watakuwa wanapokea fedha katika huduma. Je, sheria inawaruhusu wao kama Hospitali ya Mnazi Mmoja kuweza kufanya hivyo.

Mhe. Spika, pia nilikuwa nataka kuzungumza kwenye masuala ambayo wataweka katika *strategies* zao ni kuhakikisha kwamba kwenye eneo zima la Hospitali ya Mnazi Mmoja na kufunga mkataba ambayo wanafunga kwa ajili ya kupata huduma, lakini mikataba ambayo pia watakuwa wanafunga katika kununua ardhi au kuweza kukopa au kuweza kuanzisha miradi tofauti ya kibiashara kwenye kuongeza fedha kwa ajili yao. Naomba sana katika mikataba hii wanapoweka hizo *collateral*, sheria iweze kulinda Hospitali ya Mnazi Mmoja tusikute kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja inaweza ikajikuta pahala inapigwa mnada. Sheria iilinde hospitali na mambo yote yale ya kisheria yaende katika serikali au katika wizara husika.

Mhe. Spika, lakini pia katika mpango wa mbele nilikuwa ninataka watakapoipanga kwenye mfumo wa sheria ambao wameitaja humu ndani vifungu tofauti, wajikite pia katika masuala ya tafiti ndogo ndogo na tafiti kubwa kubwa ambazo zitaweza kuwapatia fedha kwa pamoja na vitengo hivyo ni muhimu katika kujenga umoja.

Pia katika eneo moja nimeliangalia la kisheria kwamba Bodi nyingi za serikali zinampa Mhe. Waziri na Mhe. Rais kuchagua mwenyekiti pamoja na wajumbe wa Bodi wanachaguliwa pia na Waziri.

Mhe. Spika, ningependa kumshauri Mhe. Waziri kwamba katika sheria hii hii kama ataweza basi aanzishe eneo ambalo litampa fursa au nafasi yeye Mhe. Waziri ya kuchagua watu kumi ambao atawaita mabalozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja au marafiki kumi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Watu hawa wasiwe lazima wawe ni raia kutoka Tanzania, wawe ni watu ambao wanaweza kutoka katika Jumuiya za nchi Afrika Mashariki, wanaweza kutoka Ulaya, Marekani. Na pia wawe wanaweza kualikwa katika Bodi yetu; hiyo Bodi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kushiriki kutoa mawazo yao. Lakini pia katika kuwaunganisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na nchi nyengine tofauti ili katika kufanya utafiti, pia katika kusaidia kwa nia njema kwa mpango mzima wa kubadilishana madaktari wazoefu ili kujenga uhusiano mwema.

Mhe. Spika, tumeona juzi Mhe. Waziri alishiriki katika mkutano mkubwa huko Geneva na alikutana na Mawaziri tofauti katika sekta tofauti za afya. Kwa hivyo si vibaya kwamba akawa na uwezo pia kuchagua watu kumi na akaweza kuwaita marafiki wa Hospitali ya Mnazi Mmoja au Mabalozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, ikiwa sheria inamruhu ni safi, kama haimruhusu basi aangalie ataweza kufanya vipi.

Mhe. Spika, lakini pia ningependa nitoe indhari katika suala zima la kisheria kwenye mfumo wa huko mbele tunakokwenda. Ningependa nimshauri kwamba katika dawa na manunuzi ambayo yote yatakuwa yanatumika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, basi ninaomba kwenye *labelling* au kwa mfano itakuwa ni dawa ya malaria au dawa ya kukohoa ambayo inatumika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwa ni chupa basi katika kiboksi, lakini ndani ya kichupa basi sheria ambazo tutazozitunga huko mbele kuhakikisha kwamba ile dawa inaandikwa usinunue ni mali ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa dawa zozote ambazo utakazonunua katika kiwango cha aina fulani ya fedha basi ziwe tayari zina nembo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili mwananchi au mtu yeyote ambaye atakusudia kufanya wizi au anataka kufanya ubadhirifu wa aina yoyote basi mali ya serikali, mali ya wananchi au ile huduma inayotoka inakuwa na jina la Hospitali ya Mnazi Mmoja ili iweze kuwasaidia wananchi wetu hasa wananchi ambao ni maskini.

Mhe. Spika, kwa sababu inawezekana kuna tatizo la kwamba serikali inapeleka dawa, inapeleka fedha kwa ajili ya kununua manunuzi tofauti ya Hospitali ya Mnazi Mmoja lakini hazifiki zinapotea njiani. Kwa hivyo ikiwa ni dawa ambazo zinanunuliwa kutoka nje ya nchi, dawa kutoka Dar es Salaam au maeneo mengine basi zihakikishwe zinawekwa hivyo.

Mhe. Spika, lakini pia katika eneo ambalo limetajwa la *fast track* alilozungumza ndugu yangu Mhe. Mwakilishi au Meya wa Chake Chake umaarufu wake ambaye yeye anaitwa jembe. Niseme pia katika eneo la *fast track* hili ni eneo muhimu. Ni eneo ambalo lina nafasi kubwa sana na ninaamini eneo la *fast track* litaweza kutoa kiwango cha kazi...

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, ninakushukuru.

Eneo la *fast track* Mhe. Spika, ni eneo ambalo lina changamoto na ni eneo ambalo pia tunazungumzia kuhusu afya, tunazungumzia pia ni fedha. Kwa hivyo katika eneo la *fast track* kama itawekwa huduma nzuri kwa ajili ya

Wazanzibari wote wanaoishi hapa, kwa ajili ya ndugu zetu wote wanaotoka Tanzania Bara pia wanaokuja hapa, basi inawezekana tukaanza kuona mapinduzi ya kiafya Tanzania, kwamba badala ya Wazanzibari kwenda Hospitali ya Muhimbili kutibiwa, tukaona sasa watu kutoka Tanzania Bara wanakuja hapa. Lakini naomba sana Mhe. Spika, kwenye maeneo ya *fast track* watakapojipanga wasiamue kwenda kila pahala, waamue kama wanashika maeneo ya ndani kama itakuwa ni maeneo ya kwenye masuala ya tumbo, masuala ya miguu au mifupa, masuala ya *ENT*, washike sehemu moja. Isiwe kwamba huduma inayotolewa iwe huduma ya kila mara, wanataka kufanya mpaka mwisho kupasua vichwa, wanataka kufanya operesheni za moyo, wanataka kufanya sijui operesheni za miguu. Wakamate eneo moja la *fast track* ambalo watasababisha wao kuwa ni eneo ambalo wanapata pesa nzuri. Kwa sababu kule tayari kuna watu zaidi ya milioni arobaini na huduma hii pia ambao wanalipa kule Tanzania Bara ni kubwa.

Mhe. Spika, mimi nataka nione ndoto yao katika mpango mzima kwenye Bodi hii kwamba watu kutoka Tanzania Bara sasa wanakuja kutibiwa Zanzibar. Lakini pia katika suala ambalo nimelizungumza la kuunganisha marafiki kwa nia njema wawe karibu pia na *University of Dar es Salaam* na katika mafao mazima ya masuala ya madaktari.

Ningeomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwenye mpango huu katika masuala ya macho aende akamrudishe Dkt. Ahmed Atasi ambaye yuko *CCBRT*, aliyeondoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, madaktari wetu wote ambao wameondoka afanye mpango wowote katika mafao yao awarudishe Zanzibar, asiwarudishe kwa maneno, awarudishe kwa vitendo pamoja na wote waliokuwepo humu ndani.

Mhe. Spika, baada ya hayo mchango niliotoa nitamuandikia mwengine kwa maandishi. Ninakushukuru sana na mimi naunga mkono yote yaliyokuwemo. Naitakia Wizara ya Afya na Serikali kila kheri.(*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Simai Mohamed Said. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy atafuatiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bisimillahi Rahmaani Rahiim*. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu sana kila siku kwa kunijaalia uzima.

Vile vile Mhe. Spika, niende kumpongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuletea Mswada wa dharura ambao ninaamini amekaa ametafakari, ana uzoefu nao na kakaa na wahusika ambao wanalijua suala hili na karidhika na katuletea. Mimi ninampongeza sana kwa sababu anawatakia mema wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri ambao ni watendaji wazuri wa kazi. Ninawaaminia sana wanafanya kazi uzuri lakini tunawasubiri mwaka 2017/2018, kuona kazi gani wamefanya. Ninawapongeza sana kwa kazi zao nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi ningeenda kwenye *general contribution*. Sitoingia kwenye Mswada moja kwa moja kidogo nina mawazo yangu na mchango wangu.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali kubwa na ina hadhi ya kufanyika kuwa Hospitali ya Rufaa. Lakini ninachotaka kumshauri Mhe. Spika, Mhe. Waziri watu wengi wanaopata ajali huwa wengine unaweza kusema wanakufa bila ya kujitakia. Kwa sababu mtu anapopata ajali hutakiwa kwenda Polisi hasa inapotokezea ajali au suala lolote lile, kupata *RB* ile ya kwenda kutibiwa inachukua muda sana.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri wa Afya angeweka kituo cha Polisi ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili wale wanaopata ajali hawana kwenda Kituo cha Polisi Malindi au Kituo cha Mwembe Madema kuchukua *RB*, wakapewa *RB* ndani ya hospitali ile wakatibiwa mara moja. Kwa sababu tumeona matatizo mengi yanatokezea, wananchi wamo katika hali mbaya ya *emergency* lakini anaambiwa akapewe kitambulisho cha *RB* kinachukua muda na hatima yake hupoteza maisha au huzidi kuumwa kupita kiasi.

Sasa tutakapoweka Kituo cha Polisi ndani ya hospitali ile, mtu kapata ajali, kafanya tatizo lolote, ndani ya hospitali kuna kituo inatoka *RB* na madaktari wanaweza kuendelea na matibabu. Hilo ni wazo langu moja ambalo lipo nje ya mada.

Mhe. Spika, vile vile niende kwenye suala la mchango mwengine ambao sijauona ndani ya Mswada kwamba ndani ya Hospitali ya Rufaa au kwa ufupi Zanzibar nzima, hakuna kitu ambacho *presidential special department*. Hii sehemu nchi nyingi inazo hasa kwa viongozi wenye hadhi ya juu pamoja na wale matajiri ambao wanatoka nchi za Ulaya na nchi nyengine, wanapotokezewa na dharura ndani ya kisiwa chetu au ndani ya nchi yetu, sijui watakimbilia wapi kwa msaada wa dharura.

Mhe. Spika, lakini ushauri wangu ni kwamba Mhe. Waziri, wizara yake ijenge ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja sehemu muhimu, sehemu makini hasa kwenye sehemu eneo la bahari pale. Angalau sehemu yenye vyumba vinne lakini hii sehemu iwe ya watu ambao ni mashuhuri hasa kwa Mhe. Rais na viongozi wake pamoja na *investors* wanaokuja nchini wanapotokezewa na tatizo la kuumwa ghafla, wakawa wanatibiwa pale, hata chumba kiwe laki tano kwa siku basi watu wapo tayari kulipa. Kwa sababu nchi nyingi ambazo tumeona kuna vyumba mpaka milioni nne cha hospitali kwa siku, hizi ni *presidential rooms* za viongozi wa hadhi ya juu.

Mhe. Spika, ningeomba sana tuwe na kituo hichi kwa sababu litakapotokezea lolote, basi tuwe tunaweza kuwapa *service* hawa watu mashuhuri. Hii inatokana kwamba watu wengi sasa hivi pia wanaogopa kuja Zanzibar, wanasema kwamba tunapokuja hasa wale wenye uwezo, tunapotokezea na tatizo Zanzibar hakuna matibabu ya kutosha na hili lipo. Hata yeye Mhe. Spika, Mhe. Waziri kama atafanya uchunguzi ataligundua.

Mhe. Spika, niende kwenye mchango mwengine kwa sababu huu Mswada ni mrefu, mimi nitakachojaaliwa kuchangia kwa maneno nitachangia na baadae nitapeleka maandishi. Suala jengine nitakwenda kwenye gari ya *ambulance*.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri gari ya *ambulance* bado hatuna lenye kiwango, tuna ma-*ambulance land cruiser* zina bei mbaya. Lakini siyo *ambulance* ambazo zina *full equipment* ndani, tutafute gari moja *special*, hata kama mtu tunaamua kwenda kumchukua sehemu basi hafiki kwenye gari, kama kunatakiwa *oxygen* imo, kama kunatakiwa kifaa cha kushitulia moyo, maana yake kuna mpaka mashine za kupiga moyo kumshitua zinakuwemo. Lakini mimi kwenye gari zile nina hakika kwamba hakuna hivyo vifaa ambavyo vyengine vinatakiwa viwepo.

Mhe. Spika, gari hizi hazina bei ya hivyo hata akienda Uingereza. Mimi kwa uzoefu wangu gari hata *pounds* elfu thalathini, elfu ishirini na tano zipo zinapatikana na nzuri za mwaka 2014 au 2013 ambazo ni *brand new* zimetumika kilomita elfu tatu, elfu nne.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ningemuomba sana gari za aina hizi zingekuwepo japo mbili ndani ya Zanzibar ili inapotokezea *emergency* kubwa ndani ya gari mtu anatibiwa. Gari tulizonazo hazipo katika kiwango za kuwa *ambulances*.

Mhe. Spika, vile vile ningekwenda sasa kwenye Mswada nikaingia.

Mhe. Spika, mimi hospitali nimefahamu kwamba inataka kuitwa Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja. Lakini mimi ushauri tu ningependelea majina haya yafuatayo, kwa ushauri tu kama itawezekana, kuwa iitwe Hospitali Kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hilo moja. Na jina la pili Hospitali ya Rufaa ya Zanzibar. Huu ni ushauri tu.

Mhe. Spika, vile vile ningekwenda kwenye suala jengine ambalo lipo hapa linasema kutoa huduma kama Hospitali ya Rufaa na kuwepo utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya, hichi kisehemu ya pili kwenye Kifungu 4 (a).

Mhe. Spika, hii hospitali tumesema itakuwa ya rufaa lakini tutakapozungumza hapa, kutoa huduma kama Hospitali ya Rufaa inabidi sisi hatupo tayari kuwa Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ningekuomba sana sehemu hii irekebishwe kwa sababu tutakaposema ikiwa kama rufaa, inamaanisha kwamba tayari hatujajiamini kuwa ni Hospitali ya Rufaa. Kitu kama maana yake kama kina wasi wasi, lakini ilikuwa itumike Hospitali ya Rufaa, isitoe kama huduma kama Hospitali ya Rufaa. Mimi ushauri wangu upo hapo.

Mhe. Spika, vile vile ni kwenda kwenye kuwahudumia wagonjwa wa nje na wa ndani kwa mujibu wa maadili ya kidaktari.

Mhe. Spika, mimi ningeomba sana kwamba huduma inataka madaktari na madaktari kwa kweli hakuna wa kutosha. Juzi tulikuwa tuna semina na laiti Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wangekuwepo mule ndani kusingetosha, na ingekuwa bajeti yao haijapita basi isingepita kwa sababu madaktari *specialists, experts* hatuna wa kutosha, na tunakwenda kwenye Hospitali ya Rufaa. Ningeomba sana madaktari waje waongezwe wasiumizwe ambao waliopo, wale ni binadamu, kuna siku anaweza akaumwa wakatokezea na dharura, atakapokuwa mmoja hayupo basi kuna hatari ya kuja kufa mtu. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeandika lakini kuna vitu vyengine vinasababishwa kwa madaktari ambapo akiwa hayupo huyu, huyu atapata tatizo.

Mhe. Spika, ningeomba sana wanaonekana wale ambao waliopo, wapewe pia muda wa kupumzika wakawepo na wengine kubadilisha zile *timetables* zao ambazo huyu anaingia *time* gani, huyu atakuwa *time* gani.

Mhe. Spika, vile vile kuna kifungu hichi hichi cha sehemu ya pili Kifungu 4 (g) Kutoa ushauri elekezi na huduma nyengine kwa serikali, mashirika, kwa watu

binafsi kwa msingi wa maendeleo ya huduma za matibabu, matibabu ya afya ya binadamu, ustawi mzuri wa watu kwa ujumla ndani ya Zanzibar.

Huu ushauri ni mzuri kuuchukua kwa watu binafsi sehemu tofauti, lakini ningeomba sana kwamba hiyo Bodi ambayo itakayoundwa ushauri huu wakauangalia vizuri ili mambo yaende sawa. Kwa sababu kuna ushauri mwengine unaweza ukawa mzuri na ushauri mwengine ukawa mbaya.

Mhe. Spika, kuna mchango mwengine kwenye hiyo hiyo Kifungu cha sehemu ya pili 4 (k), Kutekeleza ama peke yake au kwa kushirikiana na mtu mwengine yeyote au mashirika ndani na nje ya Zanzibar katika kukuza, kuzalisha vifaa vya maabara ya hospitali, vifaa tiba na zana.

Mhe. Spika, mimi hapa kifungu hichi sijakifahamu nitakuja kumuomba Mhe. Waziri aje anifahamishe, kwa sababu hii kukuza au kuzalisha vifaa vya maabara vya hospitali. Sijui kakusudia kifunguliwe kiwanda cha kutengeneza hivi vifaa au vipi, aje anifahamishe hapa.

Mhe. Spika, vile vile hapo hapo kwenye Kifungu cha (i) Kutoa huduma za uchunguzi na huduma zinazohusiana na matengenezo na utunzaji wa hospitali na vifaa vya maabara. Hichi kifungu vile vile mimi Mhe. Spika, sijakifahamu nitamuomba Mhe. Waziri aje anifafanulie.

Mhe. Spika, nende kwenye Kifungu cha (n) Kusimamia na kudhibiti kuibuka kwa maradhi ya mripuko kwa umuhimu wa afya kwa jamii.

Mhe. Spika, hili suala tunalijua sisi vitu gani tukivifanya tunaweza tukadhibiti. Nilizungumza kipindi cha nyuma kwamba hasa ya maradhi ya kipindupindu tumegundua kwamba nyumba nyingi hazina vyoo Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri inavyotakiwa wawasaidie wananchi waliokuwa hawana uwezo wajenge vyoo, zile kwenye Shehia au sehemu muhimu vijengwe vyoo ili watu wasiende kufanya haja zao nje, kukawa kuna vyoo katika Shehia, kwa sababu tumeona kama mimi kwenye Jimbo langu sehemu ya Banda Maji nyumba karibu thamanini, tisini hazina vyoo. Sasa pale Mhe. Waziri akivijenga vyoo viwili vitatu basi watu wale wangeweza kwenda kutumia vile vyoo kuliko hivi. Kuna maradhi mengine tunayajua hasa tukifanya nini yatapungua, lakini sisi bado hatujachukua hatua za dharura.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ningemuomba achukue hatua za dharura. Vipo vyoo ambavyo unakwenda kununua tu unaviweka vile vya ma-*cabins* na vipo vyoo vya kujenga, tena ushauri nishampa ataangalia mwenyewe upi unafaa.

Mhe. Spika, vile vile nitakwenda kwenye hiyo hiyo sehemu ya pili 4, Kufanya utafiti wa dawa, afya ya kinywa, uuguzi, dawa za matibabu ya afya, binadamu na taaluma za sayansi, afya na taaluma za usaidizi tegemezi.

Mhe. Spika, huu utafiti kama hakuna vifaa utafiti huu utafeli. Mimi ningeomba Mhe. Spika, kuja kujua kuna vifaa gani ambavyo vya uchunguzi vinavyoweza kudhibiti dawa ambazo ni mbovu, mambo ambayo yatakuwa yanatokezea kwa mripuko, wataweza kuyakamata au kuyachunguza. Wana vifaa gani na eneo gani ndani ya hospitali ile vimo na ma-*scientists* gani wanao wa kuchunguza haya masuala ndani ya Zanzibar na wangapi.

Vile vile mimi ningekwenda kwenye namba 4(2) hiyo hiyo. Katika kutekeleza majukumu yake hospitali inaweza kuingia kwenye mikataba na hospitali nyengine, vyuo na taasisi. Mimi ningeomba sana suala hili liangaliwe kwenye kifungu hiki namba 2, hii mikataba mara nyingi huleta matatizo. Naomba sana Mhe. Waziri aje awe makini, ili watakapotaka kuingia kwenye masuala kama haya ya mikataba, basi ihakikishe kwamba serikali haitokuja kuingia kwenye matatizo, hasa ya kifedha na mambo mengine ambayo yatapangua ratiba.

Niende kwenye sehemu ya tatu kuhusu uongozi wa hospitali. Mhe. Spika, hii bodi itaundwa na wajumbe wafuatao; kuna wajumbe hapa karibu mpaka (f) wameelezwa. Lakini ningependekeza kwamba mimi sijaona hapa watu wenye ulemavu kuwemo katika bodi hii, sijaona kutajwa hapa, ningemuomba Mhe. Waziri katika bodi hii na watu wenye ulemavu wakawepo japo mmoja kwenye Baraza la Wawakilishi angetoka akawa ni mmoja wa wajumbe wa bodi hii.

Pia sikuona hata Mwakilishi mmoja ndani ya Baraza hili kuteuliwa kuwemo ndani ya bodi hii kuwa mwanachama. Lakini naomba sana nafasi hii ikija ikitoka nisijekupewa mimi, apewe mtu mwenye uzoefu wa udaktari. Namuomba sana Mhe. Waziri asije akanichagua mimi, ampe mtu mwenye uwezo wa udaktari, kwenye nafasi za uwakilishi watoke japo wawili humu ndani, watu wenye ulemavu pamoja na mtu wa kawaida ambaye ana uzoefu wa udaktari akawa mwanachama wa hiki kitengo, ili siku za mbele tujue tunamuhoji vipi huyo mwanachama ambaye atateuliwa.

Vile vile nije kwenye kifungu namba 6(d), Kuangalia na Kusimamia Utendaji wa Kazi. Mhe. Spika, hili suala ni muhimu sana katika hospitali hii, kwa

sababu mimi nilizungumza katika kipindi cha nyuma, ukitaka kwenda kusomea maneno ya ukorofi basi nenda kasome Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuna matatizo makubwa. Sasa kwenye huu utendaji wa kuangalia usimamizi wa utendaji kazi, huyu Mkurugenzi au Msimamizi awe makini sana kwenye kusimamia suala hili, ili kuhakikisha kwamba mgonjwa anakwenda pale anaumwa na bado anatukanwa, tunategemea tutakuwa tunamtibu mtu au tunamzidishia maradhi. Kwa hivyo, mimi naomba sana suala hili tuliangalie.

Mhe. Spika, kifungu (e), kuhakikisha mazingira ya fedha za hospitali. Suala hili ni muhimu na ni adui sana, hili linasababisha matatizo mengi. Sasa ningependa kumweleza Mhe. Waziri kwamba ahakikishe kwamba fedha za serikali zinakuwa *controlled* vizuri, hazitumiki kwenye mambo ambayo hayana maana na zinaangaliwa kwa kina kabisa.

Mhe. Spika, katika kifungu (f), kuhakikisha huduma za afya zinatolewa na hospitali ikizingatia vipaumbele vya kuwahudumia wananchi na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika...

Mhe. Spika: Dakika mbili Mhe. Mjumbe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Ahsante sana. Mhe. Spika, mpaka hivi sasa huduma za Hospitali ya Mnazi Mmoja Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naishukuru inajitahidi, lakini bado haiko kwenye kiwango kutokana na hali pengine ya bajeti na mambo mengine. Lakini namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba huduma hizo wananchi wanazipata, hasa wale wanyonge. Lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sana liangalie wanyonge, wenye pesa zao wanatafuta sehemu za kwenda, lakini hospitali ile ipo kwa ajili ya wanyonge zaidi.

Kwa hivyo, ningeomba huduma hizi ziwe nzuri, madaktari waongezwe, ma-*nurse* wawepo wa kutosha masaa 24 hakuna tatizo, na wasisumbuliwe, muhimu sana wasisumbuliwe. Sio mtu anaambiwa matibabu bure lakini anakwenda kuchezea matusi, bora akalipe sehemu nyengine.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 16 Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na majukumu yafuatayo. Hapa twende kwenye hospitali Mhe. Spika.

Mimi nimeona Wizara ya Afya inategemea misaada sana. Ningeomba sana bajeti ya fedha ya Wizara ya Afya iwe ndio muhimu inaingiziwa bajeti ya kutoka serikalini, na isitegemee misaada kwa sababu hii ni afya. Wizara nyengine zitegemee misaada kama Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na

Usafirishaji na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi zile zikategemee misaada, lakini kwenye afya suala la misaada lipungue lifanywe ni asilimia 10, lakini tumegundua kwamba Wizara ya Afya inategemea misaada kwa asilimia 80, bajeti haitoshi.

Mimi sitoendelea sasa hivi, nau-*support* mswada huu mzuri, naomba na utendaji wa wizara yake uje uwe mzuri. Lakini yaliyobakia naweza kuchangia kwa maandishi. Mimi nau-*support* mswada huu asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, nina tangazo moja la mgeni. Mgeni aliyepo ni wa Mhe. Omar Seif Abeid ni ndugu Khamis Seif Ali yule pale. Huyu ni Katibu Mwendeshaji wa Baraza la Mji la Wete ambaye pia ni Katibu wa Club ya Mwenge, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaendelea, sasa namwita Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa imani yako na kwa kunipa nafasi hii saa hizi.

Kwanza niseme nimpongeze sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutuletea mswada wa dharura, lakini vile vile nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na kupitia kwa watendaji wake wote ambao wamekaa na kutuletea mswada huu muhimu sana.

Mhe. Spika, nasema mswada huu ni muhimu sana kwa sababu ndio mkombozi wa wananchi wa Zanzibar. Nina sababu nyingi sana Mhe. Spika, kusema kwamba mswada huu ni muhimu na ni mkombozi wa wananchi wa Zanzibar.

Moja katika sababu hizo wananchi wengi walikuwa wanakosa huduma muhimu sana katika hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini sasa huu ndio utakuwa ukombozi wao. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tutunge mkono mswada huu, ili tuwape watendaji wakatekeleze majukumu yao.

Mhe. Spika, niende sasa kwenye mswada moja kwa moja kwenye Sehemu ya Kwanza. Mhe. Spika, mswada huu kwenye Sehemu ya Kwanza umekamilika, na niseme tu hauna doa lolote la kuweza kuongoza au kupunguza. Katika idara zote ambazo zimepangwa hapa ni idara muhimu sana, na vyote ambavyo vimeorodheshwa vimetekelezeka.

Mhe. Spika, niende katika Sehemu ya Pili, kuanzishwa na kazi za hospitali. Mhe. Spika, nimeangalia sana uanzishwaji huu wa hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa. Vile vile nilikuwa nikipata mashaka sana kuona kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio itakuwa wakala. Nilipitia nchi zaidi ya saba ambazo zina *Corporate Board*, nchi hizo naomba nizitaje hapa, nimepitia Tanzania Bara ambayo imeanzisha *Muhimbili National Hospital*, nimepitia Kenya ambayo imeanzisha *Kenyatta National Hospital*, nimepitia South Africa, nimepitia Abuja Nigeria, nimepitia na Zambia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hawa wote walifanikiwa sana, lakini wao walikuwa wameweka *corporation*, lakini yetu inakuwa *agent*. Lakini nikasema kwa nini inakuwa *agent* yetu au serikali imekusudia nini kuweka *agent*, nimegundua tunapishana kisera. Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu mwaka 1964 ni matibabu bure, sasa hapa ndipo tulipokosana. Lakini nasema tuipe nguvu tuone, sheria hii tukiipa nguvu tutakwenda kule tunapotaka, zile kelele za rafiki yangu sana Mhe. Jaku Hashim hapa zitapungua, na tutakwenda katika hali nzuri, tuone basi wananchi wetu wanakwenda katika matibabu ambayo wanayataka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme moja katika hili. Hapa kwenye hospitali hii, anasema hospitali itatekeleza kazi zake kwa ushauri wa Bodi na usimamizi wa waziri. Mimi mwanzo nilikuwa napata ukakasi mkubwa sana, kwa nini tumuweke Mhe. Waziri awe juu ndiye ashauri, tusiweke tu Mwenyekiti wa Bodi. Lakini bado nataka niseme katika sheria hizi tunazokwenda nazo, waziri bado ana mamlaka makubwa sana ya kuwa yeye ashauriwe na bodi na yeye ndiye awe *head* katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika, nije kwenye kifungu cha (h) katika ukurasa wa 27, anasema kutoa huduma kwa ajili ya sehemu ya kituo cha kujifunzia mafunzo na utafiti katika taaluma za sayansi, anatomia, maumbile ya binadamu, patholojia na masomo mengine yanayohusiana na haya. Nadhani kila mjumbe anao mswada huu atauona.

Mhe. Spika, niseme tu kwanza tuna tatizo la *mortuary* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. *Mortuary* yetu ni ndogo sana, kama inachukua basi ni maiti wanne tu au watatu, hisia zangu mimi. Sasa tunaweza tukafanya kama tulivyoona huku mbele kushirikisha na hivi vyuo au skuli za afya zilizokuwepo, itatupa tabu sana kuna mambo mengi wanafunzi wanataka kujifunza. Kwa hivyo, niiombe sana serikali ijitahidi kwa uwezo wake kujenga *mortuary* kubwa ili basi kuweza kuwapa nafasi hata hawa wanafunzi kufanya mambo kwa vitendo.

Mhe. Spika, kuna *post-mortem* zinafanyika, sasa kama ni ile tu haifanyiki. Kwa hivyo, niombe sana Mhe. Waziri pamoja na sheria yako hiyo itayokwenda, tunakuomba uongeze *mortuary* ili kuona upasuaji wa vitendo kwa wanafunzi unakwenda sawia.

Vile vile Mhe. Spika, katika kifungu cha (k) kwenye ukurasa huu huu, utekelezaji ama peke yake au kwa kushirikiana na mtu mwengine yeyote, au shirika la ndani au nje ya Zanzibar, kukuza na kuzalisha.

Hapa mimi nataka niongeze tu Mhe. Spika, na naomba nilete marekebisho kidogo kwa uono wangu mdogo sana. Nasema hapa tuongeze kukuza na kuzalisha dawa na zana za vifaa tiba na elimu ya afya na kinga, ili tuweze kuongeza. Naomba nitaleta marekebisho hayo kama wenzangu wataniunga mkono ili tuendelee pamoja.

Mhe. Spika, vile vile niende kwenye kifungu cha (n) kusimamia na kudhibiti kuibuka kwa maradhi ya mripuko wa umuhimu wa afya ya jamii.

Mhe. Spika, hapa pia nina marekebisho madogo sana. Nataka kusema kusimamia na kudhibiti kinga ya maradhi, kwa sababu kuibuka ingawaje hospitali ikiwa ya rufaa inakuwa na mikono mingi katika Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa, lakini sio kazi yake kudhibiti. Sasa ningemuomba hapa Mhe. Waziri nilete marekebisho madogo ili kuona kama yatakubalika basi tuweze kwenda sawia.

Mhe. Spika, niende kwenye Sehemu ya Tatu, sehemu ya uongozi wa hospitali. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuileta hii kubwa sana. Lakini nasema kwenye sifa zote ambazo zimeanzishwa hapa, tusimpe *loophole* kubwa sana Mhe. Waziri kwa kuteua tuseme tu basi, pamoja na wote waliochaguliwa kwenye sehemu hii ya uongozi, tuweze kumchagua na mfanyabiashara mmoja katika bodi hii itapendeza zaidi, huo ni ushauri wangu tu, ili kuona basi wigo unatendeka, kwa sababu tunadhani tutaweza kuweka mfuko wa pekee katika kuanzisha, ili tuone basi mfuko huu wanachanga watu mbali mbali na kuona tunapata dawa, tusije tukakosa chanjo kama zile tulizozikosa muda mwingi.

Mhe. Spika, nirudi tena kwenye ukurasa wa 30 kwenye *margin* hii inayoitwa posho. Wajumbe wa Bodi watapaswa kulipwa posho kwa kadiri itakavyoamuliwa na waziri. Mimi nadhani tuweke kidogo tuweze kumbana waziri, waziri anaweza akawapa posho ndogo na hii ndio hospitali ya rufaa, atakavyoamka ndivyo atakavyoona. Sasa tuseme tu kwa kushirikiana na bodi

au Mwenyekiti wa bodi ili washauriane pamoja kwa kuona maslahi ya nchi hii yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, kwa nini niseme hivyo, kwa sababu tulianzisha *fast track* kwa nia njema kabisa, lakini *fast track* ile sasa hivi imekuwa na maudhi makubwa na maudhi yenyewe sio kwa wafanyakazi, ni kwa sababu ya huduma duni ambazo tunazipata pale. Lakini tukianzisha hivi na bodi hii ikiwepo inaweza ikamshauri waziri wakaweza kuweka *fast track* kubwa, nzuri na tukapata matibabu yaliyokuwa mazuri.

Mhe. Spika, nadhani unaelewa wazi sasa kuwa watu wengi wamekuwa wanaacha hospitali Zanzibar na wanakimbilia Dar es Salaam, hawakimbilii kwa kutaka, wanakimbilia kwa sababu huduma duni zilizopo hapa. Lakini tukianzisha hospitali yetu ya rufaa, tukianzisha bodi yetu hii itakayomshauri waziri, itakayoleta mambo mengi katika serikali na ikiwa ndio wakala wa serikali, basi tunaweza tukafanikiwa sana na *fast track* ile itakuwa ndio kimbilio letu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 32 kwenye kifungu (f), katika hizi idara ambazo zimetajwa, anataja Idara ya Huduma za Uchunguzi wa Afya. Sasa mimi nilikuwa nataka niongeze tu, katika Idara ya Huduma za Uchunguzi wa Afya na Maradhi, kwa sababu tunafanya *medical examination* au *medical check-up*, lakini wale wanaofanya *medical check-up* ndio wale ambao wako vizuri, ndio tunasema uchunguzi wa afya, sasa hawa wagonjwa tutasema wanaanza afya, kwa sababu afya tayari zimeshakuwa na mgogoro. Tuweke tu Mhe. Waziri kama utaniridhia, tuweke Idara ya Huduma za Uchunguzi wa Afya na Maradhi.

Mhe. Spika, niende kwenye hii namba (2) katika kifungu cha 18. Anasema, Wakurugenzi watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji katika utekelezaji wa majukumu yao. Mimi nilikuwa nataka kutoa rai tu, labda watu hapa inaweza kuingia *contradiction* hawawezi kujua hawa Wakurugenzi, kwa sababu sifa za Wakurugenzi ni wale ambao Mhe. Rais anawateua. Lakini nilivyofahamu mimi kwa ufahamu wangu mdogo hapa, Wakurugenzi wale wa ndani wa idara zile ambazo tulizitaja hapa juu. Idara ya Dawa, Idara ya Utaalamu wa Afya ya Binadamu, Idara ya Huduma za Maabara, wale wawe ndio Wakurugenzi ambao, hawana sifa ya kuchaguliwa na Rais, lakini wamechaguliwa na bodi yenyewe ili wawe Wakurugenzi wa ndani. Isije ikafahamika vyenginevyo, kwa sababu tukisema Wakurugenzi hawa walioteuliwa na Rais, hata kima cha mishahara yao kitakuwa kikubwa na tutawaongezea *burden* ya mishahara katika hospitali hii.

Mhe. Spika, nije kwenye namba 19, niende haraka haraka. Katika yote waliyotaja, Kamati ya Uongozi itakuwa na wajumbe wafuatao; Lakini (e) inasema, itakuwa na mlezi wa hospitali. Mimi nataka hapa tutamke wazi mlezi wa hospitali, wengine hawawezi kumjua ni nani, aidha awe *Chief Nurse Officer* au awe *Matron,* katika hao mmoja tuambiwe ni nani. Kwa sababu unapotamka tu mlezi hakuna mtu atakayemjua tu mara moja.

Mhe. Spika, nadhani sasa maabara imekuwa inasaidiwa na *East African Support* kwa kuleta *reagent,* na inatumia si chini ya milioni 60 kwa mwezi, ili kuweza kutusaidia na sisi tunatakiwa tupate *quality laboratory* na *quality standard* ambayo inaweza ikawepo. Lakini niseme huu ndio muongozo wetu. Mhe. Waziri unapokuja hapa angalau uweze kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe, ni nini *quality laboratory*, ni nini *standard* ambayo inaweza kupatikana. Nadhani ikiwa tutapata *reagent* hizi kwa wingi, basi tunaweza tukatekeleza vipimo vyetu kwa hali ya juu sana.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Spika, nimekuona huko, waukubali mswada huu, mswada huu ni mzuri sana na unaweza ukatupeleka pahala pazuri tunapopatarajia, niwaombe sana. Lakini kabla ya kumalizia Mhe. Spika, niseme tu, ingekuwa ni vyema sana kama tungeiwacha hospitali ya Mnazi Mmoja, nadhani kuna kiwanja kimeshasemwa sana Binguni tungekwenda tukaanzia kule. Lakini kwa kuanzia tu nimuombe waziri tuanze moja, tuanze hospitali au tuanze sheria hii, atwambie nini kimoja, nini kinatakikana.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa). Naomba kumwita sasa Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei) na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika kuupitisha mswada huu, wa kuanzishwa kwa Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja.

Nitangulie kutoa shukrani na pongezi kwa Mhe. Waziri wa Afya aliyetuwasilishia mswada huu kwa ufasaha wake. Lakini vile vile niipongeze Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa kuweza na wao kutoa michango yao ya marekebisho ambayo imesaidia katika kuweka mswada huu kwenye hali nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niwapongeze vile vile wajumbe ambao wamechangia mswada huu kwa ufasaha sana. Pia nitoe pongezi za dhati sana kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweza kufikiria kuleta Mswada huu kuwa wa dharura katika Baraza hili, kutokana na umuhimu wa kuwa na Hospitali ambayo itakuwa na huduma muhimu na za lazima kwa Wazanzibari, kuweza kuwarahisishia zile huduma za afya ambazo wanazihitaji.

Mhe. Spika, Mswada huu ni mswada mmoja muhimu sana, na mimi bila ya kupoteza wakati nataka nielekee katika michango yangu midogo midogo katika kuufanya mswada huu kukaa vizuri zaidi.

Nije kwanza katika sehemu ya pili ya Mswada huu kifungu cha 4(p) na kifungu cha 4(q).

Kifungu cha 4(p) Mhe. Spika, nilikuwa napendekeza napenda ninukuu kidogo" Kushirikiana na vyuo vilivyoanzishwa ndani ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Chuo chengine chochote kitakachotambulika kutoa elimu na mafunzo...". Hapa nilitaka liingizwe neno Chuo Chochote nje ya Zanzibar au nje ya nchi kwa sababu tayari kuna Zanzibar na Jamhuri ya Muungano, kwa hivyo ili kuweka mawanda makubwa zaidi tunaweza kushirikiana na vyuo hata nje ya nchi ya Tanzania.

Tukienda kwenye kifungu 4(q) kinasomeka napenda ninukuu. "Kuendesha, kujenga, kuandaa, kutunza, kuhifadhi na kufanya". Napendekeza hilo neno kufanya lisomeke kuzifanyia matengenezo mali zake na sio kufanya matengenezo mali zake.

Mhe. Spika, niendelee na michango yangu midogo midogo kuna suala hili la *consistency* ya maneno Mwakilishi, kuna sehemu nyengine iko muwakilishi kuna sehemu nyengine Muwakilishi kwenye kifungu cha 5 namba (2) napenda kuwe na *consistency*, hayo maneno kama tunakubali kuwa Mwakilishi iwe Mwakilishi kwa yote, na kama tunakubali Muwakilishi basi Muwakilishi kwa yote.

Vile vile *consistency* katika maneno hospitali napenda wayapitie Hospitali kuna (i) kuna mengine hospital, kwa hivyo kuwe na kitu kimoja kama ni hospitali basi iwe li na kama hospital basi tukubaliane kwamba iko l.

Mhe. Spika, nikiendelea na michango yangu midogo midogo tukija kwenye kifungu cha 8 (f) nilikuwa napendekeza hapa napenda niseme. "Kuhakikisha

huduma za afya zinazotolewa na hospitali zikizingatia vipaumbele vya kuhudumia wananchi na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika".
Napendekeza paingizwe neno huduma hizo zinapatikana kwa wakati na kwa uhakika, kwa sababu kuna wakati wa kuzorota unaweza ukawa na mgonjwa wako lakini akazorotoshewa kupata zile huduma, lakini huduma zikatolewa kwa uhakika kwamba katibiwa lakini ule uharaka na unapokuwa na mgonjwa unatarajia kwanza kupata huduma za haraka. Kwa hivyo hili neno la haraka na uhakika nafikiri lingesomeka vizuri zaidi.

Mhe. Spika, nije kifungu hicho hicho cha 8 (h) kwenye kifungu cha (h) kuhakikisha kuwa Hospitali inatekeleza wajibu wake kwa Wizara, kuna kifungu kinasomeka hivyo, hili neno Wizara hapa kwa sababu halikutolewa ufafanuzi mwanzo kwa hivyo linakuwa lipo tata sana, ningependa liwe wazi kwa Wizara ya Afya, *otherwise* liwe limetolewa maelezo awali, kwamba Wizara itakapoonekana katika hiyo Sheria basi iwe ni Wizara ya Afya, vyenginevyo inaweza ikawa haiko wazi.

Mhe. Spika, niendelee kwenye kifungu cha 15 (1) kuna *mistake* hapo ya neno Mkurugenzi linasomeka Mkurugeni, kwa hivyo napenda lisomeke Mkurugenzi lakini neno ikiwa ambalo limemalizia hiyo *statement* basi hili likae vizuri lisomeke akiwa, kwa hivyo inaendelea akiwa ni Mzanzibari sio ikiwa.
Lakini tukija kwenye kifungu cha 16 (1)(a) Kuongoza mambo ya Hospitali na kutoa huduma bora na zinazojitosheleza. Mimi napenda hilo neno zinazojitosheleza lisomeke zinazotosheleza sio zinazojitosheleza, zinazotosheleza.

Kifungu 16 (b) Kusimamia mapato, Matumizi yanayotolewa hili neno yanayotolewa napendekeza isiwe yanayotolewa lakini yanayofanywa na Hospitali, sio yanayotolewa na hospitali, matumizi hayatolewi yanafanywa.
Mhe. Spika, sasa nije kwenye kifungu cha 17(1) Kuanzishwa idara za Hospitali ambazo, ambayo inasomeka Hospital ambazo zitakuwa kama ifuatazo, napendekeza ilo neno lisisomeke hivyo lisomeke aidha zifuatazo au ifuatavyo, maneno mawili hayo mojawapo linaweza likakaa vizuri zaidi kuliko neno ambalo lipo hapo.

Mhe. Spika, niendelee katika kifungu cha 18 neno masharti linasomea asharti kwa hivyo ningependa hiyo m iwepo hapo kifungu cha tatu hicho, ambacho kilikuwa kinasema Mkurugenzi aliyeteuliwa chini ya (a) asharti na isomeke masharti.

Kifungu cha 19 (2) hii namba mbili imejitokeza vifungu viwili, kwa hivyo hicho kifungu ambacho ni namba mbili cha pili kiwe ni kifungu cha namba tatu ambacho kinasema. "Mwanasheria wa Hospitali atakuwa Katibu wa Kamati". Lakini vile vile kama Mwanasheria wa hospitali atakuwa katibu wa kamati kwa nini asiingie hapa awe ni kifungu cha baada ya d (f) e, f, g Kwa nini asiwe g halafu akaainishwa tu kwamba yeye ni mjumbe wa kamati awekwe kwamba ni Mwanasheria lakini mbele awekwe kwamba ambae atakuwa ni katibu, nafikiri ingependeza zaidi.

Mhe. Spika, nije kwenye *consistency* ya neno utaalamu mwahali mwengine mnasomeka utaalam, mwengine utaalamu au kama kuna wataalamu, wataalam napenda kuwa na muundo wa aina moja hilo neno na nafikiri muafaka iwe wataaalam au utaalam na sio utaalam.

Mhe. Spika, sasa nioneshe wasi wasi wangu juu ya hiyo hospitali kuonekana kwamba itajitegemea, suala la mwanzo kwamba kuna madeni ambayo yanaachwa na Hospitali au Wizara ya Afya katika hospitali hii. Madeni haya kwa mujibu wa Mswada huu ni kwamba yatarithiwa na hii hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja, sasa sina hakika kwamba hivi sasa deni liko kiasi gani, kwa sababu kama tunataka iwe ya kujitegemea halafu ikaja ikarithi madeni mengi maana yake kazi yake ya mwanzo itakuwa ni kuweza kulipa madeni. Kwa hivyo niiombe sana Wizara hii kabla ya kupitisha mswada huu kuweza kutathmini haya madeni, na kama ni makubwa basi ifanyiwe tahafifu au isamehewe ili ikianza kazi zake basi isiwe ina madeni ya kuweza kulipa.

Vile vile wasi wasi wangu mwengine wa kuifanya iwe ya kujitegemea hili suala la huduma bure au afya bure hili Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi nalo sana, kwa sababu hivi sasa tuna suala la elimu bure, kwa kweli lina changamoto nyingi sana maskulini, sasa nina wasi wasi na hii huduma ya afya bure katika hii Taasisi, mimi naona tunaweza tukaja tukawa na neno tu la afya bure lakini utekelezaji wenyewe haufanikiwi. *Otherwise* ningeishauri Serikali kama ni ruzuku ambazo zitaingizwa katika taasisi hii basi ruzuku hizi ziingie kwa wakati, na ruzuku hizi ziwe zinatosheleza haja ya kuwa hospitali hii kuwa ni hospitali ya rufaa.

Vile vile uongozi wa hospitali hii kuwa na ubunifu katika kutafuta vyanzo mbali mbali vya mapato, lakini vyenginevyo tu tukikaa bila ya kuwa wabunifu basi tutakosa kuwa na fedha za kuendeshea hospitali hii na kuonekana kweli kama ni hospitali ya taifa au hospitali ya rufaa.

Mhe. Spika, sasa nije katika kipengele cha madhumuni na sababu ukurasa wa 34 kuna aya haiko vizuri ambayo inasomeka kwamba. "Mswada huu wa Sheria unakusudia kuunda halafu kuna neno wakala kuunda wakala wa Serikali". Mimi naona kama isomeke kuunda chombo ambayo hiyo chombo imeshajitokeza huku chini, chombo cha wakala wa Serikali. Napenda waitazame hivyo jinsi gani hiyo *statement* itakavyokaa vyema.

Vile vile aya ya pili inasomeka hospitali inayoanzishwa inatoa huduma kama rufaa, hili neno kama sijui kama liko sawa, naomba litazamwe mimi nilikuwa naona kama pawe na za huduma za rufaa.

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, nimalizie katika ukurasa wa 25 kwenye Sehemu ya Nne ambayo mwisho wake ilikuwa inasema Hospitali na uhamishaji wa wafanyakazi, hichi kipengele kwa ufupi kilikuwa kinafafanua sehemu ya nne jinsi ilivyo ndani, lakini huku ndani mimi sikuona suala zima linalohusiana na uhamisho wa wafanyakazi. Kwa hivyo naomba Waziri akija basi atuoneshe kipengele gani ambacho humu ndani kilikuwa kinahusiana na uhamihso wa wafanyakazi.

Mwisho Mhe. Spika, katika suala la wafanyakazi hospitali hii au mswada huu kabla ya kuanzishwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ina wafanyakazi, na wafanyakazi watakaokutwa na mswada huu ina maana hao watakuwa ni wafanyakazi katika hii taasisi ya rufaa, ningependa sana Mhe. Waziri, kabla ya kuanzisha mswada huu kuweza kuwachunguza wafanyakazi ambao hivi sasa wapo na wale ambao hawafai, kwa sababu kuna wafanyakazi hawafai, hawafai kimaadili katika kazi zao lakini hawafai vile vile uwajibikaji wao.

Mimi ningependa sana kabla ya kuanzisha hao watu angewafanyia uhamisho kwenda katika maeneo mengine ili wasije wakaanza na chombo hichi ikiwa kama ni uzoefu unavyojionesha hivi sasa, Lakini vile vile wale watakaobakia pamoja na kutumia hii sheria ya utumishi wa Serikali basi vile vile maslahi yao yaweze kuangaliwa vizuri, kwa sababu bila ya maslahi mazuri tusitarajie kwamba watakuwa wawajibikaji na huduma nzuri zitapatikana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa nafasi hii na mimi naupongeza na kuupa *support* mswada huu upite ili kuanzisha taasisi hii, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Hamad Abdalla Rashid : Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu wa Wizara ya afya na nafurahi kwa sababu na mimi niko kwenye hii kada ya afya.

Mimi kwanza nimpongeze Mhe. Rais, kama walivyompongeza wenzangu kuniletea mswada huu wa dharura, na kama walivyotangulia kusema kwamba utakuwa mkombozi kwa wananchi wetu katika upande wa afya.

Mhe. Spika, mtoto akizaliwa hatutegemei kwenda kwa siku moja, na wenzangu wanapata mashaka sana wanaposikia hospitali ya rufaa, mimi nasema kwamba rufaa hata Apollo ile ya India ni hospitali ya rufaa lakini bado pale wananchi wanakufa na hospitali yenyewe bado ina-*refer* tena wangonjwa kwenye mahospitali mengine. Sasa tusiwe na dhana kwamba tutakapoita ile ni hospitali ya rufaa wananchi wetu hawatokufa, muhimu ni kupata huduma bora ambayo itapanua wigo kwa kusaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, uwepo wa hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja kama alivyotangulia mwenzangu Mhe. Dimwa kusema kwamba utawasaidia wananchi wetu, na mimi naunga mkono na nampongeza Waziri pengine kwa kumshauri Mhe. Rais kuuleta haraka haraka mswada huu wa dharura, kuna mambo tu ya kuzingatia na iwapo mambo haya tutayazingatia vizuri kwa haraka kabla ya mswada huu kupitishwa basi bado tutafanikiwa sana katika kuhakikisha kwamba hospitali yetu hii ya Mnazi Mmoja inakuwa hospitali bora ya rufaa katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, na mimi nije kwenye upande wangu hasa nazingatia hichi kifungu nambari 8(f) kinasema kwamba. "Huduma za Afya zitakazotolewa na hospitali ikizingatia kipaumbele cha kuhudumia wananchi na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika".

Kupatikana huduma za afya kiuhakika katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ndio njia pekee itakayoweza kuwasaidia wananchi, na uhakika upi basi kwenye waraka huu wa mswada tumeelezwa kwamba hospitali itakuwa chini ya Bodi.

Sasa Bodi hii itakaposimamia vizuri utendaji wa wafanyakazi na kazi zenyewe, basi ndipo pale ambapo itaondoka ile mgonjwa kufika hospitali saa moja daktari akaingia saa nne, ni jambo la ajabu mgonjwa kufika saa moja daktari akafika saa nne, sasa hii bodi itasimamia vizuri pale kuhakikisha kwamba daktari naye saa 12.30 yupo anasubiri mgonjwa. Sio mgonjwa aje hospitali kusubiri daktari.

Mhe. Spika, kwa kutekeleza haya yafuatayo basi mimi naona tutafanikiwa kabisa kuwa na hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja bila ya woga. Kwanza majengo yarekebishwe yatakaporekebishwa majengo ya Mnazi Mmoja na kuhakikisha kwamba vitengo vyote vinavyohusu huduma za afya vipo pale, hiyo itakuwa sehemu moja.

La pili wafanyakazi wa kada zote wakianza wauguzi, nesi, *orderly*, wauguzi wasaidizi, Madaktari, Madaktari bingwa wa fani zote kwa mfano wawepo mpaka wachunguzi *Lab Technician, neurologists, oncologists, pathologists, psychriatricits, radiologists, pediatric nurse, pediatrician, gynecologists,* wa kutosha na sio mmoja. Angalau kila kitengo kwa kuanzia tuwe na watatu, yaani akiondoka huyu mwengine awe yupo, basi hapo tutaanza kupiga hatua ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma bora zile ambazo tunatarajia tukiita kwamba ni hospitali ya rufaa.

Mhe. Spika, vitendea kazi kama nilivyoanza kwanza kusema majengo sasa naingia kwenye vitendea kazi. Hivi vitendea kazi vikiwepo vya aina zote na tutakapoacha yale malumbano ya hapa mara hichi hakipo hichi hakipo, nikianza na vitendea kazi vya uchunguzi na hotuba ya wenzetu wa kamati walisema kwamba tunakabiliwa na upungufu wa vifaa vya uchunguzi. Sasa katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kama tutaweza kutekeleza hilo na naamini kwa sababu hospitali inapokuwa ya rufaa wahisani wengi sana wanapenda kuja pale, aidha kwa kutoa misaada au kuhakikisha huduma bora zinatolewa, watakuwepo kwa wingi. Sasa hili lisitufanye kuwa woga, hospitali ya Mnazi Mmoja itapokuwa Hospitali ya Rufaa itaweza kuvutia wawekezaji wengi, wahisani, mabingwa wengi kuja pale kutoa huduma kwa wananchi na hospitali yetu itaweza kujitegemea angalau basi wale watendaji ni hospitali au bodi yenyewe itapokuwa na uwezo wa kujipangia, mabingwa hawa au bingwa huyu malipo yake ya mshahara uwe huu, ili kumfanya asiinue mguu katika hospitali na aweze kutoa huduma bora kabisa.

Hata wauguzi wetu hospitali ile itapokuwa ya kujitegemea haidhuru ina mawakala wa serikali itakuwa bado ina uwezo wa kupanga mikakati yake ya kuweza kuwapa vipaumbele hata wauguzi kuwaongezea mishahara hospitali ile, na ndipo utapokuwa ule utendaji wa kazi. Lakini tuje tuache ile blaa blaa, mimi Mhe. Spika, nimesoma Muhimbili pale, nimesoma mpaka nimemaliza pale sijamuona mtu anaitwa *Clinical Officer.*

Mhe. Spika, sasa nashauri Mhe. Waziri tusije tukaanzia hapo hospitali ya rufaa tukaanza na watu wanaitwa ma-*clinical officers* wale bado ni wa vijijini, pale tuanze na madaktari kuelekea madaktari bingwa ili wananchi wetu

wataposhindwa huduma huku katika hospitali zetu ndogo ndogo wakienda pale wanapata huduma ya uhakika.

Mhe. Spika, kwa kumalizia mimi naiomba Wizara kwa kupitia kwako Mhe. Spika, tumechelewa ile hospitali kuifanya Hospitali ya Rufaa, na kwa sababu labda tulikuwa na wasiwasi au woga. Kama nilivyosema mwanzo mtoto hazaliwi siku moja akaenda, ile itakapoanza kuitwa Hospitali ya Rufaa yenyewe itajiendesha na itaondokana na hii lawama ya kiwango kidogo ya bajeti inayopewa Wizara ya Afya kwa sababu hospitali itakuwa inajitegemea itakuwa na uwezo wake, sasa hizo lawama ndogo ndogo tutakwenda kwenye hospitali zetu ndogo lakini ile hospitali ya rufaa itakuwa ni hospitali ambayo inajitegemea na kuweza kufanya mambo yetu haya yote. Lakini pale itakapokuwa na usimamizi wa uhakika bodi iwe na uwezo na nguvu na Waziri mwenyewe akihakikisha kwamba utendaji wa kazi katika hospitali ile unakwenda sawia na vile ambavyo kakusudia katika mswada huu, bila ya hivyo tutakuja kuwa hospitali ya rufaa ambayo tunawaogopa watendaji hakuna zile *access* na *interests* za wafanyakazi wa Wizara ya Afya lazima zile zizingatiwe kwanza Mhe. Waziri ziwepo, ili utendaji wa kazi katika hospitali ile uende vizuri inavyotakikana.

Mwisho mimi nasema kwamba hakuna lisilowezekana, tunao uwezo wa kuhakikisha tunakuwa na hospitali bora ya rufaa ndani ya Zanzibar yetu na huu ndio mwanzo. Nawatakia utendaji mwema, naunga mkono mswada huu. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji wa mswada huu mzuri kabisa wa Wizara ya Afya unaolenga kuwepo kwa Hospitali ya Rufaa hapa Zanzibar. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kusimamia sana kuwepo kwa hospitali hii pamoja na kusimamia mambo yote ya maendeleo ambayo tunayaona katika nchi yetu. Ni imani yangu kwamba hospitali hii ya Rufaa ya Zanzibar na hasa ukilinganisha na uwezo mkubwa wa wazanzibari wa kufanya mambo makubwa ya maendeleo yanayojulikana duniani mwingi sana wazanzibari wanapata sifa, na hivi karibuni tumeona tumeweza kupiga vita malaria na imefikia chini ya asilimia moja. Kwa hivyo nina imani sana kwamba uendeshaji wa hospitali hii utakuwa wa mfano, Tanzania, Afrika Mashariki, Afrika na Duniani.

Baada ya kusema hayo nianze sasa kutoa mchango wangu. Kwanza katika jina la hospitali, tukizingatia mchango mkubwa sana wa Rais wetu katika kuleta maendeleo mimi napendekeza hospitali hii iitwe *A.M. Shein Referral Hospital*

Mnazi Mmoja. Hili jina la Mnazi Mmoja lije chini pale, lisitoke lakini ianze iwe *A.M Shein Referral Hospital* Mnazi Mmoja Zanzibar.

Baada ya kutoa pendekezo hilo nakwenda tena kwenye changamoto kwanza ambazo zinakabili uanzishwaji au uendelezwaji wa hii Hospitali ya Rufaa.

Kuna changamoto kubwa sana ya sera, sera kwa kiwango kikubwa haijaweza kuweka bayana mifumo ya kutosheleza mahitaji ya afya kwa ngazi mbali mbali katika maeneo mengi ya visiwa vyetu, hiyo changamoto ya kwanza kwa sera.

Halafu changamoto nyengine imetajwa na wengi hapa kuna uhaba wa wataalamu wa kada mbali mbali na hiyo baadae nitapendekeza tena, niliwahi kupendekeza nitapendekeza zile nyanja ambazo zinaweza zikatusaidia.

Ya tatu kukosekana kwa vivutio (*incentives),* najua unaweza kumpa kivutio kizuri mwanadamu bahati mbaya akakiona cha kawaida akaona kama si kivutio. Lakini angalau kuwe na kivutio kitakachowafanya wananchi hata kuwapa kivutio cha kuwafanya wao wajione kwamba ni wazalendo wawe na imani ya nchi yao, na hicho pia ni kivutio ambacho kinaweza kikasaidia wawepo hapa.

Changamoto ya nne, ni maendeleo na mabadiliko ya tabia ambayo imebadili sura ya magonjwa ambapo magonjwa mengi ya kuambukiza na sio ya kuambukiza pamoja na yale yanayotokana na ajali mbali mbali za barabarani, kuna ajali za aina nyingi yanajitokeza sana katika nchi yetu.

Halafu changamoto ya tano ni uwepo wa magonjwa hatarishi sana katika dunia yetu hii ambapo hayajafika hapa, lakini ni hatari madamu yapo kwenye dunia, na dunia inajulikana kama kijiji ni hatari.

Magonjwa yenyewe ni mafua ya ndege, ambayo yanaanza kujitokeza, *ebola* yanaanza kujitokeza, kuna bonde la ufa limetokea halafu kuna hiyo ya siku hizi ya *zika*, ambayo kwa kweli ni tishio kubwa sana hasa Marekani na baadhi ya nchi za Asia.

Sasa kutokana na hayo basi nipendekeze *facility* ambayo nishawahi kutoa hapa lakini na leo napendekeza tena. Napendekeza kwanza kuwe na *specialist* wa *cardiology* na *hard surgery*, najua mengine yapo haya yameshapendekezwa lakini natilia mkazo tu. *Specialist* wa *diabetes*, na *endocrinology, ear, nose and throat* tuimarishe, *gastroenterology* na *GI Surgery, geriatrics, gynaecology,* narudia tena kwamba haya magonjwa yapo lakini na yanashughulikiwa nasema

yaimarishwe zaidi. *Nephrology, neurology* na *neuro surgery, ophthalmology orthopedic, psychiatric, palmology, rehabilitation, rheumatology, urology* na mengineyo ambayo watayaona wataalamu madaktari wetu.

Nasema kwa kweli ni mswada mzuri, narudia kuwapongeza wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine kuufanyia kazi mswada huu ukafika hapa Barazani na leo tunauchangia.

Sasa naingia kwenye mswada wenyewe na sina mchango mkubwa kwa sababu mengi yameshachangiwa mimi nakwenda moja kwa moja kwenye ukurasa wa 32 namba 19 pale pametajwa kutakuwa na Kamati ya Uongozi ambayo wakatajwa Kamati ya Uongozi itakuwa na wajumbe. Nasema Kamati ya Uongozi hii ingekuwa ni vizuri ikapata na mwakilishi kutoka Wizara yenyewe, kama Naibu Mkurugenzi au Mkurugenzi wa Mipango lakini awepo hapa na kama ni Naibu Katibu Mkuu basi awe ni Mwenyekiti wa hii kamati.

Halafu napendekeza kwamba kuwe na Kamati Tendaji, hamna Kamati Tendaji haikutajwa hapa nadhani wenyewe wataalamu wanajua kwamba labda haina umuhimu, lakini nadhani ina umuhimu. Kamati Tendaji ambayo itawashirikisha wataalamu wa fani mbali mbali wao wawepo katika kutoa maoni yao kuhusu uendeshaji wa hospitali ya Mnazi Mmoja.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, sitaki kupoteza muda kuwaruhusu na wajumbe wengine nao wachangie naona niishie hapa. Mimi naunga mkono mswada huu ufanyiwe kazi na hospitali ya Mnazi Mmoja ifanye kazi ili wanyonge nao waweze kutibiwa hapa hapa, wale wanaohitaji *refer,* hospital basi wakawa wanafanyiwa hapa ili magonjwa haya tuyapige vita kwa kasi kubwa sana. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya kuanzisha hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, wenzangu wamechangia na kuna baadhi tayari wameyagusa mimi nitaacha, mengine nitaongeza nyama, lakini vile vile na mimi nitatoa ushauri wangu.

Mhe. Spika, kwanza tunatoa pongezi kubwa sana kwa Mhe. Rais kupitia Mhe. Waziri kwa kuweza kuleta mswada huu ambapo kama tunavyojua Mhe. Rais wetu wa Awamu hii kipaumbele chake cha mwanzo ni afya, kwa hivyo kuletwa

kwa mswada huu kunadhihirisha kwamba kweli amedhamiria kuboresha huduma za afya kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nilikuwa ninaomba tu, ninamuomba sana Mhe. Waziri huu mswada ni muhimu sana, lakini huu mswada tukiupitisha kama ulivyo kwa kweli tutakuwa tumetengeneza *white elephant.* Tutakuwa tumetengeneza kitu kizuri lakini ufanisi wake bado utaendelea kusuasua, kuna msemo wa Kiswahili huko mitaani kama unataka pepo lazima ukubali kufa, kwa hivyo ufe ili upate pepo.

Sasa huu mswada Mhe. Spika, inaonesha Mhe. Waziri anataka pepo ya afya kwa Zanzibar, lakini kila nikiuangalia huu mswada Mheshimiwa naogopa kufa. Sasa mimi ninafikiri tukubaliane tufe ili tuweze kupata pepo.

Mhe. Spika, naanza moja kwa moja katika jina fupi. Jina fupi mimi naomba tufanye marekebisho lakini pia kamati tunaishukuru ilifanya marekebisho. Lakini na mimi pia nilikuwa naomba niongeze hayo marekebisho. Naomba jina fupi la sheria hii iseme Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Nadhani hapo itakuwa ime-*cover* maeneo yote, maana yake wengine walikuwa wanazungumza kwamba huu mswada wa kuanzishwa hospitali ya rufaa, hospitali ya rufaa tayari imeshatangazwa Mnazi Mmoja, lakini hapa ilikuwa inatengenezwa yale mambo yake iwe ya kirufaa rufaa. Sasa hilo mimi naamini jina litakuwa liko vizuri sana. Na kama kuna watu wanaogopa neno taifa, sisi pia tuna timu ya taifa ya Zanzibar hapa mbona haijavunjwa na wala hakuna mtu yeyote aliyehoji kwa nini Zanzibar timu yake ya taifa iitwe timu ya taifa. Kwa hivyo bado na hii naomba iendelee kuitwa hospitali ya taifa ya rufaa ya Mnazi Mmoja kama nilivyohisi mapendekezo yangu haya.

Jengine Mhe. Spika, naona humu kwenye mswada kuna baadhi ya maneno hayakupatiwa tafsiri, kwa hivyo nikifika katika maeneo hayo nitajaribu kukushauri Mhe. Waziri nayo yaingizwe kwenye tafsiri au kwenye ufafanuzi.

Mhe. Spika, nakuja kwenye kifungu cha 4 au sehemu ya pili ya mswada, kifungu cha 4 kinasema:-

"Kazi za hospitali zitakuwa kutoa huduma kama hospitali ya rufaa kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji huduma".

Mimi nadhani Mheshimiwa kuna wenzangu walisema neno kama tunakuwa kama tunafananisha fananisha, hii tayari ni hospitali ya rufaa. Kwa hivyo mimi napendekeza kazi ya hospitali iwe:

a) Kutoa huduma za kawaida na rufaa na kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya. Kwa hivyo mimi ninafikiri hiyo itakuwa imeweza ku-*cover* eneo lote.

Chengine Mhe. Spika, nilikuwa naomba kifungu hicho hicho cha 4 ukurasa 27(c) kinasema "kuwahudumia wagonjwa wa nje na ndani kwa mujibu wa maadili ya udaktari".

Sasa mimi naomba yaongezwe maneno pale kwamba; kuwahudumia wagonjwa wa nje na wa ndani kwa mujibu wa sheria na maadili ya daktari, ninafikiri itakuwa imekaa sawa.

Chengine Mhe. Spika, kwenye mswada huu nimejaribu kuja katika kifungu cha 8 kazi za Bodi. Bodi itatekeleza kazi zifuatazo; zimeelezwa (a) mpaka (p). Sasa mimi hoja yangu iko hapa kwenye (h):

"Kuhakikisha kuwa hospitali inatekeleza wajibu wake", hapa imewekwa kwa wizara, kuna mwenzangu mmoja aliuliza wizara gani, mimi nilikuwa napendekeza hili neno wizara liwekwe huko kwenye tafsiri au kwenye ufafanuzi, ili ikisomeka hii wizara ijulikane ni wizara gani. Kwa hivyo ikiwepo kwenye tafsiri wizara maana yake ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa hivyo ina maana hii sentensi itakuwa imekaa vizuri.

Vile vile (i) Mhe. Spika, inasema, kazi za bodi:

Kupendekeza masharti ya utoaji huduma na maslahi ya ajira kwa wafanyakazi wa hospitali kwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, kifungu hiki ndicho ambacho kitakachoweza kuipunguzia nguvu na uwezo na hayo malengo yaliyokusudiwa katika sheria hii. Mimi napendekeza kwamba kifungu hiki kisomeke kwamba kupendekeza kwa waziri maslahi ya utoaji wa huduma na maslahi ya ajira kwa wafanyakazi wa hospitali ya Mnazi Mmoja. Na kwa nini nikasema hivyo.

Mhe. Spika, unaposema kwamba kwa kufuata sheria ya utumishi wa umma katika suala zima la maslahi Mhe. Spika, kwa kweli sasa hivi maeneo mengi

yamekuwa na manung'uniko hasa wanapopeleka mapendekezo yao ya maslahi kwenye Tume ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, wewe mwenyewe ni shahidi lakini kwa bahati mbaya ndio ulikuwa hupo, hata sisi ndani ya Baraza la Wawakilishi tuna tatizo kubwa sana tunapopeleka mapendekezo ya stahiki za watumishi wetu. Wakati mwengine mpaka yaani vile vitengo Tume ya Utumishi inavikataa. Nitatoa mfano kwa sababu nataka nitoe mfano ili waziri anifahamu. Leo Tume ya Utumishi wanaposema ah! Kitengo cha *Hansard* kifutwe, ina maana patakuwa hapana Baraza hapa, itakuwa tuko katika maskani. Maana maskani ukishasema maneno, ukishaondoka yule mwengine akija ukisema jana nilisema kitu fulani ukikataa hakuna kumbukumbu. Sasa hii inatokana na nini? Ni kwamba wenzetu hawa wanashindwa kufahamu umuhimu wa kazi na zile taasisi.

Mhe. Spika, suala hili kama tutakibakisha kifungu kama kilivyo utakuja kurudi kama utaratibu wetu wa sasa hivi, watu wasubiri Rais afanye ziara ili katika risala wamwambie maslahi yetu madogo; hatuwezi tukenda huko. Mimi nadhani kwa kuwa hapa kutakuwa kuna bodi na hii Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali ambayo ni tegemeo kubwa, kwa kweli katika hospitali nyingi za binafsi ambapo wananchi wetu wa Zanzibar sasa hivi wamekuwa ndio wanakokimbilia, ukiangalia *qualification* za madaktari wao basi wa Mnazi Mmoja wao wako vizuri zaidi, kuliko hata huko wanakokimbilia. Pia wakati mwengine hawa wa Mnazi Mmoja ndio wanakwenda katika hizo hospitali nyengine.

Sasa ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu ya maslahi na haya maslahi tukiiachia bodi kwa kushauriana na waziri mimi nafikiri hospitali itakuja katika kile kiwango ambacho tunakitaka.

Mhe. Spika, leo hospitali yetu ina upungufu mkubwa sana wa madaktari bingwa, hasa wa maradhi haya ambayo yasiyoambukiza na ambayo wataalamu wanatwambia sasa hivi ndio yanayoongoza kwa kuua watu, lakini ukija ukiangalia madaktari mabingwa hatuna wa kutosha. Mhe. Spika, kwa hiyo nitaomba tu, kidogo nijaribu kutoa mfano wa upungufu wa madaktari wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika maelezo yake alisema tuna madaktari bingwa wengi, lakini madaktari bingwa tunataka katika yale maeneo ambayo stahiki.

Kwa mfano, kama maabara leo daktari bingwa Zanzibar tunae mmoja, katika sehemu ya *ultrasound* tuna daktari mmoja pamoja na *CT-Scan*. Kama ile *CT-*

Scan serikali imenunua kwa gharama kubwa na mambo mengine, lakini leo matokezeo yake unaambiwa daktari bingwa ni mmoja.

Mhe. Spika, vile vile kwenye kitengo cha pua, koo na masikio daktatri bingwa ni mmoja, kwenye *pressure* na sukari angalau ndio tuna wawili, ukija kwenye saratani daktari bingwa tumempata *alhamdulillah* mmoja, lakini dawa hakuna. Leo ina maana daktari yupo ameshakwenda kusoma na amesharudi, lakini dawa hakuna na huyu naye tukifanya masihara atatukimbia.

Mhe. Spika, lakini vile vile kwenye figo hatuna daktari bingwa na figo sasa hivi ni katika maradhi ambayo yanaathiri sana maisha ya binadamu na maradhi ambayo ukiyakosea dakika moja tu basi unakwenda na maji. Pia ukienda kwenye kitengo cha *emergency* na *ICU* daktari bingwa hatuna, kwenye upasuaji *alhamdulillah* angalau tunao watatu lakini kazi kuwa-*retain* wakaendelea kubakia.

Mhe. Spika, ukienda katika maradhi ya kina mama Mhe. Nadir Abdul-latif juzi alizungumza sana hapa kwamba hapendi kuona kina baba wanakwenda kuwahudumia kina mama, hasa wakati wa kujifungua. Tulikuwa nao hapa madaktari wawili lakini tayari mmoja amekimbia na *Aga Khan* na mmoja amekwenda zake *UN* kufanya kazi huko, kutokana na nini? Ni kutokana na maslahi madogo.

Mhe. Spika, ukija kwenye kitengo cha macho daktari hatuna, tulikuwa nae sasa hivi amechukuliwa hospitali kule *CCBRT*, lakini ukija katika kitengo kile cha nusukaputi daktari bingwa tunae lakini Mhe. Waziri ameshamchukua yeye amempeleka wizarani. Kwa hiyo, ina maana inapotokezea kesi inabidi aache kule aje huku.

Vile vile maradhi ya mkojo na tenzi dume ambayo sasa hivi yanaongoza daktari bingwa tukiangalia pale nako hatuna, tulikuwa naye hapa alikuwepo amechukuliwa wizarani, Dkt. Mohamed Jidawi na sasa hivi ameshastaafu, sijui Mhe. Waziri atamchukua vipi. Lakini kwa sheria hii mimi naamini hiki kifungu nilichokuwa nakifafanua tukikirekebisha na Dkt. Jidawi tutaweza kumuajiri hata kwa *part-time*, ili aweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, sitaki nimsifu Dkt. Jidawi lakini katika ziara zetu hizi za kimichezo tunapokwenda Arusha kuna daktari mmoja tulikutana naye akatuuliza yule Dkt. Jidawi angalipo Zanzibar? Tukamwambia yupo, alinyanyua mikono juu akasema *alhamdulillah*, akasema yule mtunzeni, kweli

kweli ile ni hazina ya kweli. Katika *qualification* za madaktari mabingwa duniani na yeye anatambulika.

Mhe. Spika, sasa kama tutaweza kuipa nguvu hii sheria tukaiachia mamlaka bodi kwa kushirikiana na waziri, mimi naamini wataweza kuwa-*retain* madaktari na hawa wengine wataweza kubakia.

Mhe. Spika, nakuona…

Mhe. Spika: Mheshimiwa bado dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa dakika zangu mbili najitahidi nimalizie, lakini hii nilikuwa naeleza kuonyesha uhaba wa madaktari na wakati mwengine wananchi wanakwenda hospitali wanafika pale daktari hawamkuti. Mheshimiwa ni kwamba binadamu anachoka, leo daktari bingwa mfano kama haya maradhi tuliyosema yasioambukiza. Kuna orodha ya wagonjwa karibu 1,000 wote wanapokelewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ya Rufaa wanatoka Zanzibar.

Sasa hebu tuangalie wagonjwa wale wote wangekuwa wanakuja pale Mnazi Mmoja daktari huyo anakuwa vipi, lazima atafika pahala atachoka. Sasa mimi nilikuwa naomba sana kile kifungu ambacho nimekisema kwamba bodi kwa kuangalia maslahi ya wafanyakazi, bodi ishauriane na waziri, naamini kwa sababu waziri ndio mshauri mmoja mkubwa wa bodi wanaweza wakazingatiwa maslahi yao na wao wakaendelea kubakia.

Mhe. Spika, nilikuwa katika kifungu cha 19, nilikuwa naomba hili neno 'mlezi' nalo pia tungeliweka kwenye tafsiri. Maana yake hapa imewekwa mlezi wa hospitali katika ile Kamati ya Uongozi. Hapa naona kidogo neno 'mlezi' liko juu juu haijuilikani mlezi wa nini. Mlezi wa watoto, mlezi wa nani? Mlezi wa hospitali lazima aweze kuonekana.

Mhe. Spika, lakini kifungu cha 23 sehemu ya tano, Masharti ya Fedha. Mimi hoja hii naungana na hoja ya wenzangu kwamba kifungu hiki kinachosema hospitali inaweza kubakiza fedha kilichopatikana kutokana na malipo ya huduma ilizozitoa kwa kiwango kitakachokubaliwa na waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha.

Mhe. Spika, mimi naomba katika eneo hili hospitali kwa kuwa itakuwa ina bodi yake na bodi hii Mhe. Waziri ndiye anaesimamia, mimi nafikiri hakuna haja ya

kuweza kwenda Wizara ya Fedha, fedha zibakie katika hospitali, ili ziweze kuboresha vitendea kazi na maslahi mbali mbali.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo, lakini vile vile kwa kuwa sasa hivi serikali ilitaka kuleta Sera ya Bima ya Afya kwa nini tuogope kuchangia wananchi? Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba, tutapokuja kwenye vifungu nitajaribu kupiga buti ili kuweza kutoa ufafanuzi zaidi na kumsaidia waziri, ili kuweza kuuboresha huu mswada. Lakini pamoja na yote naunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada ulio mbele yetu wa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kwanza mimi napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji kwa niaba ya Mhe. Rais wamefanya kazi kubwa sana ya kuleta mswada huu mbele yetu katika kuongeza na kuboresha huduma ya afya katika hospitali yetu ile kubwa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, mimi naomba niende Sura ya Tatu, Uongozi wa Hospitali. Kuanzishwa kwa bodi inayojuilikana kama Bodi ya Ushauri ya Hospitali, mimi naomba nishauri hapa, naomba kisomeke badala hivi kilivyo, “Bodi ya Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja”. Kwa sababu tukisema Bodi ya Ushauri itakuwa hii kazi yake ni kushauri tu, vitu vyengine vyote hivi tulivyoviainisha katika kazi zake inakuwa sio wajibu wake. Sasa naomba kitafsiri na umuhimu wa bodi hii isomeke tu moja kwa moja Bodi ya Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, niondoke katika eneo hilo nishuke katika kifungu Nam. 4, Mwanasheria kutoka wizara inayohusika na masuala ya afya atakuwa ni miongoni mwa Katibu wa Bodi. Mimi kidogo hapa niendelee kumshauri Mhe. Waziri, ili kuondoa urasimu wa utumishi na utekelezaji wa majukumu, kuendelea kuwaunganisha viongozi wa wizara kwenye taasisi hii, kwa umuhimu wake na ubora wake wa utekelezaji ni bora tutapopitisha mswada huu basi kuwe na Mwanasheria tutakayemuajiri katika kusimamia kazi za bodi, lakini na majukumu yatakayotokezea katika Hospitali hii ya Taifa ya Mnazi Mmoja na yeye ndio aainishwe kuwa Mjumbe wa Bodi badala ya Mwanasheria kutoka katika wizara.

Mhe. Spika, mimi naomba niende kwenye eneo la kuanzishwa Idara ya Hospitali, sina tatizo na idara hizi lakini nina tatizo katika kuwapata wale viongozi wanaosimamia idara kwa majina tu, ili kusomeka wakurugenzi wa

idara hii mimi siko pamoja na eneo hili. Ni bora kwa kuondosha lile neno 'ukurugenzi' bora hawa wakasomeka wakuu wa idara ambao watapatikana kama mfumo huu ulivyoainishwa katika sheria hii.

Tukiongeza majina ya wakurugenzi inaweza ikaja ikafika pahala wakaja wakadai *facilities* nyingi na tuna dhana nzuri, lakini ule uhalisia ukaondoka. Sasa ni bora huyu Mkurugenzi Mtendaji atakayeteuliwa na Rais mimi sina tatizo naye, lakini hawa wakurugenzi wa hizi idara naomba tufanye mabadiliko wasomeke “wakuu wa idara”, hizi idara ambazo tumeziainisha hapa chini.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye eneo la madhumuni na sababu, kuna neno la uwakala. Mhe. Mohammed Said Mohammed alilizungumza kwa upana wake na mimi lilikuwa linanipa mashaka sana, nikataka baadae tupate tafsiri hasa ya uwakala ili tusije tukafika pahala tukarudi kule kule. Leo tuna nia njema ya kupitisha mswada huu lakini uwakala huu ukaja ukatuharibia yale malengo tunayoyataka, wizara ikawa inaingilia majukumu ya taasisi hii ikawa wakati fulani tuna wataalamu wazuri hivi, tunakwenda kuwahamisha siku moja hawakumpokea waziri vizuri, hata bodi haihusiki.

Sasa uwakala huu ukawa unanipa mashaka, naomba tafsiri halisi ya uwakala huu ili kutengeneza majukumu na kuyabakisha katika mfumo mzuri wa mswada huu unakoelekea, basi naomba waziri aje anipe tasfiri kamili ili twende vizuri katika eneo hili.

Mhe. Spika, lakini hapo hapo chini katika kifungu ambacho kinaendelea kuna maelezo na nayasoma pale ambapo mimi nataka kujenga hoja yangu. Hospitali inayoanzishwa itatoa huduma kama rufaa, hiyo kama rufaa maelezo wenzangu wameshatoa, kuweka mfumo mzuri wa utoaji wa huduma ya afya ya Zanzibar na itakuwa na jukumu la kusimamia uendeshaji wa hospitali nyengine yoyote itakayokuwa chini ya usimamizi wa hospitali hii, kwa mujibu wa sheria nyengine yoyote.

Mhe. Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hapa tulipo kabla ya kupitisha mswada huu kumbukumbu zangu inawezekana akaja kuniambia zina usahihi au sio sahihi. Uongozi uliopo sasa unaziongoza Hospitali ya Mwembeladu na Hospitali ya *Mental*. Sasa tunapokwenda mimi zaidi naizungumzia hii *Mental Hospital*, kwamba tunapopitisha mswada huu hii tunaiweka wapi?

Maana hospitali hii haihitaji rufaa ukiingia mle ndio umeingia tu lazima kuwe kuna *new set-up*, labda Mhe. Waziri aje aniambie. Sasa sijui kama tulipopitisha mswada huu ile tunaiacha tunaitengenezea uongozi wake mwengine au

tunaingiza hapa, mana nasema hakuna wodi ya rufaa katika ile, ukiingia kule ndio umeingia. Kwa hiyo, aje anipe maelezo ya kina ili tuweze kujua maana tusije tukaunganisha vitu baadae vikatukwaza.

Mhe. Spika, mwisho kwa sababu mengi yameshachangiwa na wenzangu katika moja ya majukumu ya serikali na wizara hii, wametupa *plan* nzuri tu ya ujenzi wa hospitali ya Tunguu ambayo itakuwa ni hospitali ya rufaa. Sasa katika mfumo huu wa kuleta bili hapa mbele yetu na huko mbele tuna *target* ya kusogeza huduma katika hospitali ya rufaa ya Tunguu na ndio azma ya serikali. Hii tutakuja kuiunganisha hapa au tutakuja kuleta bili nyengine ya kuirejesha hospitali hii kuja katika *primary*, kuna kutumika kwa wilaya ili tuelekee Tunguu. Sasa hebu hapa katika azma ya serikali ijayo akija waziri anielezee tu ili nipate ufafanuzi mzuri zaidi.

Mhe. Spika, mimi naomba niishie hapa na sina buti, nachangia mswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kuweza kunipatia fursa hii ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi naomba nitoe shukurani zangu za dhati na pongezi kwa Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuwa na dhamira njema na ya dhati kabisa katika kuhakikisha huduma ya afya inakua na inakuwa endelevu katika Taifa letu la Zanzibar. Lakini pia nipongeze sana jitihada za Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri sambamba na watendaji wote wa wizara hii pamoja na changamoto kubwa ambazo zinawakabili, lakini bado wamekuwa wakipigana kwa hali na mali kuhakikisha huduma na sekta nzima ya afya changamoto nyingi zinaweza kutatuliwa kwa dhamira ya kuwasaidia wananchi wote kwa ujumla.

Pia naomba niungane na wajumbe wenzangu waliopita ambapo kwa urefu kabisa wameweza kutoa michango mingi kwa dhamira kwamba mswada huu uwe wenye tija na wenye mafanikio, hasa katika kuboresha huduma hii ya afya. Sasa nianze kwenda moja kwa moja katika mswada huu.

Mhe. Spika, na mimi niseme tu kama ambavyo wajumbe wenzangu waliopita walipokuwa wana hofu katika hii Ibara ya 3(i), hasa katika yale maneno mawili ya mwisho “wakala wa serikali”. Nami binafsi nimepata hofu, lakini baada ya kutizama na kurudi nyuma kuangalia sera ya afya hasa katika maeneo yote tangu kuanzia mwaka 1964 nikaona kwamba ni sahihi, lakini ni vyema

tukamshauri Mhe. Waziri kwamba angalau uwakala huu na wenyewe ufanyiwe *interpretation* katika *Section Number Two,* kwa dhamira ya kwamba hata atakayekuja kusimamia hili angalau maana halisi ya huu uwakala wa serikali iwe imetolewa ufafanuzi kwa kina.

Mhe. Spika, pili niende moja kwa moja katika Ibara ya 4(d) inasema: “kushajihiisha”. Ni vyema tukafanya marekebisho hapa iwe ni “kushajihisha”, maana hapo hizo (ii) zimekuwa nyingi kitu ambacho si sahihi katika lugha yetu ya Kiswahili.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika Ibara hii ya 4(k) naomba kunukuu.

Ibara ya 4(k) inasema kwamba:

“Kutekeleza, ama peke yake au kwa kushirikiana na mtu mwengine yeyote au mashirika ndani au nje ya Zanzibar, kukuza au kuzalisha vifaa vya maabara ya hospitali, vifaa tiba na zana”.

Mhe. Spika, mimi nashauri ama napendekeza iwe vifaa na dawa au kuzalisha dawa na kutoa elimu ya afya na kinga, nashauri maeneo hayo tuyaongezee.

Pia nitakuwa *very brief* kwa sababu michango mingi wajumbe wenzangu wameshaiwasilisha, niende moja kwa moja katika Sehemu ya Tatu, Ibara ya 5(2)(e) ambayo imesema, "wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi".

Naongezea hapo, nashauri hawa wawakilishi wawili katika sekta binafsi lakini lazima wawe na mahusiano na sekta ya afya, isiwe tu wawakilishi wawili kutoka katika sekta binafsi. Ni vyema tukapata *contribution* nzuri kutoka kwa wadau ambao watatoka katika ile sekta ya afya.

Mhe. Spikia, lakini hapo hapo katika *section* 5, kama ambavyo wajumbe wenzangu walifanya marekebisho kwamba kuna *section* 5(1), *section* 5(2), lakini hizi 5(2) zipo mbili. Bahati nzuri mjumbe aliyepita alishawahi kusema kwamba iwe 3 lakini katika hiyo 3 naomba ninukuu, inasema kwamba:

"Isipokuwa wajumbe wanaoteuliwa kwa nafasi zao, Wajumbe wengine wa Bodi watateuliwa na waziri baada ya kushauriana na taasisi husika", naomba tuongeze kwa kuzingatia jinsia. Maana tusipofanya hivi tutakuwa tunawaweka baadhi ya watu pembeni, kitendo ambacho hakitokuwa sahihi na *gender equality* tunayokwenda nayo katika taifa letu.

Mhe. Spika, lakini jengine niende moja kwa moja katika *section* 8(i) ambayo inasema, ... bora niache hii lakini niende kwenye *section* 12 ambayo naomba na yenyewe ninukuuu inasema: "Wajumbe wa Bodi watapaswa kulipwa posho kwa kadiri itakavyoamuliwa na waziri". Nashauri iwe hivi:

"Wajumbe wa Bodi wataweza kulipwa posho kwa kadiri itakavyoamuliwa na waziri kwa mashauriano ama kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Bodi".

Mhe. Spika, wakati tunayafanya haya tutambue kwamba Mhe. Waziri atakuwa ni mtu mkubwa sana, sasa kila kitu tukimwachia yeye wakati tayari tuna bodi husika tukitoa *power* yote kwa Mhe. Waziri na kukiuka Bodi hatutakuwa tumefanya kitu sahihi. Kwa hiyo, nashauri hapa angalau katika hili na Mwenyekiti wa Bodi na yeye ashirikishwe.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika Sehemu ya Nne ambayo ninataka kurekebisha *marginal note* ya pembeni kwenye mkono wa kulia katika *section* 14 ambayo imesema sifa za Mkurugenzi Mtendaji. Nashauri kama ilivyoshauriwa na Mwenyekiti wa Kamati kwamba iwepo uteuzi wa mkurugenzi. Halafu katika hii *section* ya 15 kwenye *marginal note* hiyo hiyo ambayo imesema uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji, hapa wakati katika *section* hii chini yake tunaona sifa; kwa hiyo nashauri katika *marginal note* hiyo iwe sifa za mkurugenzi, ili tutakapotizama katika *right side* tizama na chini utaona hizi sifa zake kama ambavyo zimekuwa zinahitajika.

Mhe. Spika, pia niende moja kwa moja katika *section* ya 17(i) ambayo inayosema kunaanzishwa idara za hospitali ambazo zitakuwa kama zifuatazo kama ambavyo imerekebishwa. Lakini pia katika *roman one* inasema Idara ya Huduma za Usafi, nami nashauri kwamba iwe Idara ya Huduma na Utabibu kwa dhamira ya kuwa tujuwe moja kwa moja kwamba kila tunachokifanya pale lazima kihusiane na sekta nzima ya afya. Lakini katika *section* hiyo hiyo, 17(f) ambayo imesema Idara ya Huduma ya Uchunguzi wa Afya nami nashauri isiwe afya peke yake lakini iwe Idara ya Huduma, Uchunguzi wa Afya na Maradhi. Kwa sababu tukitizama afya peke yake bila ya kuliacha neno maradhi pembeni naona haitakuwa sahihi.

Mhe. Spika, pia niende moja kwa moja katika *section* ya 19 ambayo napendekeza kuongezwa kwa kipengele kipya, maana kimeishia (e). Mimi ninapendekeza (f) kiwe kuna Muuguzi Mkuu wa Hospitali. Maana katika ibara hii inasema kutakuwa na kamati itakayojulikana kama Kamati ya Uongozi wa Hospitali.

Sasa kama tutakuwa tuna Muuguzi Mkuu wa Hospitali na yeye hayupo katika Kamati ya Uongozi itapelekea mawazo yake kuwasilishwa na mtu mwengine kitu ambacho kwangu mimi naona hakitakuwa sahihi, ni vyema tukatoa ushirikishwaji wa *direct* kwa Muuguzi Mkuu huyu na yeye kuingia katika Kamati ya Uongozi. Maana kwa kufanya hivyo angalau tutaweza kuja kusaidia kazi ambayo kwa pamoja inaweza ikafanywa.

Mhe. Spika, mimi kwa uchache nimekusudia kusema haya lakini zaidi napongeza sana jitihada za Mhe. Rais na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa dhamira ya kuboresha huduma yetu ya afya. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mihayo Juma N'hunga. Sasa naomba nimwite Mhe. Nassor Salim Aljazira, atafuatiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia mswada huu wa kuanzishwa Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja. Kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dokta Ali Muhammed Shein kwa busara zake za kuamua kuja na sheria hii, kwani mswada huu ndio hatua ya kupeleka mbele sekta ya afya.

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze kwa kuwachagua viongozi ambao wanaongoza sekta hii au Wizara hii ya Afya, akiwemo Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu ambao hawatokani kabisa na sekta ya afya, lakini wamekuwa wakifanya kazi zao vizuri kwa kuleta maendeleo na kuinua Wizara hii ya Afya. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuwaamini watendaji hao.

Mhe. Spika, lakini vile vile kwa kuzingatia kwamba hawa watendaji tukirudia nyuma katika sheria Mzee wetu Thabit Kombo Jecha pamoja na Mhe. Mzee Ali Mwinyigogo ndio waliokuwa viongozi ambao hawakutokana na sekta ya afya, walifanya kazi nzuri lakini leo Mhe. Waziri amekuja kurithi mikoba ile ya Mzee wake Mzee Thabit bin Kombo. Kwa hivyo nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuwateuwa viongozi hao.

Mhe. Spika, pamoja na kuwateuwa mawaziri hawa akiwemo Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Waziri wa Afya, nimuombe sana Mhe. Rais, kwa sababu ya matatizo ambayo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja asichelewe kushirikiana na Mhe. Waziri kutumbua majipu yaliyopo baadhi katika wizara hii au katika

Hospitali hii ya Mnazi Mmoja. Lakini na mimi pia niungane na Kamanda wangu Mhe.Hamza Hassan Juma kwa kumuomba Mhe. Rais na serikali kwa ujumla kuilinda na kuienzi hazina tuliyonayo ya ndugu yetu Dokta Mohamed Jidawi, kwa kweli ni hazina na inahitajika kuenziwa ili kwa faida yetu na kwa faida ya vizazi na wizara hii nzima ya afya.

Mhe. Spika, baada ya hayo nije katika mchango wangu katika mswada huu. Katika mswada huu mchango wangu mdogo ambao nilikuwa nataka kuutoa katika kifungu cha 17 katika Sehemu ya Nne ambayo inazungumzia Mkurugenzi na Mtendaji wa Wafanyakazi. Katika neno kidogo ambalo nilikuwa nataka msaada wa Mhe. Waziri, kutokana na tafsiri ya maandishi ambayo yamo katika mswada huu. Ukiangalia kifungu cha 17(a) Idara ya Huduma ya Usafi. Mhe. Spika, ukiangalia katika mswada huu kwa kiingereza unasema kwamba *"department of cleaning service*" sasa nilikuwa tu nataka aje anieleze kwamba Idara ya Kuhudumia Wagonjwa au tafsiri hii inaeleza hapa kwamba Idara ya Huduma ya Usafi, sasa tafsiri yake sijui ikoje hapa, naona kama kuna kidogo mchanganyiko, Mhe. Waziri akija atueke sawa hiyo.

Mhe. Spika, lakini jengine vile vile sehemu hiyo hiyo ya 17(e) Idara ya Usalama wa Afya ya Binaadamu. Ukija katika tafsiri ya kiingereza inasema kwamba *"department of medical engineering"* sasa ni Idara ya Uhandisi wa Vifaa au hii ni ambayo imo katika tafsiri ya kiswahili, ni vyema akina atuweke sawa ili kuweza kuandaa vyema mswada huu.

Mhe. Spika, nije katika sehemu ya 5, masharti ya fedha. Katika kifungu cha 22 kinasema hapa kutakuwa na fedha za hospitali ambazo zitajumuisha (a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku, lakini (b) michango, ada, malipo na mikopo ambayo hospitali inaweza kupokea mara kwa mara kutoka kwa mtu au taasisi yoyote. Sasa mimi mchango wangu ni kwamba pale baada ya kusema mchango, ada na malipo kuwepo na neno misaada na mikopo ambayo tunaweza kuyapata katika hospitali hii. Kwa sababu misaada tunaweza kuipata kwa njia ya wafadhili wa ndani na wafadhili wa nje ni vyema ikawa lipo neno hilo misaada.

Mhe. Spika, lakini jengine ambalo nilikuwa nataka kuchangia kuhusiana na sehemu ya sita. Katika sehemu hii ya sita katika kifungu cha 27(2) bila ya kuathiri aah! mabano (1) hospitali itaendelea kutoa huduma za afya kwa wagonjwa bila ya malipo na kufuata sera na miongozo ya wizara. Hapa nilikuwa natakakuchangia kwamba mimi niiombe wizara au serikali kwa ujumla kwamba tuendane na sera zile za waasisi wa nchi yetu Mzee wetu Abeid Amani Karume pamoja na wenzake kuweka matibabu bure kwa

wananchi. Kwa sababu ukizingatia wananchi wetu ni masikini na sera hii ya Afro Shirazi ilikuwa na malengo mazuri na ni vyema tu kwamba kuendeleza sera hii kuhakikisha kwamba wazee wetu, watoto wetu, ndugu zetu, jamaa zetu wanapata matibabu ya bure katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa sababu sera hii ilikuwa na lengo zuri. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla ili kuendana na sera hii kuhakikisha kwamba tunaendeleza yale ambayo waasisi wetu waliyaanzisha kwa ajili ya wananchi wao.

Mhe. Spika, baada ya hayo na kwa sababu ulinipa dakika tano. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni na niwaombe waheshimiwa wenzangu tuiunge mkono hoja hii ili kupata sheria ambayo itatusaidia sana kusukuma maendeleo na sekta hii ya afya kwa faida ya wananchi wetu na Zanzibar kwa ujumla. Nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Nassor Ali Jazira. Sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajiandae.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe.Spika, awali ya yote na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako hili tukufu. Lakini pia na mimi niungane na wenzangu nichukuwe fursa hii kwa kumpongeza sana Mhe. Rais Dokta Ali Muhammed Shein ambaye kwa nia yake thabiti ameonyesha kuwasaidia wananchi wake wa Zanzibar kwa ajili ya kupata tiba iliyo sahihi.

Mhe. Spika, pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote. Lakini pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha ambaye ameonyesha matumaini mazuri na usimamizi mzuri wa fedha, hii anatupa moyo na tunasema hata huko Wizaraya Afya tunakopiga kelele tunaweza tukafanikiwa vya kutosha.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa mdogo sana lakini nilisema itakuwa si vyema wala si busara kama sikuinuka nikaunga mkono mswada huu wa Wizara ya Afya,kwanza tukielewa sisi kina mama ni wadau wakubwa kabisa katika wizara kwamba sisi tuna mahitaji mengi zaidi, sisi ndio mama, sisi ndio wenye watoto ambao tunawahudumia kila mara kwenda katika hospitali, kwa hiyo nimeona niinuke na niunge mkono mswada huu kwa sababu una lengo zuri na kuweza kutupatia afya sisi kina mama hasa tukiona

tunasumbuka sana katika au tunalalamika sana tupatiwe huduma iliyo bora ya uzazi salama.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu nilitaka nitoe ushauri kidogo katika hichi kifungu nambari 7 ambacho kinaeleza Mjumbe wa Bodi atasita kuwa mjumbe iwapo.. yapo majukumu hapa sasa yanaelezwa (a), (b) lakini mimi nasema paongezwe kitu kwa sababu pia mjumbe anaweza kusita kuwa mjumbe wa Bodi iwapo atafariki, hili neno lingewekwa kwa sababu mjumbe anaweza akachaguliwa leo na kesho mungu akamuhitaji ikawa hatunaye lazima nacho hichi ni kitu muhimu kiweko.

Mhe. Spika, lakini pia mchango niende katika kifungu nambari 22 ambacho hichi ndicho kinatuhakikishia sasa haya yote ambayo yamepangwa katika mswada huu yataweza kutekelezeka nacho ni fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku na kifungu (b) wamesema mikopo, ada, malipo. Lakini Mhe. Spika, hapa ndipo penye utekelezaji wa mambo yote kwa sababu utekelezaji unakuja kwa upatikanaji wa fedha nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha, pale afya huwa wana vipesa vidogo vidogo na wao wenyewe wanavyovikusanya, naomba sana tuone kwamba waziri anarejeshewa mwenyewe hizi fedha kwa mpango maalumu ambao utakwenda kuonekana matumizi yake zinavyotumika ili aweze kutekeleza kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, kwa sababu kama vunavyojua kilio lazima uanze wewe mwenyewe mfiwa ndipo na wa mbali aingie. Sasa lazima wao wawe na kitu kidogo mkononi ili na wale wahisani wanaokuja kuleta basi na yeye mwenyewe awe anacho cha kujianzia. Kwa hiyo naomba sana kwa sababu huwa yanajitokeza mahitaji madogo madogo, uharibikaji wa feni, vyoo, nini, ili basi kujihudumia katika fedha hizi na baadaye utaratibu wa fedha utumike kwa kukaguliwa kama kawaida ili waweze na wao kupata matumizi.

Mhe. Spika, pia niende katika kifungu nambari 28(1). Kifungu hichi kinamtaka waziri aweze kutunga kanuni kwa utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii. Na hapa ndipo ninapotaka kupasisitiza kwa sababu kifungu hichi mara nyingi huwa tulikuwa tunapendekeza, hii kusema anaweza inaleta kama inavunja nguvu kidogo maana yake anaweza akatunga au la! Sasa mara nyingi tulikuwa tukisema tunashauri kwamba tuseme waziri atatunga kanuni kwa utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii, lakini bado naona sijui kunakuwa na tatizo gani la lugha za kisheria hizi.

Mhe. Spika, lakini waziri huwa anachelewa sana katika utungaji wa kanuni na hapo huwa anasababisha kuzifanya sheria zije na utekelezaji mzuri. Sasa mimi

tu kwamba mswada huu umekuja wa dharura na umekuja kwa kutaka kutujenga afya zetu wananchi; nimuombe sana Mhe. Waziri awe makini na haraka zaidi kwa kujijenga hizi kanuni ili basi sheria hizi ziweze kuwa katika utekelezaji mzuri.

Mhe. Spika, mimi ilikuwa mchango wangu ni mdogo sana, lakini kutokana na umuhimu wa mswada huu nimeona ni lazima ninyanyuke niunge mkono hoja hii kwa sababu ina maslahi kwa wananchi wa Zanzibar na nawaomba sana waheshimiwa wenzangu ili basi waweze kuchangia mswada na kuuboresha ili wananchi wa Zanzibar ziendelee afya zetu kuimarika.

Mhe. Spika, pia mimi wakati wa mchango wangu katika wizara hii niliomba Baraza kwamba kwa umuhimu wa afya ulivyo na tunahisi mahitaji na fedha walizonazo kidogo niliwahi kusema kama tukate posho yetu ya siku moja ili tuweze kusukuma fedha hizi katika wizara hii ambayo inajenga matumaini yetu ya kuwa na afya. Sasa niombe tu Mhe. Spika wewe ndiye ambaye unapenda kutuhoji Wajumbe kama suala hili tutakuwa tumeliridhia basi tuweze kupata ridhaa hiyo na Mhe. Waziri ajue atapata fedha hizo kwa kupitia njia ipi ili tuweze kuisaidia wizara yetu tukijua tunataswadaki, hasa katika Mwezi huu wa Ramadhani, lakini pia tunajenga afya za wananchi wetu ambao tunawaongoza.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja Mswada huu wa Sheria na *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu atujaalie yale mafanikio mema tuweze kufanikiwa ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nachukua fursa hii adhimu ulionipa kukushukuru na wewe kunijaalia na mimi ukaniona kidogo kuweza kuchangia Mswada huu muhimu kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa taifa letu.

Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii pia kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuusaini mswada huu uingie Barazani kama Mswada wa dharura kutokana na uzito wa suala lenyewe. Kwa sababu imekuwa ni kilio kikubwa ambacho sisi Wawakilishi kila wakati tunalia juu ya kilio cha afya za wananchi wetu.

Mhe. Spika, kabla ya kuendelea mimi nitamke wazi kuwa naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, nikiwa nina imani kwamba na wenzangu wote wataunga mkono Mswada huu kwa ajili ya maendeleo ya afya za wananchi wetu. Sasa mimi niingie kidogo kuchangia katika sehemu ya pili ya

kuanzishwa na kazi za hospitali. Kuanzishwa hospitali itakayojulikana kama Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, mimi naona ni vyema hili neno 'kama' kama walivyozungumza wenzangu likarekebishwa likasomeka 'kuanzishwa kwa hospitali itakayojulikana kwa jina la Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja', ingekuwa ina mantiki nzuri kuliko kusema 'kama'. Kwa sababu neno 'kama' kwetu sisi wazee wetu wa zamani walisema ukisema kama basi ni jambo ulilokuwa huna uhakika nalo, lakini tukisema tunalitaja kwa jina tuna uhakika nalo.

Mhe. Spika, niende katika Sehemu ya Tatu. Sehemu hii mimi nilipendekeza na naomba kwamba inaposomeka kifungu 5(1) "Kuanzishwa kwa Bodi. Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:". Mimi naomba watajwe kwa namba ikisha ndio ije ile orodha pale chini yake; Ingawa wapo wanaonekana lakini ni vizuri ikawa hivyo.

Pia tukija kwenye kifungu cha (c) "Mkurugenzi Mkuu wa wizara". Tukija katika namba 3 wamepewa wajumbe wa bodi uwezo wa kuteuwa mjumbe mmoja kuwa miongoni mwao kuwa ni makamo mwenyekiti, lakini hapa kutokana na uzito wa jambo hili mwenyekiti anateuliwa na Rais, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ana mamlaka yake yaliyotajwa, lakini kwa nini Mkurugenzi Mkuu wa wizara humu isisomeke kwamba awe ndiye Mwenyekiti wa Bodi. Pamoja na kuwa bodi nyingi tumezowea kwamba wajumbe ndio wanateuwa miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti, lakini hili ni jambo zito.

Mimi ninapendekeza kwamba hawa watu wenye mamlaka kubwa ambapo huyu akiondoka mwenyekiti anashika mamlaka. Kwa hiyo, na yeye awe miongoni mwa watumishi wakuu wa wizara ambapo anajua kama ikitokea uharibifu anaweza hata akapoteza nafasi yake ya kazi kwenye wizara. Kwa hiyo, mimi napendekeza jambo hili liangaliwe tusiende kwenye mazowea kwamba tumezowea bodi inafanya hivi na hivi tutizame na uzito wa suala hili.

Mhe. Spika, mimi leo sitaki kuchangia sana kwa sababu Mswada huu wote ni mzuri, lakini pia nataka niende kidogo juu ya kifungu cha 8(a). Hapa namuomba Mhe. Waziri awe yeye mwenyewe ndiye mwenye mamlaka ya kuteuwa na kazi ya bodi iwe ni kuthibitisha tu, wapange vizuri hiki kifungu lakini iwe mamlaka ya kuteuwa ni ya waziri mwenyewe na bodi iwe na kazi ya kuthibitisha.

Tukienda kifungu cha (e) kinasomeka kwamba: "Kuhakikisha mazingira mazuri ya fedha za hospitali". Mimi napendekeza kifungu hiki kisomeke "kuweka mazingira mazuri ya kazi na kudhibiti fedha za umma". Kwa sababu, hospitali hii ni mali ya serikali, ni mali ya Wazanzibari. Kwa hivyo, ni vyema ikasomeka hivyo nilivyosema.

Kifungu cha (f) kinasema: "Kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa na hospitali". Mimi kifungu hiki nilikuwa pia nakipendekeza kidogo kiongezwe maneno au kiwekwe sawa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba kwa ajili ya huduma za afya zinazotolewa na hospitali na mwisho wa hiyo *paragraph* inavyosema "kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika", lakini pia liongezwe neno "kwa wakati unaostahiki". Kwa sababu tunaweza tukapata huduma za afya lakini kwa wakati gani, iwe inajifunga kwamba wakati unaostahiki ili watu waweze kuwajibika, wanajua kama mimi sikuwajibika kifungu hiki kinanikamata. Kwa hivyo, napendekeza hicho nacho kiongezwe hayo maneno kule mbele.

Pia kuhakikisha kuwa hospitali inatekeleza mahitaji. Mimi napendekeza isomeke, "kuhakikisha kuwa hospitali inatekeleza jukumu lake la mahitaji ya ufundishaji na utafiti na huduma za afya na masomo mengine". Kwa sababu hii yenyewe itakuwa na jukumu la kupata hawa wataalamu na kufanya utafiti, hili neno jukumu lazima liwepo kwa sabahu wao wajue kwamba hospitali ina jukumu hilo.

Mhe. Spika, nikienda kwenye kifungu cha 16(a) kinachosema kuongoza mambo ya hospitali na kutoa huduma bora zinazojitosheleza. Mimi napendekeza napo pia liongezwe neno hapo kati kati, baina ya 'na' na 'kutoa' liwepo neno 'kuongoza mambo ya hospitali na kusimamia na kutoa huduma bora na zinazojitosheleza'. Kwa hiyo, baina ya neno 'hospitali' na 'kutoa' hapo liwepo neno 'kusimamia na kutoa huduma bora zinazojitosheleza'.

Mhe. Spika, pia tukienda kwenye kifungu cha 16(2) Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukasimu majukumu yake kwa Mkurugenzi au Afisa Mwandamizi wa hospitali kwa wakati gani? Muda maalum utakaoonesha kwamba kwa muda huo au kwa dharura hii Mkurugenzi Mtendaji ndio alipokuwa anaweza kukasimu madaraka yake, isiwe tu kwamba yeye leo kajisikia nataka kukasimu madaraka yangu anapunguza madaraka yake anasema mimi sijisikii kwa hiyo wewe fanya hili. Kuwe na muda maalum na sababu zinazoweza zikamfanya Mkurugenzi Mtendaji akakasimu madaraka yake.

Mhe. Spika, kifungu cha 21 kinasema "hospitali inaweza kwa mujibu wa masharti ya vigezo kuajiri au kuteuwa mfanyakazi au huduma". Mimi nasema kuajiri napendekeza lisomeke neno 'kuteuwa mfanyakazi au mshauri wa huduma elekezi', liwepo hilo neno mshauri wa huduma elekezi.

Mhe. Spika, mimi baada ya haya napenda kusema kwamba madhumuni na malengo ya mswada huu ni mazuri, wenye nia ya kuboresha afya za watu wetu na ni matumaini yangu kwamba sisi Wawakilishi wote tutauunga mkono Mswada huu. Kwa upande wangu narudia tena kusema kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja na nasema Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono Mswada huu. Ahsante. *(Makofi)i*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kutoa mchango wangu katika wizara hii ambayo ni nyeti sana kwenye masuala ya wizara yangu.

Kwanza pia nipende kumshukuru Mhe. Rais wetu kwa kuweza kutoa nafasi ya ruhusa ya kwamba tuweze kuipitisha mahali hapa, katika kipindi hiki muwafaka ambapo tunahitaji sana suala hili liweze kupitishwa ili Wizara ya Afya iweze kujitegemea na kuweza kufanya mambo mengi ambayo hayakuweza kupata nafasi ya kufanywa kwa muda mwingi. Pia nadhani nitakuwa sijatosheleza kushukuru kama sitamshukuru mwandalizi mkuu Katibu wa Baraza la Mapinduzi (Katibu Mkuu Kiongozi) kwa maandalizi ya kuweza kurudia waraka huu mara kwa mara katika maandalizi mpaka kukamilika na kufika mahali hapa. Vile vile Mwanasheria Mkuu wetu ambae anafanya kazi kwa bidii sana kuhakikisha kwamba haya tunayoyaleta hapa yanakuwa ni yale ambayo hayaendi kinyume na sheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba nampongeza Waziri wa Afya na ofisi yake, watendaji wake wote, nasema mswada huu umeletwa wakati mzuri kwa sababu, ili kuweka mambo mazuri na kuangalia kuongezeka kwa huduma bora za hospitali, ili iweze kuwa ya rufaa. Hii itapelekea kutumbua majipu ambayo muda mrefu yamekuwepo. Mara nyengine nisingesema ni majipu tu ya kusema kwamba labda wamefanya kwa makusudi au kwa kitu gani ni kwa sababu ya mazingira mengi yaliyokuwepo. Nadhani hayo majipu Mheshimiwa hayako kwenye maeneo mamoja tu, yako katika kila sehemu hata katika sehemu ya ndani ya familia kuna majipu ambayo yanahitaji kutumbuliwa.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wahudumu na wafanyakazi wote wa idara za afya Zanzibar ikiwa pamoja na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Katika mazingira yao magumu wameweza kufanya kazi hivyo hivyo, kwa namna hiyo waliyoweza na wamefanya mambo mengi sana ya kufanya ambapo wangesaidiwa zaidi wangejengewa mazingira kama tunayotaka kuyafanyia sasa hivi, naamini wangeweza kufanya miujiza. Kwa sababu wengine wana wito wanajitolea katika mazingira magumu, lakini bado wanafanya kazi kwa uaminifu, ingawaje kuna wale wachache ambao nasema Mhe. Waziri akipata nafasi basi na hawa ndio vijipu vidogo vidogo, aidha kutumbuliwa kabisa au kutibiwa ili viweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, mimi ningependa kuzungumzia katika ukurasa wa 27 nina *point* c, d, na p. Katika hizi *point* ile ya kusema kwamba kuhudumia wagonjwa wa nje na ndani kwa mujibu wa maadili ya kidaktari. Naamini kabisa hao watendaji wakifanya kazi vizuri na wakazingatia maadili ya madaktari wanaweza kufanya kazi vizuri sana.

Mimi napenda kuwaamini na kusema kwamba Wazanzibari ni wao ambao wana upendo, isipokuwa wakisikitishwa kidogo wanakuwa na hasira na yale mambo ya kusema ya muhali. Muhali unakuwemo na mara nyengine ari; aa, kama hivyo basi na liwe. Lakini naamini wakisaidiwa wanaweza kufanya kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, nina mfano hai katika hili kwamba katika Chuo chetu cha Afya tunaweza kuwapitisha watoto wengi waliosoma pale, lakini kuna mtoto mmoja aliwahi kusoma mahali pale ni mwaka juzi tu, ameweza kupata kazi nje ya nchi baada ya kwenda kufanya *interview* na kuvutana kwamba chuo cha Zanzibar labda hakitoi watoto walioiva ipasavyo. Lakini katika *interview* ya watu 13 alipatikana yeye mmoja tu na hasa alikuja kupatikana pale walipompeleka kwenye *practical. (Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kukwambia hasa Zanzibar kwenye masuala ya *practical* watoto wetu wanafanya *practice* kwa hali ya mazingira magumu, lakini wanafanya vizuri sana. Kwa sababu chuo kile kinawashirikisha moja kwa moja kufanya kazi na watendaji walioko katika sehemu za hospitali. Kwa misingi hiyo kwamba wakipewa nafasi ya kuweza kufundishiwa pale na kikafanywa kama ni chuo kitakachoweza kuwasaidia na kuwaandaa watoto naamini watafanya kazi nzuri zaidi kuliko hiyo tunayoitarajia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine ni katika kushajihisha mpango wa kuendeleza mipango ya uwezeshaji kwa uendelezaji wa afya na ustawi kwa ujumla kwa watu wa

Zanzibar. Hii kwa katika ukurasa wa 27(d). Mimi nikitaka kusema kwamba, katika hili naomba nisisitize sana kwa sababu kuna suala zima la bima. Bima ya Afya kama kila mwananchi atachangiwa ataweza kusaidiwa kwa namna moja au nyengine na kila mtoto atakaezaliwa katika familia yoyote ile akapewa suala la bima nadhani tutasaidiana sana, itakuwa ni njia moja wapo ya kujenga upendo na umoja katika wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa sababu mgonjwa sio kama kila siku anaumwa, hatuumwi sote kwa mara moja kwa maana yule ambaye haumwi kwa mwaka mzima anakuwa amechangia watu watano au sita kwa bima yake moja, kwa maana ya kwamba, hata lile suala linalowagusa wanawake wanaoachwa na watoto inapovunjika ndoa kama mtu ameshachangiwa katika bima ile, inamsaidia naye pia kumuondosha hofu na fadhaa ya kuendelea kulea watoto anaoachiwa pale masuala yanapokuja ya uharibifu wa ndoa. Hawa wale wanaopata watoto katika umri mdogo, wanaokuwa hawajaweza kuolewa, nao pia wakiwa katika suala la bima wanaweza wakachangiwa vizuri.

Pia kama Wizara yangu ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuna masuala mengi tu ya mikopo wale ambao watakuwa hawawezi kabisa wanaweza kukopa basi, kwa sababu bima yenyewe kuchangia nadhani shilingi 50,000 tu, ukichangia shilingi 50,000 kwa mwaka si sawa na pale unapoumwa ghafla kupelekwa hospitali ikafika mamilioni ya pesa au malaki, kipimo kimoja tu kinakusumbua kuweza kupima. Kama tulivyoelimishwa hivi juzi tu kusema kwamba tunaweza kuruhusiwa kwenda kutibiwa katika sehemu za hospitali mbali mbali za *private* yoyote utakayotaka Tanzania. Sio Watanzania Visiwani peke yake, hata Tanzania Bara. Kwa hiyo, hilo litatusaidia kuona kwamba ukishachangia ile una hakiba ya kwenda na kuishi katika hali ya amani.

Jengine ni katika kipengele cha (p), Kushirikiana na Vyuo vilivyoanzishwa ndani ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Chuo chengine kitakachotambulika katika Elimu na Mafunzo. Kama nilivyosema hapo awali kuhakikisha kwamba tukiwa tunashirikiana na hawa tunapata kupanuliwa mawazo zaidi watakapotembeleana, watakaposhirikiana na ninadhani pia tunapata michango mingi sana kutoka nchini nje. Mimi tangu nimeanza kukaa kwenye meza yangu nimeona watu wengi sana wanaokuja wa nchi za nje wanaokuwa ni *volunteers* ambao katika ku-*volunteer* kule naamini wanajifunza hao watoto wanaokuwa nao. Kwa misingi hiyo na wao kesho na kesho kutwa wanaweza wakahitajika hawa wakenda wakawa ni *volunteer* katika sehemu nyengine za nchi duniani.

Mhe. Spika, labda kabla sijamaliza nipende kusema tu, ningependa kuwaomba sana wizara itakapoanza kazi kuhakikisha kwamba wanapitia maadili ya kihospitali. Wafanyakazi wote wanapewa kazi wengine wanaachwa muda mrefu hawapandishwi vyeo, wanakaa muda mrefu wanakuwa hawapewi katika semina zinazostahili, mazingira ya utendaji wa kazi, vifaa vya kufanyia kazi vinakuwa katika ugumu. Lakini kama itapitishwa kuhakikisha kwamba hii inaweza kujitegemea, naamini mambo mengi sana yatakuwa *set about* na wao wenyewe watafanya kazi kwa amani pasipokuwa kunyooshewa mikono tu kwamba labda hamfanyi vizuri na pia kama itakuwa inawezekana kukawa na *incentives* nyingi tu. Kwa sababu kuna wakati mwengine mtendaji wa wizara anaweza akafanyakazi katika muda usio faa akafanya kwa masaa mengi, lakini hata kile cha kutoka anajua anakwenda nyumbani hajui anakwenda kufanya nini.

Labda *incentives* zitakazoweza kupangwa vizuri kwa makusudi na viongozi wa wizara inaweza ikawatia moyo kendelea kufanya kazi vizuri na kupata kwa urahisi na kupingana na haya masuala ya unyanyasaji na udhalilishaji. Ikiwa kuna vipimo sahihi vitakavyokuwa vinasaidiwa pia hii haitoshelezi kwa mtoto kwenda kumpima kipimo tu cha kuona kuwa ameharibiwa, katika kuharibiwa kule kuna mambo mengine yanaashiria kutoka kwa huyu mtu mwengine kuingia kwenye mwili wa mtoto mdogo inawezekana ameambukizwa masuala ya Ukimwi inawezekana magonjwa ya zinaa anaweza kuambukizwa mambo chungu nzima.

Kama hii itapewa rufaa ya kuweza kufanyia kazi na kuwa na vipimo vya kutosha naamini kabisa hata watoto wakati wanasubiri masuala ya kufatilia sheria zinafanyaje na wao watakuwa katika mazingira mazuri ya kutoweza kuambukizwa pasipokuwa na maana.

Mhe. Spika, ningependa kusema tu kwamba kila wakati maisha ya pamoja ya kila mahala yanasaidia kwa wazazi na kila mmoja. Kwa hiyo, napenda nitoe wito kwa ndugu zangu wote Wazanzibari tujitahidi sana kujiunga na Mfuko wa Bima ili tusaidiane kwa namna moja au nyengine.

Pia natoa wito kwa viongozi wetu Wawakilishi mtoe elimu kwa wale mtakaoweza na kama Mwenyezi Mungu atawajaalia kupata michango miwili mitatu kuwasaidia wale ambao hawawezi kabisa basi wasaidiwe, ili waweze kufaidika au kuwaboresha kuwatafutia mazingira ya kuweza kupata mikopo kwa urahisi ambayo itawatia moyo.

Mhe. Spika, nisingependa kusema mengi wengi wameshachangia na ukishachangiwa mwisho unakuwa unaarudia mambo ambayo yameshachangia. Napenda niseme tu kwa moyo msafi kwa moyo mmoja na kwa nguvu kabisa kuweza kuchangia kabisa kuunga mkono mswada huu ulioletwa mezani kwenu kwa kipindi na muda muafaka, ili ipitishwe tuweze kuwapa nafasi Wizara ya Afya kufanyakazi vizuri na kuleta matokeo mema. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said): Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote kwanza napenda kumpongeza Mhe. Dkt Ali Mohd Shein kwa kumteuwa Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo kuwa Waziri wa Afya na hii kwa sababu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo atafanyakazi kwa mujibu wa mirathi.

Mimi nikiwa na fahamu yangu na uwezo wangu na akili nimegundua na niliona Marehemu Thabit Kombo kuwa Waziri wa Afya kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mambo yalikuwa mazuri sana na wizara ilikwenda vizuri sana, sasa hii ni dalili ya kwamba waziri anayehusika na wizara hii katika awamu hii naamini atafuata nyayo za babaake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ningetaka niseme kwamba Baraza la Wawakilishi kulinda na kutetea sera ya Chama cha Mapinduzi Zanzibar inawezekana. Hoja ya kuleta mswada huu ni miongoni mwa ahadi za Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanapata huduma za afya bora ndani ya nchi yao. Kwa mantiki hiyo hakuna sababu ya mswada huu kuwa na masuala mengi, kwa sababu Chama cha Mapinduzi kinatekeleza ilani yake na ndio maana ilani hiyo ilipendwa na ikakubaliwa na wananchi ndio wakatoa ridhaa kwa asilimia 91% kumpa Mhe. Dkt Ali Mohd Shein awe Rais wa Zanzibar. Sasa yanapokuja mambo kama haya katika Baraza la Wawakilishi ni kusema kwamba zile ahadi mlizozitoa Chama cha Mapinduzi sasa mnazitekeleza. (*Makofi*)

Wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba mswada huu unapita na hatimae tunaacha serikali inasimamia shughuli hizi ambazo zitawapelekea Wazanzibari kupata afya bora katika nchi yao. Imani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba mataifa ya karibu ya Zanzibar Kenya, Uganda, Ruwanda, Burundi na nchi nyengine wanakuja Zanzibar kupata huduma ya afya kutokana na mikakati ya serikali ilivyojipanga. (*Makofi*)

Sasa usifikirie kwamba labda mkakati huu ni mkatati uliokuwa labda unakwenda kuanzishwa kwa misingi ya kwamba labda watu wanapiga ramli tayari serikali imeshajipanga nini watafanya, nini watakusudia na malengo gani yatafikia Zanzibar kujitangaza kitaifa na kimataifa.

Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi kama ni Wawakilishi kuwaelimisha wananchi vijijini kujua haki hii, kwamba ni haki yao ya msingi na ni miongoni mwa ahadi za serikali kutekeleza yale yaliobora juu yao. Ni wajibu wetu Wawakilishi kuelimisha tena wananchi kuona kwamba malengo haya yanaletwa kwa madhumuni ya ile ahadi ambayo itatelekezwa katika awamu hii, ili kuwafikishia malengo yao ya kupata afya bora.

Wawakilishi tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba Serikali iliyoko madarakani inafanyakazi yake kwa mujibu wa taratibu za kuleta huduma kwa wananchi inavyotakiwa.

Kwa hiyo, ni wajibu wenu kuona kwamba taasisi hii inaanzishwa na kasoro zake mnazifatilia, ili kutuambia kama serikali kuweka vizuri mambo yale ambayo yanatakiwa Zanzibar ifikie hatua nzuri ile inayotakiwa. Tunataka Zanzibar kuifanyia mabadiliko makubwa na tunakwenda na taasisi moja baada ya nyengine msione ajabu hili kwamba liko leo V. I Lenin, lakini si ajabu mkaja kulikuta suala hili nalo Abdalla Mzee Hospitali, si ajabu mkaja mkalikuta limezalishwa na Wete Hospitali, si ajabu mkaja kulikuta na Chake Hospitali kutekeleza sera ya Chama cha Mapinduzi kuifanya serikali iliyoko madarakani kwamba inafanya wajibu wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, serikali hii imejipanga kwa hoja hii, kwa hiyo, napenda kuwatoa wasi wasi Wazanzibari kwamba hoja ya kuwepo afya bure iko pale pale. Lakini haimaanishi kwamba maji yako visimani ikawa leo watu wasinunue ya *drop*, watu wananunua maji ya *drop* na maji yamejaa tele visimani.

Huu ni utamaduni uliozalishwa na nchi mbali mbali duniani hatuanzi sisi tu nchi nyingi zimeshaanza, na kwa vile mazingira haya ya kuweko *facility* bora zaidi kwa wale watu ambao wanatafuta afya Israil wanakawenda *South African,* wanakwenda China, wanakwenda India badala yake waje Zanzibar na huu ndio mkakati wa serikali waje Zanzibar kupata afya bora. Zanzibar ina wataalamu, Zanzibar ina madaktari bora, Zanzibar inaweza kufanya suala hili likatambulika kitaifa na kimataifa.

Hayo yote yaliyojitokeza sisi kama serikali tunapiga mstari mwekundu, madaktari waje tushirikiane tuifanye taasisi hii iwe bora katika Afrika Mashariki na Kati. Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza kabisa kwa heshima kubwa naomba nitoe shukurani kwako kwa kuniruhusu kufika hapa, ili niseme yale machache yanayohusu Hospitali yetu ya Mnazi mmoja.

Mhe. Spika, napenda pia nichukuwe nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi zake kwa ushauri pamoja na maelekezo yake yenye mashiko ya kuitaka Hospitali ya Mnazi mmoja iondoke ilipo na kuelekea katika huduma bora na za kiwango cha hali ya juu kwa wananchi wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunawapongeza kwa dhati wahisani na Wajumbe wa vikao vilivyokutana na kujadili na kupanga suala zima la Hospitali ya Mnazi mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa na kupanga uwendeshaji wake kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waelewe kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dkt. Ali Mohammed Shein Rais mwenye upendo mkubwa kwa Wazanzibari wote muaminifu na muadilifu, anaiongoza nchi hii ya Zanzibar kwa busara haiwezi kuwa na nia mbaya kwa wananchi wake. Serikali hii ina nia njema kwa wananchi wote na bila ya ubaguzi wowote na ndio maana imeleta mswada huu mbele yenu Wawakilishi wa wananchi ili muone umuhimu wa afya kwa wananchi na wapiga kura wenu.

Mhe. Spika, waswahili wanasema "mwanzo wa jambo lolote ni mgumu", na mimi nathibitisha kwa kusema kwamba hasa mwanzo wa jambo la kheri ni mgumu kama hili la Hospitali ya Mnazi mmoja lililo mbele yenu leo.

Mhe. Spika, baadhi ya watu hasa wale wasioitakia kheri nchi yetu na sera yetu ya Mapinduzi Daima wanathubutu kupotosha kwa kukejeli maendeleo yaliyopatikana baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, wameishiwa. Kwani kabla ya Mapinduzi tulikuwa idadi yetu hatuzidi watu laki tatu na kidogo. Lakini sasa tupo zaidi ya milioni moja laki tano na kidogo.

Watu hawa wanakejeli kwa kusema kwamba Mapinduzi ya Zanzibar hayakufanya kitu, yaani ni bora kulipokuwa kabla ya Mapinduzi kulikoni sasa hivi wanakeli yale matunda zile neema ambazo zimepatika baada ya Mapinduzi.

Mimi nataka waambiwe kwamba wajue kwamba Mapinduzi yamefanya jambo kubwa sana kabla ya Mapinduzi nataka niwakumbushe ingawaje nilikuwa

sifahamu, lakini historia nimeisoma na nimeielewa na nimesomeshwa na walimu makini, kwamba kabla ya Mapinduzi ilikuwa huwezi kutapata matibabu mazuri kama hujataka kwanza kabila lako ni nani, lakini pia unatokana katika ukoo gani.

Tuangalie sasa unakwenda hospitali unatibiwa, unalazwa, unafanyiwa upereshen unatoka umepoa bila ya kujulikana wewe kabila lako nani na katika cheti cha hospitali za Zanzibar hakuna neno kabila haitakiwi kujulikana wewe kabila lako ni nani, unatibiwa bila ya kujulikana wewe kabila lako ni nani na huduma unapewa sawa sawa na yoyote atakaekuja. Hili naomba sana wale ambao hawaitakii mema serikali yetu basi waliangalie kwa kina wasikae tu na kupotosha wananchi.

Mhe. Spika, naomba sasa kidogo nieleze kwamba uwasilishaji wa mswada huu ni hatua ya awali ya kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi moja kuweza kujitegemea kifedha na utawala. Hospitali baada ya kupata uwezo wa kukusanya fedha na kufanya matumizi itaendelea kujiwekea malengo yake yenyewe ikiwemo utowaji wa huduma kwa mujibu wa mahitaji. Huduma zitakazoongezeka zinaziwezesha hospitali hiyo kutoa huduma za rufaa kwa wagonjwa wa ndani na nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi mmoja itakapojitegemea itakuwa na bodi huru itakayosimamia menejimenti ya hospitali. Miongoni mwa kazi za bodi hiyo itakuwa ni kubuni na kusimamia vyanzo na mapato. Kwa sasa vyanzo vikuu vya mapato ni Maabara, Mafunzo ya Madaktari wa nje, tafiti mbali mbali, huduma ya *first track*, maegesho ya magari na kadhalika ambayo kwa mfumo wa sasa baadhi yake makusanyo hupelekwa moja kwa moja Hazina, pale tu hospitali itakapoaza kujitegemea. Bodi ya taasisi hiyo itasimamia makusanyo ya vianzo vyote vya sasa na vitakavyaonziswa.

Mhe. Spika, sambamba na kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi mmoja, serikali inaendeleza *course* za madaktari zinazotolewa na *SUZA* na kuingozea hadhi kukidhi matakwa ya Kamisheni ya Elimu ya Juu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Naomba kulijuulisha Baraza lako tukufu kwamba serikali imekamilisha mpango wa kukiunganisha Chuo cha Sayansi za Afya Mbweni kuwa ni sehemu ya *SUZA*, jambo ambalo litaongeza wataalamu wenye hadhi sio tu kwa upande wa madaktari, bali pia kwa upande wa wataalamu wengine wenye afya.

Mhe. Spika, naomba sasa kidogo nianze kufafanua au kujibu changamoto au ushauri ambao imetolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na hasa naanza na Mhe. Ussi Yahya Haji.

Mhe. Ussi Yahya Haji ametushauri zaidi kwa kutwambia kwamba wataalamu watakaofanya kazi wapatiwe mikataba maalum usiowaruhusu kuondoka katika hospitali hii na kuwe na masharti yenye manufaa kwao na kwa hospitali. Pia amesema kuwepo na Idara ya kitengo cha usalama ndani ya hospitali.

Mhe. Ussi Yahya Haji kaendelea kutushauri kwamba majengo au wodi za hospitali hiyo ziwe na majina ya waasisi wa Serikali yetu ya Mapinduzi kwa mfano Mhe. Abeid Aman Karume, Mhe. Thabit Kombo Jecha, Mhe. Seif Bakar Omar, Mhe. Ramadhan Haji Faki n.k.

Mimi napenda nichukuwe nafasi hii kumueleza Mhe. Ussi Yahya Haji kwamba hili tutalichukuwa litajadiliwa na vikao vinavyohusika kwa sababu huu mswada mpaka unafika hapa leo ni kwamba umeshajadiliwa sana katika vikao vingi na leo ukaletwa mbele yenu ili muupitishe. Kwa hiyo, hili tunalipokea kwa dhati litachukuliwa lijadiliwe na *in shaa Allah* kwa uwezo wa *Allah* kwa sababu ni ushauri mzuri basi utaingia katika mkondo huu wa hospitali yetu ya rufaa.

Mhe. Spika, naomba sana nichukuwe nafasi hii ya mwisho kuwaomba Wajumbe wa Baraza hili kwa heshima kubwa waangalie sana mswada wetu huu kwamba uletewa kwenu Waheshimiwa Wawaikilishi wa wananchi kwa maslahi ya wananchi wenyewe na nasio kwa maslahi ya kitu chengine chochote. Serikali ina nia njema sana na wananchi wake, serikali hii inaongozwa sana Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein ina busara ina nia njema kwa wananchi inayowaongoza na kweli nia na mantiki ya mswada huu kuletwa kwenu ni kwamba muukubali, muujadili kwanza, mtoe changamoto, mtoe ushauri lakini hatimae muukubali ni wananchi wetu waendelee kupata matibabu bure kama sera yetu ya Mapinduzi Daima inavyoeleza na kuondokana na matatizo ya matibabu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, lakini pia naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa na afya njema na kuwemo katika Baraza hili tukufu la wananchi na pia tukiwa tunajadili masuala ya afya ambayo yanamgusa moja kwa moja mwananchi wa Zanzibar.

Pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii Mhe. Spika, na natumai muda utakuwa wa kututosha, kwa sababu michango ni mingi sana. Lakini naomba kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia, kutushauri na kutupa mawazo yao na maoni mbali mbali na kuturekebisha baadhi ya sehemu ambapo tumechukuwa yale marekebisho na tutayafanyia kazi.

Mhe. Spika, naomba pia nichukuwe fursa ya kuwashukuru sana Kamati ya Maendeleo, Wanawake, Afya, Elimu na Ustawi wa Jamii, kwa kweli mchango wao ulikuwa mkubwa sana, tumekaa nao kwa muda mrefu sana, tumejadiliana baadhi ya sehemu tumevutana, lakini yote ni kwa ajili ya kumtumikia mwananchi wa Zanzibar. Ninawashukuru sana na ninaomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hiyo wakiongozwa na:-

1. Mhe. Mwinyihaji Mwadini Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
4. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Mjumbe
6. Mhe. Makame Said Juma - Mjumbe
7. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
8. Ndg. Aziza Waziri Kheri - Katibu
9. Ndg. Khamis Ahmada Haji - Katibu

Ndugu Salum ambae ni Katibu aliyekuwa wa ziada aliyetusaidia sana na mimi pia kunisaidia sana kwa upande wa sheria.

Naomba pia Mhe. Spika, shukurani za pekee kabisa nizipeleke kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu. Maana lazima tuseme ukweli huu Mswada ni kidogo wa muda mrefu sana na tumekuwa tukienda nao mbio sana na Mhe. Mwanasheria Mkuu nafasi yake ni kubwa sana aliyeongezea nguvu na kutuwekeza vizuri hadi ukafika hapa na anaendelea kutushauri Mhe. Said Hassan Said. Naomba nimshukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba niwatambue waliochangia wote kwa maandishi na wale waliochangia kwa maelezo mazuri kabisa ya kujenga sheria hii na kutuunga mkono kwa asilimia mia moja. Nao ni:

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Nassor Salim Ali

5. Mhe. Suleiman Sarahan Said
6. Mhe. Simai Mohammed Said
7. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
8. Mhe.Waziri wa Uwezeshaji, Kazi, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
9. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
10. Mhe. Mwanasheria Mkuu
11. Mhe. Mohamed Said Mohamed
12. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
13. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Kwa maandishi katupa historia kubwa sana na pana ambayo anaifahamu yeye mwenyewe.
14. Mhe. Rashid Makame Shamsi
15. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
16. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
17. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
18. Mhe. Hamza Hassan Juma
19. Mhe. Miraji Khamis Mussa
20. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
21. Mhe. Panya Ali Abdalla
22. Mhe. Omar Seif Abeid
23. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara (Maalum)
24. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
25. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
26. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Kwa maandishi

Mhe. Spika, naomba kwanza moja kwa moja niende kwenye sheria lakini kabla sijaenda kwenye sheria naomba nitoe shukurani za kipekee kabisa kwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye ana nia njema sana kwa wananchi wa Zanzibar, amekuwa akitupa muongozo mzuri kutuelekeza sisi Wizara ya Afya pamoja na uongozi wetu wa Wizara ya Afya. Jambo kubwa ambalo tunafaidika sana sisi Wizara ya Afya, ninaweza kusema ni upendeleo maalum. Ni kupata zile changamoto ama pia *experience* yake, uzoefu aliokuwa nao Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na Hospitali ya Mnazi Mmoja. (*Makofi*)

Naomba niseme ametumia zaidi ya miaka 30 akiwepo yeye mwenyewe pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Huo ni uzoefu mkubwa sana ambao daima amekuwa akitupa katika kutuongoza kuelekea hadi kufikia sheria hii kuletwa hapa Barazani.

Naomba nimtambue Mhe. Ussi Yahya Haji kwa sababu yeye alitambuliwa pia na Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa mchango wake.

Naomba moja kwa moja Mhe. Spika, niende kwenye Mswada na nitaanza na mfumo huu kwanza kabla ya kwenda kwenye michango ya Wajumbe. Na nitaanzia moja kwa moja kwenye ukurasa wa 26 wa Mswada wetu Kifungu cha 1 kabisa.

Sheria yetu ya Kiingereza Mhe. Spika, naomba niisome kwa Kiingereza maana hii ndiyo iliyoletwa mwanzo kabisa. Kifungu cha 1 katika Sheria ya Kiingereza ni ukurasa wa 35, *"This Act may cited as the Mnazi Mmoja Hospital Act, 2016 and shall come into operation on such date as the Minister may by notice published in the Gazette appoint"*.

Sasa hapa hakuna neno *National Hospitali*, hakuna taifa. Naomba sana kwamba tuanzie na hatua hii. Hii ndiyo hatua ya awali. Huko baadae tunakoelekea mbele, kwa sababu kuna Waheshimiwa hapa walichangia kuhusiana na Hospitali ya Binguni itakayojengwa hapa. Hospitali hii ni kubwa na itakuwa ni ya aina yake na imetamkwa wazi na imetajwa wazi katika ukurasa wa 76 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa naomba sana tubakie na tafsiri hii iliyokuwepo hapa katika sheria yetu. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ya 2016 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri mwenye dhamana ya Afya ataitangaza katika gazeti rasmi la serikali ambayo inaendana na sheria ya Kiingereza. Neno taifa tusiende nalo kwa sasa.

Mhe. Spika, pia tunaomba sana katika neno "Hospitali" maana yake. Ni Hospitali ya taifa ya Mnazi Mmoja. Hili neno taifa lisiwepo hapa, tunaomba sana kwa sababu tunachukua kule kule kwenye tafsiri ya Kiingereza, ninarudi tena kwenye tafsiri ya Kiingereza. *Hospital means Mnazi Mmoja established under this section 3(1) of this Act* ambayo imetajwa hapa.

Hii nilieleza jana katika ile Hati ya Dharura ya Mhe. Rais. Imeletwa hapa kwa lengo lile la kufikia kuwa hospitali ya kuweza kufundishia kwa ajili ya zile kozi ambazo watoto wetu ndizo wanazosoma sasa hivi kwa ajili ya udaktari kuweza kukubalika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo bado kuelekea kwenye taifa, taifa tutafikia huko Binguni na kwengineko tutakapofikia. Ninaomba nitumie fursa hii pia kutoa tafsiri ya neno rufaa. Maana limeulizwa na Wajumbe wengi sana.

Mhe. Spika, neno rufaa nilikuwa nikitazama kwenye *internet* sasa hivi, kila nchi imejipangia ngazi yake ya rufaa. Sisi ngazi yetu kwa Zanzibar ya rufaa ni Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini hatuwezi kuita ya rufaa kwa sababu tukishindwa Hospitali ya Mnazi Mmoja sisi tuna mikataba na Hospitali ya Muhimbili; tunawapeleka wagonjwa wetu Muhimbili. Kwa hivyo, kwetu sisi Muhimbili pia inakuwa ya rufaa. Tukishindwa kwa Muhimbili ama KMC ambayo pia tunayo mkataba nao tunawapeleka nchini India. Kwa hivyo kwetu sisi pia India inaweza kutafsiriwa kuwa ni ya rufaa. Hivyo tukilitumia neno rufaa tutakuwa hapa tunajibana sisi wenyewe kwa sababu haikufikia kiwango kile.

Tupo katika kuelekea kwenda rufaa ndiyo maana likatumika neno kama ya rufaa. Kuna Wajumbe wamehoji na Mhe. Hamza Hassan Juma ni mmoja wapo kwamba kwa nini Kifungu cha 4 (1) (a) Kutoa huduma kama Hospitali ya Rufaa. Huko ndiko tunakotaka kuelekea.

Sasa pale patakapokuwa labda Hospitali Binguni pameshakamilika, huduma zile za rufaa zitaelekezwa huko. Lakini kwa sasa tafsiri ya rufaa kila nchi hata kule India nako ambako kwenye hospitali nyingi sana, basi huduma za rufaa zinatofautiana baina ya *state* na *state*. *State of Maharashtra* rufaa yake tofauti na *state of Tamid Nadu*. Tamil Nadu akishindwa anapelekwa kwengine *Hyderabad*. *Hyderabad* akishindwa anamleta huku Maharashtra. Kwa hivyo hata kule *definition* zao tukiangalia kwenye *internet* pia za rufaa ni tofauti.

Kwetu sisi kwa hapa sasa hivi tutaendelea kutoa huduma hizo kama ilivyoelezwa kama ni Hospitali ya Rufaa kwetu sisi. Tukishindwa sisi pale *next line of command* ni Hospitali ya Muhimbili kwetu sisi, ndiyo hospitali ya kirufaa ya taifa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ikishindikana pale tunakwenda mbele zaidi.

Kuna tuliowapeleka India, kuna tuliowapeleka Israel, kuna tuliowapeleka Afrika Kusini na kila maradhi yana rufaa yake. Haiwezekani maradhi yote rufaa yake yakawa India haiwezekani. Kuna wataalamu bingwa wengine wapo Afrika Kusini, kuna wale wataalamu bingwa ambao wanapasua, tumeshapeleka watoto wetu sisi kwa sababu ubingwa mkubwa kama hawa madaktari wa watoto wadogo *pediatric*. Kwa sababu wale wana-*deal* na vitu vidogo sana ndani ya mwili. Hata moyo wa mtoto mdogo, mtoto mchanga unakuwa mdogo sana.

Kwa hivyo hata operesheni yake inahitaji taaluma kubwa sana. Wale tumekuwa tukishirikiana na mashirika yale ya Israel tukiwapeleka Israel. Hivyo naomba

sana hapa tukubaliwe Kifungu hiki cha 4 (1) (a) kiendelee kubakia kutoa huduma kama hospitali ya rufaa na kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza alisema kwamba alitania ambaye ni rafiki yangu sana, amenitania anasema tunataka pepo lakini tunaogopa kufa. Hata kule hospitali katika nafasi hii nimegundua jambo moja, hata kule hospitali kuna daraja na daraja na daraja. Ukishatiwa *ICU* watu wengi wanakuwa wanahisi laa! hapa vipi. Lakini mara nyingi tunakuwa sisi watu wa afya tunatarajia kwamba yule mgonjwa atatoka *ICU*.

Kwa hivyo naomba niseme Mhe. Hamza kuwa tunataka pepo hatuogopi kufa ila tunataka kwenda hatua kwa hatua, hatua kwa hatua. Tuanze na usingizi kwanza, tuanze na ndoto nzito ama usingizi mzito, tuanze na yale madawa ya akina *doctor* Jamala kutolewa fahamu ukapotea kabisa ukawa kama hupo, unasaidiwa mpaka kupumua ili tufikie huko unakosema wewe kwenye kufa kupata hiyo pepo yenyewe. Maana tunataka kuelekea kwenye pepo. Mimi nimekuelewa ulivyozungumza. Kwa hivyo ninakuomba sana na ninaomba Waheshimiwa Wajumbe twende hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, neno taifa nimeshali-*cover* hapo. Neno rufaa nimeshalitolea *definition* yake. Naomba twende kwenye Kifungu cha 4 (1) (i). Hiki kilizungumziwa sana na ninaomba kidogo nitoe ufafanuzi mdogo tu. Kifungu (i) kinasomeka, "Kuweka mazingira mazuri ya kusaidia mafunzo ya wafanyakazi wa afya kwa hospitali na yanayohusiana na sayansi au taasisi nyengine zozote zinazotoa mafunzo ya afya". Hii ni kwa lengo lile lile la kuweza kushirikiana na taasisi nyenginezo.

Mfano *SUZA*; kesho na keshokutwa Mwenyezi Mungu akitujaalia tusijadharau sisi wenyewe. Tayari kuna wanafunzi wanatoka nchi zilizoendelea wanakuja kusoma kichocho Pemba. *Public Health Laboratory (PHL)* imeshatoa *PhD* kadhaa pale iliopo Pemba. Tusijidharau sisi wenyewe. Tukijidharau sisi wenyewe nani atakayekuja kututukuza. Lazima tujitukuze sisi wenyewe, tuanze kujitukuza sisi wenyewe na hili linawezekana. Kwa sababu madaktari 38 walio-*graduate* Wazanzibari wamesomeshwa hapa hapa Zanzibar. Leo tayari wanafanya kazi na wanatambulikana kama madaktari kamili.

Nani aliyekuwa na ndoto kwamba Zanzibar siku moja tungezalisha madaktari wetu wenyewe. Zamani madaktari walikuwa wanakuja kutoka sehemu mbali mbali kufanya kazi na vijana wetu walikuwa wanakwenda sehemu nyengine

kusomea udaktari wanarudi, lakini leo Zanzibar imeweza kuzalisha madaktari. (*Makofi*)

Kwa hivyo naomba Kifungu hiki kieleweke kwamba kitakuwa ndiyo chenye kufanya kazi kwenye hiyo taaluma. Na siyo *SUZA* tu hata Hospitali ya Muhimbili wanaweza kuleta watu wao, hata *University of Dar es Salaam*, *universities* zote za Tanzania na *universities* nyengine mbali mbali ulimwenguni.

Hivi sasa hapa tulipo tayari tunawapokea wanafunzi kutoka nchi mbali mbali ambao wanakuja kufanya mafunzo yao ya *field* pale Hospitali ya Mnazi Mmoja na wanatiliwa *marks* na hawa hawa madaktari wetu. Madaktari wetu hawa wataalamu wanawatilia *marks* katika karatasi zao na wanarudi na *marks* hizo kwenda hivyo Vyuo Vikuu vya nje. Naomba niseme kwamba kule Vyuo Vikuu vya nje tunatambulikana na ndiyo maana wanatiliwa *marks* pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tusikidharau cha kwetu, tukidumishe.

Kifungu cha 4 (1) (n), "Kusimamia na kudhibiti kuibuka kwa maradhi ya mripuko kwa umuhimu wa afya kwa jamii". Hapa Mhe. Mohamed Said Mohamed alichangia pia, naomba kifungu hichi tukibakishe, kwa sababu hichi kinachangia pia kutoa elimu ya kinga. Kama itakuwa ni teaching hospital pale mambo mbali mbali yatakuwa yanafanyika. Baada ya kuchunguza yale maradhi ya kipindupindu, kuchunguza *vibrio, cholera, vibrio uga one, two* na wengine wote, baada ya hapo hapa panaweza kutolewa taaluma nyengine ya kinga. Ndiyo maana tumetaka kifungu hiki nacho kiwepo.

Ninakwenda Kifungu hicho hicho cha 4 (1) (s) ambacho ni cha mwisho, tayari pale suala la Mhe. Hamza Hassan Juma limejibiwa kwamba hapa inawezekana kufanya kazi nyengine ambayo itakuwa ni muhimu au yenye kuhusiana na madhumuni ya kazi zake. Kwa hivyo hapa tayari kazi za hospitali wameshapewa fursa ya wao wenyewe kukaa na kubuni, ile Bodi imeshakaa wataweza kubuni hapa labda tunataka kitu *extra* kuongeza haiwabani. Kifungu hiki hakiwabani kinawapa fursa.

Labda niseme nikubaliane na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Mohamed Said Mohamed pia alichangia hapa, ili kurahisisha hapa tuandike hivi, "Kufanya kazi nyenginezo zozote ambazo Bodi itaona ni muhimu". Bodi ipewe fursa ya kazi zile kuona umuhimu. Ninaamini Makatibu watakaa na wataalamu wetu watarekebisha hilo. Hilo naomba nilikubali kwamba Bodi inaweza kuona in *future*, huko tunakokwenda kuna *expansion* kuna Binguni, pengine hii hii Mnazi Mmoja sheria hii itaondoka pale Hospitali ya Mnazi Mmoja itahamia

Hospitali ya Binguni. Kwa hivyo Bodi inaweza ikaona kwamba aah! Sasa hivi tunahitaji kuongeza na hiki na hiki. Pengine zitakuja *universities* kubwa huko duniani watataka kufunga mkataba na Hospitali ya Mnazi Mmoja yetu hii hii. Kwa hivyo Bodi itaweza kufanya maamuzi hayo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba sasa niende kwenye Sehemu ya Tatu yenye Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwenye Kifungu cha 5 (2) (e), hapa wametajwa wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi. Naomba nimpongeze sana Mhe. Simai Mohammed Said ametoa mifano mizuri sana ambayo ni mifano hai ambayo ipo. Hapa mimi naomba niseme kwamba tusiweke kuwa lazima huyu mfanyabiashara awe anatokana na sekta ya afya; tutakuwa tunanyima sisi wenyewe. Hapa tuwaache kwamba wawakilishi hawa wawili kutoka sekta ya afya iwe huru kuteuliwa. Bila shaka watu watajadiliana nao na kadhalika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Rais yeye anamteuwa mwenyekiti lakini hawa wanateuliwa na Waziri kwa mujibu wa sheria hii. Sasa naomba sana tumuachie Waziri. Mifano aliyetaja Mhe. Simai Mohammed Said ambayo mimi nisingependa kurudia, hawa watu wengine wawekezaji wakubwa. Wanawekeza kwenye majumba, wanawekeza huko Fumba, nyinyi mushakwenda kuona, wanaweza *Mtoni Marine* nyinyi mushakwenda kuwaona. Wale watu watakaokuja kukaa huko Fumba na *Mtoni Marine* watataka kutibiwa wapi. Ili zile nyumba ziwe na hadhi kubwa na ziwe na thamani, si vizuri ukaziambatanisha na *package* ya afya ama siyo jamani.

Mhe. Spika, ninamshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwenye *National Health Insurance*, tumeliona hili. Kwa hivyo ili zile nyumba na wale watakaokuja kukaa wapate thamani kubwa zaidi, basi ikiwa kuna afya bora na afya ambayo ipo kiwango cha juu kabisa. Ni kivutio kimoja wapo kwa wawekezaji pia. Sasa ninaomba wale waliotajwa Mwenyezi Mungu akijaalia ikishapita sheria hii wakiombwa kile wanachokitoa, wakitolee kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja basi mambo mengi yatakaa vizuri. Kwa sababu watakuwa hawakitolei kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja lakini pia wanajitolea katika zile *investments* zao walizojiwekea. Wafanyabiashara maisha wanafikia huku na kule. Hatoi bila ya kuona na yeye ataidika vipi.

Kwa hivyo hawa watakaotoa hapa na wao watakuwa wameshaiona faida. Hata banda lile la Mhe. Jaku Hashim Ayoub nalo pia litamalizika na litakuwa zuri sana. Maana pale Hospitali ya Muhimbili ukenda nje kuna *products* nyingi za Azam zinauzwa wale watakaokuwa wamekwenda Muhimbili. Kuna mikate,

kuna ile *canteen* na kuna mambo mazuri mazuri pale yanauzwa. Kwa hivyo haya yatakuwa yamewezekana kirahisi zaidi.

Kwa hivyo, naomba sana hapa tuwache kwa wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi na hilo tuachiwe sisi Wizara ya Afya pamoja na serikali kuu kuweza kuamua.

Mhe. Spika, namba (4). Nashukuru sana kamati ilirekebisha kidogo katika kifungu cha 5(4). Mwanasheria huyu atakuwa ni kutoka wizara inayohusika na masuala ya afya, ambaye atakuwa ni Katibu wa Bodi, huyu ni Mwanasheria wa Serikali ambaye yuko wizarani. Sisi tuna wanasheria wa serikali, lakini wanasheria wote katika wizara wanatokea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, huyu atakuwa ni Mwanasheria wa Wizara ya Afya mmoja wapo aliokuwemo mule ndani, atateuliwa rasmi kuwa katibu, kama hivi tunavyofanya sasa hivi.

Bahati nzuri mmoja yuko pale juu Mwanasheria wetu wa wizara, namuona mmoja tu mwengine simuoni. Yeye ni Katibu tayari katika bodi kadhaa, ikiwemo bodi ya madaktari, bodi ya wauguzi yeye tayari ni katibu sasa hivi katika bodi kadhaa. Bi Shufaa naomba usimame kidogo upate kuonekana, huyu ndiye Mwanasheria wetu, ahsante. Pahala penyewe ndio hapa hapa pa kupigia debe. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana hili lifanyiwe kidogo marekebisho la kusema kwamba ni Mwanasheria wa Serikali kutoka wizara inayohusika na masuala ya afya, ambaye atakuwa Katibu wa Bodi. Naomba nisogee mbele kwenye michango.

Mhe. Spika, kifungu cha 8(1)(f) pia kilichangiwa sana na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali, naomba nikisome ili kuhakikisha huduma za afya zinatolewa na hospitali zikizingatia vipaumbele vya kuhudumia wananchi, na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika. Hii imesha-*cover* kila kitu, sisi wenyewe tumeshaji-*commit* hapa. Sasa tuwaachie bodi itakayokuja ili waandae zile kanuni zao za kufanyakazi, waandae zile *standards* za kufanyakazi, ili waandae vipi kazi itafanyika, vipi mgonjwa akishafika hospitali ndani ya muda gani aonekane huyo mgonjwa, haya yote yatafanywa na bodi watajiwekea meno, watajiwekea *share* ya kutumbua majipu, wataweka sindano na wataweka kila kitu hii bodi watakuwa na uwezo huo. Itafikia wakati kwamba mgonjwa akishafika pale *emergency* ndani ya dakika 30 anatakiwa awe ameshaonwa na amepatiwa huduma, itafikia bodi watatunga hizo kanuni.

Sasa tuwaachieni bodi watunge kanuni hiyo kwa kujiwekea *standards* na kila baada ya muda wataendelea ku-*improve* zile *standards*. Tunaona hospitali za wenzetu nyengine, wameshajiwekea *standards* kama *emergency* ndani ya nusu saa awe ameshatibiwa, wana zile *chart* zao wanakuwa wanazibandika pale a, b, c, d na kuendelea, ndani ya kipindi fulani atakuwa ameshapatiwa huduma fulani, ndani ya muda fulani *ICU* atakuwa ameshafanyiwa kitu fulani, akikaa ndani ya muda fulani *ICU* anatolewa anapelekwa kwengineko.

Kwa hivyo, haya naomba sana tuwaachie bodi ili waweze kujipangia na kwa sababu wamo wataalamu humu ndani watakubali wao kupanga na watajiwekea zile dhamana.

Mhe. Spika, kifungu (h) kuhakikisha kuwa hospitali inatekeleza wajibu wake kwa wizara, naomba maneno haya yaongezwe ili itakuwa ime- *cover* lile suala la Mhe. Hamza Hassan na Waheshimiwa Wajumbe wengine wengi waliokuwa wanaomba *definition* ya wizara itolewe kule mwanzo.

Mhe. Spika, naomba hapa yaongezwe maneno yafuatayo, kuhakikisha kuwa hospitali inatekeleza wajibu wake kwa wizara yenye dhamana ya afya, maneno "yenye dhamana ya afya" yaongezeke itakuwa imesha-*cover* mpaka *definition* ya wizara kule mbele, tutakuwa hilo tumeshalimaliza. Lakini hapo hapo nikisogea chini kidogo kwenye kifungu (i), kupendekeza masharti ya utoaji wa huduma na maslahi ya ajira kwa wafanyakazi wa hospitali kwa kufuata sheria ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, naomba hili mtukubalie, kwa sababu sheria ya utumishi wa umma ndio sheria mama inayotuongoza sote sisi. Mhe. Hamza Hassan hata ukitikisa kichwa vipi, hawa hawa kamati ya utumishi ya Baraza la Wawakilishi mwisho wao wanaishia wapi, kwenye sheria ile, kuna ile Tume. Samahani ni Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, kukiwa na tatizo inaishia kule kwenye kamisheni, ndio.

Kwa hivyo, hii ni sheria mama, kama kutakuwa na mlolongo wa kisheria, bahati nzuri Mwanasheria Mkuu yupo hapa tutakwenda sambamba. Lakini hii sheria ya utumishi wa umma ndio sheria mama. Ndio maana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora tunamuona yupo, ameshakaa kwenye kiti chake pale. Yeye ndiye msimamizi mkuu wa sheria hii ambayo inatugusa sisi sote kijumla, hakuna mrengo ambao hauguswi, *Judiciary* inaguswa, *Legislative* inaguswa, pamoja na *Executive* yenyewe, sote.

Kwa hivyo, hili naomba sana Mhe. Hamza Hassan, Mhe. Rashid Makame Shamsi ulichangia pia hili, naomba sana na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia hili, naomba sana, kwa sababu vyenginevyo tutaleta mgongano wa kisheria hapa, tusipokwenda kwa sheria hii ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, najua mko katika kututetea, nalielewa hilo, mko katika kutetea maslahi ya madaktari nalielewa hilo. Katika michango yenu nimesikia mnataka daktari na yeye ajihisi kuwa yeye ni daktari, mnataka *nurse* na yeye ajihisi kuwa yeye ni *nurse*, lakini tusilete mgongano wa kisheria. Katika *scheme of service* tunaamini Mhe. Waziri yupo atapanga hizi ni kada maalum, hizi ni kada *very rare professions* hizi watapatiwa mambo yao yatakuwa mazuri.

Mhe. Spika, lakini nikisogea mbele kidogo kwenye kifungu (k) kutoa muongozo na ushauri juu ya uendeshaji wa hospitali, hilo ni jukumu moja wapo, kupendekeza utungwaji wa kanuni na huduma za hospitali. Vile nilivyosema kwamba hawa watakuwa wanapendekeza juu ya kutunga kanuni hizi za huduma ya hospitali. Tunachokosa sasa hivi ni kwamba hatujaweka zile *strictly condition*, kwamba ndani ya muda fulani mtu fulani awe keshapatiwa huduma fulani, ile ukishaweka ina maana yule inabidi achukuliwe hatua. Sasa haya yote yatakuja kutajwa kwenye kanuni, na Mwenyezi Mungu akitujaalia *in shaa Allah* tutafikia *standard* hizo za wenzetu waliokuwa nazo. Mimi nina moyo mkubwa sana kwamba tutafikia *standard* hizo, hapa tulipo sipo tulipokuwepo jana, na *in shaa Allah* kesho sio kama tulivyo leo.

Kifungu cha (m), kusimamia na kukuza viwango na ubora wa utoaji wa huduma za hospitali, kwa kuzingatia ustawi wa matarajio ya wagonjwa na kukuza miko na maadili ya kila kada ya afya. hiki kimeshajieleza, kimejieleza kwa upana wake, tunaomba tukubaliwe kukiacha hapo, pamoja na kuanzisha kamati ambazo zinaonekana ni muhimu katika kukamilisha majukumu.

Mhe. Spika, kuna Waheshimiwa Wajumbe, waliomba kwamba pawe na kamati nyengine. Lakini kifungu hiki kinaweza moja kwa moja, kinaipa fursa ya nguvu bodi kuanzisha kamati ambazo wao bodi wataona ziko muhimu moja kwa moja katika kutekeleza majukumu yake wala hawatozuiliwa. Maposho hapa yameshaelezwa tayari, wakipendekeza naamini yatakubaliwa hayana tatizo.

Mhe. Spika, naomba niende kwenye Sehemu ya Nne, kifungu cha 15(c), hapa tulirekebisha kwenye kamati, lakini marekebisho yale sikuyaona kwenye karatasi ya kamati. Naomba turekebishe tena, tulirekebisha kwenye kamati na tulikubaliana, lakini kwenye karatasi ya kamati marekebisho hayo sikuyaona.

Kifungu cha 15(1)(c), mwenye uzoefu usiopungua angalau miaka 10, huyu Mkurugenzi wetu Mkuu Mtendaji tunataka awe ni *experience man*.

Siku hizi, Mhe. Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wajumbe, katika digrii hizi za afya mtoto anaweza kuingia miaka 18 akasoma *first degree* pale miaka mitano, miaka 23 akishamaliza anafanya na *masters* yake miaka miwili anafika miaka 25, tayari ana *masters* huyo.

Sasa miaka 25 ukimpa miaka mitatu ukamleta kuwa Mkurugenzi Mkuu wa kitu kama kile cha Mnazi Mmoja anakuwa miaka 28 atakuwa bado ni mdogo. Atakapomaliza miaka 23 akapata pale na kidogo *course* zake, 25 tukimuongezea na 10 akawa 35, angalau anakaribia ile miaka ya uongozi ya 40 aliyopewa Mtume Muhammad (*SAW*). Kwa hivyo, tunataka hapa kifungu hiki isipunguwe angalau miaka 10. Hili tulikubaliana na kamati nakumbuka vizuri sana.

Mhe. Spika, kifungu cha 16(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na majukumu yafuatayo. Hapa (a) ni kuongoza mambo ya hospitali na kutoa huduma bora na zinazojitosheleza. Mhe. Rashid Makame Shamsi alichangia hapa katika *vocabulary* ya Kiswahili. Nataka kusema hivi, na mimi niliwauliza wataalamu walionishinda, waliobobea kwenye lugha. Anasema;

(a) Iwe kuongoza mambo ya hospitali na kutoa huduma bora, hizo huduma zinazojitosheleza, hizo huduma zenyewe zinazojitosheleza. Kuna mmoja kaandika zinazojitosheleza zenyewe. Lakini hili hatuwezi kuweka hapa kwa sababu hii ni sheria, lakini hizi huduma ndio zimekusudiwa zinazojitosheleza.

(b) Alisema, kusimamia mapato, matumizi yanayotolewa na hospitali kwa mujibu wa sheria zinazohusika. Hili liko sawa kwa upande wetu, niliona katika karatasi hii ya kamati, sikuona marekebisho yoyote hapo katika kifungu cha 16 sikuona. Kwa hivyo, hili tunaomba libakie hapa hapa.

Mhe. Spika, sasa tunakuja kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Natumai yumo na kama hayumo, basi popote pale alipo habari hizi atazipata. Kifungu cha 17(1), mimi naelewa kabisa nia ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni kama vile kwa Mhe. Hamza Hassan, yuko katika kutetea maslahi yapatikane zaidi na kuwepo na sehemu za wananchi pia kutoa maoni yao, kuwepo na sehemu za wananchi kutoa malalamiko yao, kuwepo na sehemu za wananchi ambazo yale malalamiko yakishafika yatafanyiwa kazi. Yote hayo tunayakubali na katika sekta ya afya kimataifa sasa hivi *customer care* inatakiwa iwepo. Sio sekta ya

afya tu katika kila sekta. Ukimpeleka mwanao shule, baadhi ya shule zinakuwa na *customer care*, shule zetu za serikali zina *customer care*, maana pale mwananchi anakuwa *customer care* maana yake ndio mteja anampeleka mwanawe, kwa mantiki hiyo anaitwa mteja.

Mhe. Spika, naomba nikubaliane naye kwamba kitengo cha *customer care* kitakuwa katika kifungu cha 17(1)(a), hii itaitwa Idara ya Huduma na Matibabu, naomba turekebishe hapo, Idara ya Huduma na Matibabu ama Tiba, lolote litakaloamuliwa. Maana wataalamu wamenipa maneno mawili, wamenipa neno matibabu na neno tiba yote yako sawa sawa hayo.

Kwa hivyo, hii itakuwa ni Idara ya Huduma na Matibabu, sasa zile huduma ndio zita-*cover* ile *customer care* aliyozungumza Mhe. Jaku Hashim kwamba popote atakapofika mgonjwa, akataka kuwasilisha malalamiko yake, kutakuwa na hii idara ambayo itakuwa na mtu maalum wa kupokea hayo malalamiko.

Mhe. Spika, hivi sasa tayari Mnazi Mmoja kipo kitengo hiki cha kupokea malalamiko na kinaitwa ni Kitengo cha *Public Relations (PR*), yaani mahusiano ya kijamii ndio kinachohusika na kupokea malalamiko.

Mhe. Spika, idara nyengine tunaendelea kama kawaida katika tafsiri ya Kiingereza imetolewa na iko wazi kabisa, *Department of Clinical Services*. Ni idara hii ya 17(1) kama ilivyotolewa kwenye karatasi hii ya kamati, 17(d) ambayo inasema kisomeke Idara ya Dawa na Vifaa Tiba. Tulishakubaliana nalo kwenye kamati, naona wajumbe wengine wengi walichangia bila ya kusoma kwenye karatasi hii ya kutoka kwenye kamati. Naomba wale wajumbe wote wanikubalie, wale waliosoma bila ya kusoma hii karatasi kwamba hilo tulishakubaliana nalo na Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kisomeke Idara ya Dawa na Vifaa Tiba, na hii ya Kifungu (e) kisomeke Idara ya Ufundi, kwa sababu hii ilikuwa ni tafsiri moja kwa moja kutoka Kiingereza, hii itakuwa ni Idara ya Ufundi katika kifungu (e).

Mhe. Spika, hapo hapo chini Mhe. Mihayo Juma naye alichangia pamoja na Mhe. Mohammed Said Dimwa katika kifungu (f), naomba tukubaliane naye Mhe. Dimwa kwa hoja yake nzito, kwamba Idara ya Huduma za Uchunguzi wa Afya na Maradhi. Hii kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wajumbe, ilikuwa ni idara yake yeye mwenyewe Mhe. Dimwa aliwahi kufanyakazi katika idara hiyo. Kwa hivyo, hapo kwa upeo wake mpana na ujuzi wake naomba tukubaliane naye tuongeze neno, "na maradhi". Mhe. Mohammed Said Dimwa umeweka historia hapo, kifungu (f) ndani ya Mnazi Mmoja, *story* ya miaka mia

hiyo. Idara ya Huduma za Uchunguzi wa Afya na Maradhi iwepo. Tunashukuru sana kwa mchango huo.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba nimkubalie Mhe. Rashid Makame Shamsi katika kifungu cha 18(3), Mkurugenzi aliyeteuliwa chini ya masharti. Naona walisahau kwenye karatasi ya kamati, lakini neno "masharti" lipo hapo na tunakubaliana nalo kabisa.

Mhe. Spika, kifungu cha 19(2) kwenye karatasi hii tena narudia ya kamati huyu mlezi wa hospitali jamani alishatajwa kuwa huyu ndiye Muuguzi Mkuu, yaani *matron*, yule *matron* wa hospitali ndiye anakuwepo katika kamati hii ya uongozi, *matron* wa hospitali na alishatajwa hapa katika karatasi hii ya kamati. Kwa hivyo, Muuguzi Mkuu ndiye atakuwa wa hospitali.

Mhe. Spika, narudia nyuma kidogo tena hapa katika Kamati ya Uongozi, nataka kutoa tafsiri kabisa ya Wakurugenzi hawa wa ndani ya hospitali, hawa kwa sababu ndani ya hospitali kunakuwa na *structure* yake, hawa ni Wakurugenzi wa mule ndani ya hospitali, sio wale wanaoteuliwa na Rais, sio wale wanaoingia katika ile sheria nyengine, hata maslahi yao na marupurupu yao yanakuwa *within conformity* ya Mnazi Mmoja *Act*, yaani *Act* hii.

Mkurugenzi Mtendaji yeye ndiye atakayeingia katika *category* ile ya Wakurugenzi, hawa wote wanakuwa chini yake, na hii inafanyika sehemu mbali mbali katika *Good Governance*, katika *Cooperate Governance* hili linafanyika bila ya wasi wasi.

Kwa hivyo, naomba sana Wakurugenzi hawa watakuwa ni wa idara. Baada ya majadiliano marefu tumeona tukiwaita ni Wakuu wa Vitengo tutakuwa tunawadogosha, kwa sababu huko tunakotaka kuelekea, hilo la kwanza. La pili, sheria hii ya Afrika ya Mashariki inatutaka sisi lazima tuipandishe hadhi hospitali ambayo itakuwa inatoa mafunzo, ili zile digrii zetu ziwe zinatambulikana katika Jumuiya nzima ya Afrika ya Mashariki. Kwa hivyo, naomba sana tafsiri ya Wakurugenzi hapo wasiwe Wakuu wa Vitengo hawa. Ni Wakurugenzi wa hizi Idara ambazo ziko ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, tofauti na wale Wakurugenzi ambao wametajwa katika sheria nyengine, ambao ni wateuliwa wa Mhe. Rais mwenyewe.

Kifungu (b) kimekusudiwa Wakurugenzi wa Idara zote zilizotajwa hapa na zile zitakazoundwa baadae, kwa sababu bodi itakuwa ina mamlaka, baada ya kushauriana na waziri, basi bodi itakuwa na mamlaka ya kuunda idara mpya. Sasa hivi Hospitali ya Mnazi Mmoja, naomba hili nilisome Mhe. Spika. Sasa

hivi Mnazi Mmoja hatuna idara *perse* ndani mule, lakini tuna vitengo vifuatavyo.

Mhe. Spika, sasa hivi Mnazi Mmoja tuna vitengo 9, navyo ni;

1) Kitengo cha Huduma za Wagonjwa wa Nje, yaani *out patient.*
2) Kitengo cha Huduma za Upasuaji, *Surgery.*
3) Kitengo cha Maradhi ya Kinamama *Obstrectric Gynaecology*.
4) Kitengo cha Mazoezi ya Viungo Utengenezaji wa Viungo Bandia, *Physiotherapy and Rehabilitation*.
5) Kitengo cha Maradhi ya Watoto, *Paediatrics.*
6) Kitengo cha Maradhi ya Ndani, *Internal Medicine.*
7) Kitengo cha Vipimo na Uchunguzi, *Diagnostics Services*.
8) Kitengo cha Huduma za Afya ya Akili. Huduma za Afya ya Akili pia imezungumziwa.Kule Bati Jekungu kama alivyotamka Mhe. Mjumbe, ama Mwembeladu ni Kitengo kimojawapo cha Mnazi Mmoja, nilieleza jana. Kwa hivyo, *Phychiatric and Mental Health* inaingia pale, sio hospitali inayojitegemea ile.
9) Kitengo cha Matibabu ya Meno na Afya ya Kinywa, *Dentistry*.

Sasa Mkurugenzi Mkuu anapoona kuna haja, kumekuja kitengo kipya mfano cha *Neuro*, jengo jipya, *service* mpya, *facilities* mpya, kitengo kinajitosheleza, wataweza baada ya kuwasilishwa kwenye bodi na bodi kushauriana na waziri, basi wataweza kuunda vitengo vipya wakati wowote, hilo halina tatizo.

Naomba hilo likubalike kwamba tuyape mabodi nguvu ya kuamua *structure* yake ya ndani iweze kuamua yenyewe, kuelekea huko tunakotaka kwenda, ambapo Mhe. Hamza Hassan alisema tunaogopa. Lakini hatuogopi, ila tunataka kwenda hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, kifungu chengine ni cha 21(1), hospitali inaweza kwa mujibu wa masharti na vigezo, kuajiri au kuteuwa mfanyakazi au huduma ya Mshauri Elekezi au Mtaalamu, kama itakavyoonekana inafaaa kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya hospitali. Hapa wamepewa hawa uhuru wa kufanya hivyo, kwa hivyo wanaweza kuingia katika mikataba yao namshauri elekezi.

Pili uajiri wa wafanyakazi wa Hospitali wataalam na waidizi utafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kama nilivyosema hapo awali Sheria mama Namba 2 ya mwaka 2011 na kanuni zake, lakini mle ndani ya hospitali kuna taratibu nyengine ambazo bodi inaweza kuamua katika vile vifungu vya bodi kuwawekea mambo yao, wapo wafanyakazi wengi ambao wako chini ya

sheria ya umma lakini wanafanya katika miradi mbali mbali, ambayo ina mambo mbali mbali na faida mbali mbali, ambayo inahusiana na masuala haya.

Tatu mfanyakazi anayefanya kazi hospitali kabla ya kuanza kutumika ka sheria hii ataendelea kufanya kazi na itachukuliwa kuwa ni mfanyakazi wa hospitali aliyeajiriwa chini ya masharti ya sheria hii, kwa hivyo wale wote ambao wanafanya kazi hivi sasa hospitalini moja kwa moja watakuwa *transfer* katika ile *inclement act* yao kuwa wafanyakazi chini ya sheria hii.

Kwa hivyo naomba niseme kwamba haya yanakava masuala yote ambayo waheshimiwa walichangaia katika eneo hili la kuweza kupata nguvu zao wenyewe Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya Fedha sasa sehemu ya tano masharti ya fedha za hospitali, naomba kwanza nikisome kifungu chote cha 22 a, b na c ili tufahamiane vizuri sana na Waheshimiwa Wajumbe, na nitajaribu kutoa ufafanuzi wakati nasoma.

Kutakuwa na fedha za hospitali ambazo zitajumuisha yafuatayo:

Kwanza kabisa *this is half way* kuelekea huko kwenyewe mwisho, fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku, hizi fedha ambazo Baraza la Wawakilishi litapitisha zitakwenda moja kwa moja Mnazi Mmoja kwa njia ya ruzuku chini ya sheria hii.

Pili michango ada, michango yenyewe ndio hii kama *NHIF*, kuna *Jubilee Insurance* Mnazi Mmoja haina mkataba mmoja tu na *Insurance Provider* mmoja ama anayetoa bima mmoja; wapo wengi siku hizi, na ni biashara ya ushindani na wao wanapofungua mikataba pale na wao wanachangia juzi kuna mjumbe alichangia wakati wa Hotuba ya Wizara ya Afya kwamba kwa nini Al-Rahma inapata pesa zaidi kuliko Mnazi Mmoja sikumbuki mjumbe gani, lakini alichangia hapa. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa sheria hii itawawezesha sasa wale wataalamu wetu bingwa, kuna wataalam 21 pia nalijibu hilo sasa hivi wa taaluma mbali mbali na tunaendelea kuongeza watatu wako masomoni, wale watawaza kutoa taaluma ambazo hazipo kule Al-Rahma, hazipo Global, haziko kwengineko zitaweza kutolewa pale na zitatolewa kwa kadi ya yule mhusika akija na kadi ya *NHIF* atapewa. Akija na kadi ya *Jubilee Insurance* atapewa, akija na kadi ya *ZIC* atapewa na mwengine yeyote.

Kwa hivyo pale kutakuwa na malipo ambayo yanaingia moja kwa moja kwa sababu mwisho wa siku Mnazi Mmoja ita-*generate bill* kumpelekea yule

Insurance ama Helth Insurance Provider. Lakini ya pili kuna ada Wajumbe watakuwa wameuliza hapa ada hizi zitakuwa zinatoka wapi, kuna wanafunzi pale wanakuja kusoma kutoka Vyuo Vikuu mbali mbali ulimwenguni hivi sasa ninapozungumza tuna wanafunzi zaidi ya 20 wanaotoka Vyuo vikuu mbali mbali. Mimi mwenyewe juzi nimesaini baadhi ya maombi yao kupeleka kwa Mhe. Waziri wa kazi kuwaombea muda wa kukaa hapa nchini wa kuweza kujifunza. Malipo yale wale wanaochangia kupitia malipo, kuna malipo ya mikopo kuna mjumbe aliuliza je, mtaweza kwenda kukopa ndio hapo.

Mhe. Jaku Hashim naomba kukujibu wataweza kwenda kukopa hapa malipo na mikopo wataweza kwenda *PBZ* hawa, wataweza kwenda *Exim* yoyote atakayowapatia ile rate ndogo zaidi wataweza kwenda kuchukua mikopo, bodi itakaa na Mkurugenzi mtendaji wataamua wao wenyewe kwenda kuchukua mikopo ambayo hospitali inaweza kupokea mara kwa mara kutoka kwa mtu ama taasisi yoyote, kwa hivyo kifungu hiki naomba kisomeke vizuri kinakava hayo.

Mhe. Spika, wale wafanyabiashara wawili Mungu atakaowajalia watakaoteuliwa kwenye bodi hii baada ya sheria hii kupitishwa na Baraza wao, pia watakuwa na fursa ya kuchangia zaka zao. Mhe. Simai alisema hapa wanatoa zaka kubwa kubwa mwengine anatoa zaka bilioni mbili, bilioni tatu bilioni nne, bilioni tano bajeti nzima ya Mnazi Mmoja ni bilioni nane, pengine ni nusu ya zaka ya mfanya biashara yule ataombwa kwa hivyo kifungu hichi kitamruhusu pia Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Mnazi Mmoja chini ya Sherehe kupokea fedha kama hizi.

Kifungu C fedha nyenginezo ambazo zitawekwa au kupatikana katika utekelezaji wa kazi au vyenginevyo, hapa Mhe. Jaku na Mhe. Hamza naomba niwaeleze kwamba kifungu hichi kinampa uhuru zaidi Mkurugenzi mtendaji pamoja na bodi fedha nyenginezo haijasema kutoka wapi *other sources* na naomba hapa ya kiingereza pia imeandikwa vizuri sana naomba niisome kidogo ya kiingereza, natumai waheshimiwa wamepewa wote sheria ya kiingereza.

Kifungu 22(c) *any other monies that may vest or accrue whether in the course of its operation or otherwise*, kwa njia yoyote ile nyengine kwa hivyo na kifungu hiki kwa kiswahili, kwa kazi au vyenginevyo vyovyote. Kwa hivyo naomba hili ndugu Wajumbe walipokee kama ufafanuzi wa yale yaliyoulizwa kwenye masuala ya fedha.

Naomba niingie kwenye sehemu ya sita kwenye masharti mbali mbali na naomba kwanza kabisa niingie katika neno hili kinga la kwanza kabisa, hili tumejadiliana sana na namshukuru Mhe. Mwenasheria Mkuu ametuelimisha pia kisheria sana namshukuru sana.

Kifungu cha 25 Mjumbe wa Bodi mfanyakazi au mtu mwengine yeyote ambae anatoa huduma hospitali hatoweza kuwajibishwa binafsi kwa kitendo jambo au chochote alichokifanya au kuacha kufanya ikiwa alikifanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu yake chini ya sheria hii. Daktari katika viapo vyake hili naomba niseme katika ufafanuzi vizuri lieleweke, daktari katika viapo vyake anapokuwa *theater* ndani keshakufungua kila kitu humu ndani keshaona kila kitu pale ni maamuzi baina yake yeye na Mwenyezi Mungu wake. Madaktari; Dkt. Jidawi yupo hapa atatusaidia hili baadae tukiwa nje ya eneo hili atatusaidia, kwamba madaktari wanapopasua wakati mwengine wanakwenda kukuta vitu wakati mwengine vitu vishaharibika vyote au vitu vya kiajabu ajabu huko ndani.

Sasa pale maamuzi yale ni baina ya daktari na Mwenyezi Mungu wake daktari anaamua huyu mgonjwa sasa tumbadilishe kiungo; tumtoe hiki kiungo tumkate kiungo yuko kati kati ya *theater* kuna maamuzi anafanya daktari tofauti na nje tofauti na vipimo, tofauti na picha zote anafanya kati kati ya meza ya *theater* yupo pale anapotoka jasho anafanya.

Sasa hapa tunataka yule daktari kumkava ili kusiweko na yale mambo ya kushitakiwa aa daktari huyu kafanya hivi, kwa sababu maamuzi yale aliyofanya ndani, kwa sababu daktari anakula kiapo sio *profession* zote wanaokula viapo, lakini daktari anakula kiapo na nesi pia muuguzi aanakula kiapo na sisi sote tuliokuwepo humu tunaotumikia wananchi tunakula kiapo. Mawaziri wote wanakula viapo pale ikulu mbele ya Rais mwenyewe.

Kwa hivyo, kwa kuwa huyu daktari tunamuamini ameshakula kiapo hiki na ule uamuzi wake tunauamini ni mwisho anaofanya pale ndani rufaa yake peke yake ni kupitia bodi ya madaktari ambayo inabidi uwasilishe ushahidi wote, sasa ushahidi wa *theater* anakuwa nao yeye mwenyewe daktari.

Kwanza sisi binaadamu, mie nashukuru Dkt. Jidawi ameshanifanyia upereshen mie mara mbili operesheni kubwa kujisalimisha mimi kwa Dkt. Jidawi akanifanyia upereshen tayari nimeshamkabidhi roho yangu pale kweli si kweli jamani, kwa sababu kwanza yeye ananitoa fahamu unakuwa huna fahamu kabisa na katika kutolewa fahamu viungo vinaweza kufeli vikarudi tena katika kupata fahamu, vinaweza kureli viungo inawezekana kutokea kwa hivyo

kifungu hichi kinamlinda yule daktari anapofanya maamuzi pale anapokuwa ndani juu ya mgonjwa. Kinamlinda pia muuguzi, inamlinda nesi, kinamlinda kila anayefanya kazi hospitali ndio maana kimetamka kwa nia njema neno nia njema lipo hapo, *otherwise* tutakuja kuwashitaki hawa watu kila siku tutabakia hatuna daktari hata mmoja mimi na ndugu yangu Abdalla Ali Kombo tukianguka hatuna pa kwenda, kwa hivyo naomba sana hili tuliweke wazi kabisa.

Kifungu cha 27 huduma bila ya malipo kimechangiwa na wajumbe wengi sana na Mhe. Hamza, Mhe. Jaku walikuwa kidogo wakali hapa naomba niseme hivi kifungu hiki, nawaomba sana wajumbe sera ya Mapinduzi ya mwaka 1964 bado haijafutwa iko hai mpaka leo, wakati ule ilitamkwa matibabu bure, elimu bure kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa sauti yote hiyo. Sasa ile sera haijafutwa sera ile imekuja kurithiwa rasmi na *Afro Shirazi Party* ikatolewa tamko mwaka 1967 toleo jengine likatolewa tena, lakini sera ile ile imekuja kurithiwa na Chama cha Mapinduzi CCM ambayo sasa hivi sisi tunatekeleza ilani yake.

Kwa hivyo sera ya kutoa matibabu bila ya maliopo kwa wananchi ipo pale pale, pale tunapokuwa hatuna hatumlipishi mwananchi, tunamuomba mwananchi tafadhali dawa hizi hatuna tunaomba uende ukanunue nje, mtu akichukua pesa ndani ya hospitali akapokea pesa amefanya kosa, mtatushambulia siku zote, anakwenda kununua mpira mwenyewe, anakwenda kununua *gloves* mwenyewe anakwenda kununua jiki mwenyewe pale tunakuwa tumeishiwa.

Hatumruhusu *nurse* wetu ndani ya hospitali kufanya biashara ya kuuza jiki mle si kazi yake, si kazi yake kuuza mipira mle ndani, si kazi yake kuuza golve mle ndani kama anazo anatoa hana anamwambia mama yangu naomba unisamehe leo, au baba umemleta mama hapa tunaomba ukachukue *gloves* pale nje wala si mbali.

Hilo tutalifanya, lazima tukubali, ukweli usemwe lakini halipishwi mtu pesa panapokuwa mtu analipishwa pesa mtwambie anakuwa kafanya kosa kutokana na sera ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

Sasa kifungu cha 27 kinalinda ile sera ya Mapinduzi kinasema hivi kifungu cha 27(i)

"Hospitali itaendelea kutoa huduma ya afya kwa wagonjwa bila ya malipo kwa kufuata sera na miongozo ya Wizara". Hapa imeandikwa Wizara lakini sera iliyokusudiwa hasa ni sera ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 ambayo

wana CCM wote wanaisimamia sera hiyo kwa viapo vyao vyote. Nitashangaa sana mjumbe yeyote akipingana na sera hiyo ya Mapinduzi, nitashangaa sana.

Lakini wakati huo huo kifungu cha 27(2) tumeweka hiki makusudi kwamba bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha kwanza yaani masharti ya kifungu hicho cha Sera ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar Mkugunzi mtendaji anaweza baada ya kushauriana tusikilizane kwa makini hapo, baada ya kushauriana na kukubaliana na Waziri kuweka utaratibu wa mgonjwa kuchangia kwa baadhi ya huduma za afya zinazotolewa na hospitali, naomba nifafanue baadhi ya hizo huduma.

Tukisema tunaweka 27(1) tu peke yake tutashindwa kumchukua *NHIF*, *ZHIF* itakayoundwa *Zanzibar Health Insurance Fund* itaundwa itakuja hapa tutashindwa kuchukua pesa zake, tutashinda kuchukua pesa za *Jubelee*, tutashinda kuchukua pesa za *Zanzibar Insurance* tutashindwa. Kifungu hiki kitamuwezesha yule kuchukua pesa zile. Pili kutakuwa na ma- *research* makubwa makubwa yanafanyika tafiti imeshatajwa kwenye kifungu kile cha awali, watakuja wanafunzi wa *University* mbali mbali kuja kufanya tafiti hapa, kwa sababu hapa watapata *Practical ya Tropical Disease* kule kwao hawapati *Tropical Disease* hawapati kufanya *Practical*. Tutaweza kujiwekea viwango vya kulipwa pesa nyingi kwa ajili ya wanafunzi kupata *Tropical Disease* mafunzo hapa pesa zile zitaingia kupitia kwa Mkurugenzi huyu.

Pia tutaweka kanuni ya Fedha zile ambazo zitatolewa kwa huduma nyenginezo kama *fast struck* ambayo tumeianzisha sisi wenyewe Mapinduzi kongwe, fast struck ni kama *Private Hotel Service* katika Hospitali hata ukienda India unakuta mara nyingi matibabu tofauti, vipimo tofauti na kulala tofauti bili tatu unapata tofauti. India mara nyingi na Apolo wanayo *system* hiyo Apolo bili yake ya *Diagnostic* inaandikwa kabisa *Diagnostic* na karatasi zake zinakuwa na rangi tofauti, bili yake ya daktari inaandikwa inakuwa mbali, lakini bili ya hoteli na *service* wanaita hasa *hotel service* ndio ile ya chumba kulala ndani wewe unahisi umelela hospitali lakini kuna kampuni maalum ambayo inafanya *Caterings* mule ndani inatandika mashuka, inafanya usafi, inafanya *house keeping* kama vile ilivyokuwa hotel.

Sasa pale kwa Mapinduzi kongewe sisi ndio kwanza tumeanza kuyaanzisha *First Track Service* tumeanzisha tunapima hatukuwa na *instrument* kama hii, sasa *Instrument* hii itasaidia kuimarisha huduma ya *First Truck Services* unataka kwenda kwenye *First Truck* unasema mimi nataka *Hotel Service* unafanyia upereshen kule kule kwenye *theater* ile ile ambayo kila mkwezi na mkulima anafanyiwa kwenye *theater* ile ile, lakini unasema aa mimi nataka

kulala kwenye kitanda ambacho kina TV utalipa, mie nataka kulala kwenye kitanda killichokuwa juu kwa juu utalipa ndio hii. Sasa sheria hii itasaidia pia kuweka sawa yale masuala yote ya *First Truck Service* ambayo yatakuwa bila ya matatizo.

Naomba Mhe. Spika, kwa kuwa nimetoa michango yote kwa jumla naomba nisiende kwa mjumbe mmoja mmoja, kwa sababu michango ni mingi na naomba sana wajumbe wanikubalie kuwa michango yao hii yote tunaichukua, tunaipokea sheria ikishaundwa sheria mkishaipitisha nyie kwanza Mhe. Rais akishaitia saini bodi ikishaundwa haya ndio miongoni mwa mambo ambayo sie tutawapa wao bodi ebwana haya ndio matatizo ya wakulima na wakwezi wetu yanayotoka kwa wawakilishi wa wananchi. (*Makofi*)

Tunaomba sana muyachukue muyapokee mukayafanyie kazi, kwa hivyo naomba sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, wanikubalie kwamba hii michango yao yote ya maandishi nisianze kuitolea maelezo moja moja kwa sababu michango hii yote itachukuliwa na hiyo bodi itakayokuja, na *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu atajaalia itakuwa bodi nzuri na mahiri, na *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu atajaalia hii sheria itapita vizuri mara moja ili bodi hiyo ianze kufanya kazi mara moja, kwa sababu tuna *dateline* ya Afrika ya Mashariki tusisahau ile hati ya dharura ya Mhe. Rais. Naomba sana wajumbe wanikubalie kwamba tulichukue hili na sote kwa pamoja tulifanyie kazi. Michango ya mmoja mmoja ninayo ya kutosha ziko *page* kadhaa hapa zaidi ya *page* 50 nimeandika yote hayo yatakwenda kufanyiwa kazi na itakuwa raha zaidi kwa sababu bodi wakati naingia tayari imeshapata ya kuanzia kufanyia kazi.

Mhe. Spika, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu...

Mhe. Spika: Hapana Mhe. Waziri toa hoja tu.

Mhe. Waziri wa Afya: Samahani Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante ungerudi kidogo Mheshimiwa ahsante sana. (*Makofi*) Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Mheshimiwa sasa mimi nitawahoji wale wote wanaounga mkono hoja ya Mheshimiwa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe Mhe. Waziri ametumia saa moja kasoro kama dakika mbili ambayo ni nzuri tu, na nimekubaliana nae kwamba asianze tena kumjibu mtu mmoja mmoja amefanya vizuri, lakini pamoja na kuokoa kwake wakati tunazo shughuli nyengine ndogo ndogo ambazo zitafuata baada ya kufuata shughuli yake.

Sasa tutakwenda kwa ajili ya kupitisha vifungu kabla ya hapo ili tuweze kuwa *comfortable* nitamuomba sasa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili kama ana chochote kwa ajili yangu tafadhali Mheshimiwa.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli zilizo mbele yetu bado kumalizika na kwa kuwa muda uliopo ni mdogo na kwa kuwa Mhe. Waziri wa afya anahitaji muda wa kumalizia hoja yake, na kwa kuwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atakuwa na hotuba ya kuahirisha Baraza letu. Hivyo naliomba Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Mheshimiwa sasa mimi nitawahoji wale wote wanaounga mkono hoja ya Mheshimiwa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu niliouwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu kifungu baada ya kifungu.

Naomba kutoa taarifa.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Hospitali ya Mnazimmoja na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa kufanya kazi ya kutoa ufafanuzi ingawa anasema hakutujibu mtu mmoja mmoja, lakini ametujibu kupitia katika yale maeneo kwa kweli tumeridhika sana. Sasa kuna kifungu cha 1 kuhusu Jina la Sheria. Sisi tuliomba na kwanza ninaishukuru sana Kamati ambayo iliyopitia mswada huu Kamati ya Baraza, moja katika mapendekezo yao walipendekeza kwamba kuongezwa neno 'taifa' baada ya maneno 'Mnazimmoja'.

Mhe.Waziri, kajitahidi sana kutushawishi kwamba tuendelee kukubali kwamba iitwe Sheria ya Hospitali ya Mnazimmoja. Mimi nilipendekeza kwamba iitwe Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Rufaa, lakini sasa neno rufaa kwa kuwa alilitolea ufafanuzi mzuri nimeridhika. Lakini bado nilikuwa naendelea kurudi katika mapendekezo ya Kamati neno 'taifa' likubaliwe na hoja yangu hii, kwamba hospitali hii sio kama itakuwa majukumu yake kwa hospitali yenyewe tu ya Mnazimmoja. Lakini huku mbele kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 4 kwamba:

> a) Kutoa huduma kama hospitali ya rufaa na kuweka Utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya; na
> b) Kutekeleza majukumu ya udhibiti na usimamizi wa hospitali nyengine yoyote.

Kwa hivyo, ina maana hospitali ya Mnazimmoja hii sheria tunayoipitisha pia itakuwa *regulator* kwa mpaka na hospitali nyengine binafsi ambazo baadhi yao sisi hapa wajumbe huwa tunazilalamikia kwamba zinatoa huduma chini ya kiwango. Lakini vile vile kuna taasisi mbali mbali za kimataifa na yeye mwenyewe alisema, kuna watu hapa wanatafuta *PhD* hapa hapa. Sasa neno 'taifa' bado mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako bado lina nafasi yake kwa sababu mpaka wenzetu kutoka Tanzania Bara, kutoka nje ya

Zanzibar watakuwa na uwezo wa kuja kuitumia Hospitali ya Mnazimmoja kwa mafunzo na shughuli nyengine zozote.

Sasa mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, wala Mhe. Waziri, asiogope sana hili neno 'taifa' lakini ndio bado tunaitangaza hospitali yetu kwamba mpaka watu kutoka nje watakuwa na nafasi ya kuja kupata mafunzo na huduma nyengine katika hospitali yetu. Kwa hivyo, ninamuomba tu Mhe. Waziri, kwa kuwa kamati yake imepitia na mimi vile vile, naomba aikubalie kamati pamoja na hayo mawazo yangu mimi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mhe. Hamza, kwa maoni yake hayo. Naomba niseme hivi; katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi Binguni imetamkwa ndio *the referral hospital...*

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mheshimiwa, watendaji wako wanaruhusiwa kushuka chini kama kukitokezea chochote wanaweza wakakusaidia.

Mhe. Waziri wa Afya: Bora washuke maana wengine wana nia ya kugombea. Mhe. Mwenyekiti, ile imetajwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama *referral* hiyo Binguni. Hofu yetu rufaa keshanikubalia Mhe. Hamza, tukitia hii kama ya taifa na hii ni ya hospitali ya Mnazimmoja, sasa hospitali ya Mnazimmoja itakapojengwa Binguni ikamalizika huo Mnazimmoja itabidi turudi tena kuja ku-*modify*, hilo la kwanza.

Lakini la pili hii bado haikuwa ya kitaifa, yaani sio taifa, taifa, ndio hospitali yetu kuu kwa hapa Zanzibar, lakini tukichukua ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko Hospitali ya Taifa, kwa hivyo, naomba hilo liwe la pili.

Lakini la tatu katika kifungu hicho hicho cha 4(b) yeye amesoma Mhe. Hamza, "kutekeleza majukumu ya udhibiti na usimamizi wa hospitali nyengine yoyote kama ilivyopewa chini ya sheria hii au sheria nyengine yoyote, hapa tumeweka ni kama *future provision*. Kwa sasa hivi Mnazimmoja ina watoto wawili; Muembeladu na Kidongochekundu na ndio maana tunataka hayo yaingie humu moja kwa moja. Lakini hii imewekewa kama *future provision,* kwa hivyo, naomba sana atukubalie na Kamati pia tulilizungumza sana hili, tukichukuwa ya taifa sasa hivi tunaweza tukabeba mzigo, hiki ni kipindi cha mpito baadae tunaweza kuja kurekebisha patakapokuwa pamekaa sawa. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri Mhe. Waziri, amejitahidi sana kutoa ufafanuzi na kwa kuwa amesema kwamba labda basi

kwa sasa hivi kwanza wacha tuanze na hii, halafu huko baadae twende na hiyo ya taifa. Kwa hivyo, hili nitamkubalia lakini naomba vile vile, Mhe. Waziri, isiwe kila walichokileta ndio kiwe hicho hicho, basi na sisi pia kuna mambo mengine huko mbele zaidi tunakokwenda na yeye pia aje akubali kutukubalia vile vile. Ahsante.

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Kuanzishwa na Kazi za Hospitali

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa Hospitali

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, tuweke tu *Hansard* sawa kwa sababu baada ya majadiliano baina ya Mhe. Waziri na Mhe. Hamza, neno la 'taifa' linaondoka, sasa nadhani ni vyema lisomeke hivyo, kwa sababu ukisoma kifungu cha tatu kinazungumza Hospitali ya Taifa ya Mnazimmoja, sasa ni vyema tuweke *Hansard* sawa kama neno hili linafutika ili liwe hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake kinakubaliwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, itakuwa sio cha 3 tu hata kwenye ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani angefanya Mhe. Waziri, kila sehemu ambayo imejitokeza hivyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba meza yako kila kwenye neno 'taifa' linaambatana na hospitali liondoshwe.

Kifungu 4 Kazi za hospitali

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nataka tuende kwenye kifungu (n), nilipendekeza mwanzo sentensi ilikuwa ikisomeka;

"Kusimamia na kudhibiti, kuibuka kwa maradhi ya mripuko kwa umuhimu wa afya ya jamii"

Nikapendekeza, sikumsikia Mhe. Waziri, vizuri aliponijibu, "kusimamia na kudhibiti kinga ya maradhi kwa umuhimu wa afya kwa jamii". Kwa nini nikapendekeza hivyo, kwa sababu nilipendekeza hivyo, hospitali si kazi yake ku-*deal* sana na kwenye kukinga, kazi yake sana kwenda kutibu nilipendekeza hivyo, naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Kama nilimsikia alikubaliana na pendekezo lako, sijui lakini, hebu nikusikie Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Dimwa, nilipokuwa natoa maelezo nilikubaliana na pendekezo lake kwamba, tuifanye kama vile alivyosema, "kusimamia na kudhibiti kinga ya kuibuka kwa maradhi ya mirupuko na kwa umuhimu wa afya kwa jamii". Lakini hapa Mheshimiwa, turekebisho kidogo tu, "kusimamia na kudhibiti kinga na tiba", kwa sababu maradhi mengine ya miripuko pia yanatibiwa pale na miongozo itatolewa. Ila nataka kuweka kidogo maelezo kwamba huku nje sisi tunavyotafsiri kwamba kinga ikishafeli ndio mtu huingia Mnazimmoja anaingia kwenye tiba. Lakini sasa hivi kwa sababu kuna *laboratory services* na kadhalika na yeye Mhe. Dimwa, ni mtaalam wa maeneo hayo, ndio hayo yanafanyika pale, kwa hivyo, naomba nikubaliane nae.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri, tuendelee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kidogo nipate ufafanuzi wa kifungu cha (c) kinasema;

"Kuwahudumia wagonjwa wa nje na wa ndani kwa mujibu wa maadili ya kidaktari".

Sasa nilikuwa nataka ufafanuzo kidogo hapa kwamba wagonjwa wa nje tuseme kama ni watu ambao wanatoka nchi za nje, pengine hospitali yetu itakuwa na mambo makubwa. Watu hawa watakuwa wanalipa kwa dola au watakuwa wanalipa kwa Tanzania *shilling* wale wagonjwa ambao watafanyiwa matibabu hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshmiwa, ninafikiri wagonjwa wa nje ni *out patient*, sijui hebu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mheshimiwa, unajua hii sheria ya Kingereza ukiichukua ukaitafsiri kwa Kiswahili neno '*out patient'* huipati vizuri inakuja

kama *foreign patient*. Sasa Mhe. Suleiman Sarahan, ametafsiri *foreign patient* na sio *out patient*. Sasa *out patient* tafsiri yake kwa Kiswahili ndio hiyo hiyo mgonjwa wa nje. *Foreign patient* ni mgonjwa wa nchi za nje. Kwa hivyo, naomba atukubalie mgonjwa wa nje ni *out patient*, pale unapofika hospitali ukiingia tu wewe unakuwa ni mgonjwa wa nje. Mgonjwa wa ndani ni yule anayelazwa wodini anakuwa mgonjwa wa ndani, yaani *in patient*, lakini sio mgonjwa kutoka nchi za nje kama ulivyokusudia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Maana yake nilikuwa najua mgonjwa wa nchi hii anakuwa ndio wa ndani.

Kifungu 4 Kazi za Hospitali pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, tushapitisha kikitajwa tu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuna (a) na (b) namba mbili vile vile hakusoma Katibu wako.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kikisomwa cha 4 Mheshimiwa, ni chote kama kina (a) mpaka (z), ni zote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Katika kuchangia kwangu Mhe. Mwenyekiti, nilichangia katika kutekeleza majukumu yake, hospitali inaweza kuingia kwenye mikataba ya hospitali nyenginezo, vyuo, hapo sasa, nataka kupendekeza jambo pamoja na fedha na taasisi. Kifungu hiki isomeke neno hilo.

Katika kutekeleza majukumu yake hospitali inaweza kuingia kwenye mikataba na hospitali nyengine vyuo, baada ya neno 'vyuo' liongezeke neno 'pamoja na taasisi za fedha'.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Jaku, atukubalie kwamba libaki hivi, kwa sababu hii taasisi ya kutoa huduma kwa jamii, taasisi ya tiba, si taasisi ya kifedha, wala si taasisi ya *insurance* na serikali inasimamiwa na sheria zake za fedha maalum, kwa hivyo, ndio maana tukatia taasisi zinazohusiana na hospitali ya Mnazimmoja, Taasisi za Sayansi za afya, kwa kuandaa masuala ya mafunzo, shughuli za utafiti, tunahofia sana kwa kuwa *core business* yetu ni kutoa *medical services* kwa wananchi tukianza kwenda kuingia kwenye mikataba ya kifedha tutakuwa tunagongana na Sheria Kuu ya Serikali juu ya usimamizi wa fedha. Naomba atukubalie sana kwamba hawa wataweza kukopa, lile la mwanzo

nimeshamkubalia, yaani wataweza kukopa benki, lakini hawatoweza kuingia mikataba moja kwa moja na taasisi za kifedha ulimwenguni.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hii ni *agency* sio *corporate board*

Mhe.Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ningemkumbusha tu Mhe. Waziri, akaangalia kifungu cha 22(b); ada, malipo na mikopo, kitamsaidia hichi. Kwa hivyo, mimi naomba "pamoja na taasisi za fedha" kitamsaidia huko mbele, wala sio kwa manufaa yangu mimi, kama atakikubalia atakiona faida yake huko mbele 22(b), pana ada, malipo na mikopo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kama atakuwa amenisikiliza Mhe. Jaku, kifungu cha 22, nilikisoma kizima kwa upana wake, nikaeleza ada hapa iliyokusudiwa ni ipi, mikopo iliyokusudiwa ni ipi, fedha za kupokea zipi nikaeleza yote. Tukiweka huku kwenye vifungu vya mwanzo itakuwa ni *direct transaction* na taasisi ya kifedha, ni mamlaka makubwa hayo inaweza tukaichukua serikali kwenye *ransom,* kwa Mkurugenzi Mkuu Mtendaji akaingia kwenye mkataba ambao uta-*commit* serikali nzima. Mfano anaweza kuingia katika mkataba milioni 60 au milioni 70 dola ya kutaka kufanya *expansion*, sasa ile si kazi yake, ile ni kazi ya Wizara ya Fedha na Mipango chini ya sheria kuu ya fedha za serikali.

Hapa hii ni mikataba na Vyuo Vikuu, malipo yale, ada au kwenda kwa miradi midogo midogo ile ya ndani. Mfano unataka kununua kifaa labda kinagharimu labda dola elfu kumi, elfu kumi na tano, anataka mkopo ule anaweza kwenda na patakuwa na *threshold* hizi kanuni ambazo zinataka kutungiwa sheria hii itapanga Mkurugenzi uwezo wake kukopa, mpaka kiasi gani, bodi uwezo wake wa kukopa mpaka kiasi gani, kutakuwa na *threshold*. Ninaelewa nia ya Mhe. Jaku, ni njema anataka kutusaidia, lakini katika nia njema wakati mwengine inaweza ikazaliwa nia nyengine kubwa zaidi. Nashukuru Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hili anajua kama nilitaka kumsaidia na haya yalimkuta katika kipindi kilichopita nilikuja na hoja binafsi na Mwenyezi Mungu kamjaalia kawa Waziri, aliikataa asilimia kupata wizara yake na matokeo yake yakamkuta. Hili lina nia ya vile, ulikuja ukam-*convince* Mhe. Mohammed Aboud, Serikali isikubali kupata asilimia 100. Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea tulikuwa tumeshakipitisha nilikupa fursa tu ili aweza kukuridhisha Mhe. Waziri, kwa vile hakuna mabadiliko tunaendelea.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika mchango wangu ambao niliuchangia hapa kwenye bodi na pia nilitaja majina, lakini nilitoa wazo kwamba najua utaratibu wa taasisi za serikali na idara zake na hizi bodi wanakuwa na wajumbe wa bodi ambao kuwa ni watu wa *ZAWA.* Lakini kutokana na mpango wa hospitali hii nilipoangalia kwa mujibu wa sheria hii na ambao waziri analenga wapi anapotaka kwenda, nilishauri kwa mujibu wa sheria kwamba waziri awe na mamlaka ya kuweza kuchagua wajumbe au mabalozi au marafiki wa Hospitali ya Mnazimmoja ambayo isimfunge hata kuweza kuchagua watu kutoka nchi za nje.

Sasa nilitaka kufahamu kisheria, je, sheria itamruhusu kama akiamua kumchagua raia au *professor* yeyote kutoka Marekani akawa anakuja hapa kila mwaka kuweza kusaidia kutoa mawazo yake na kujenga urafiki wa nia njema. Je, atakuwa ndani ya utaratibu wa sheria kuchagua mtu kuwa balozi wa Hospitali ya Mnazimmoja akiwa Malaysia au China. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi), kwa *contribution* yake hiyo, naomba kumwambia kwamba hapa sheria imetamka Mkurugenzi Mkuu Mtendaji awe Mzanzibar. *The law is silent* kwa hawa wengine, naomba na yeye atuachie ibakie hivyo hivyo ili aweze kufaidika kwa mawazo yake hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri, ameyatoa kimsingi anapotengeneza shughuli kama hizi kwanza tunatizama wale ambao wapo ndani. Hoja ambayo Mhe. Simai, ameitoa hao tunaweza kuwaajiri kama ni *consultancy* wakaja wakatusaidia kwenye maeneo maalum. Lakini hawa ambao wapo aidha Mhe. Waziri, ana uwezo wa kuwachagua humu ndani au anaweza kumchagua mtu kutoka Tanzania Bara kuja kumsaidia kuwa ni sehemu katika bodi hii.

Lakini hawezi akavuka *beyond* Tanzania Bara kwenda kutafuta mtu wa nje huko aje amsaidie awe ni sehemu ya bodi. Lakini anaweza kuajiri *consultancy* akaja akamsaidia. Sasa kwa hivi ilivyo na kwa hoja ambayo Mhe. Simai, ameitoa haitowezekana. Lakini inaweza ikawezekana kama ikiwa kuna haja ya kuajiri huyo mtu aje sasa atoe ushauri na anaweza akaja kutoa ushauri kwa bodi, bodi ikamu-*engage* kuja kutoa ushauri na wakamlipa kwa muda maalum, akafanya kazi yake akaondoka. Lakini sio kumpa ujumbe wa bodi alivyoshauri Mhe. Simai.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri Mwanasheria Mkuu hakunisikia vizuri. Nilichokizungumza kwamba na ninafahamu Wajumbe wa Bodi wanatakiwa wawe ni watu ambao wana uraia wao wa Tanzania na hasa wale wazawa kutoka Zanzibar. Mimi nilichokizungumza ni kitu ambacho ni tofauti, nimezungumzia kwamba kuwa rafiki wa Mnazi Mmoja ambapo sasa hivi tayari duniani nchi nyingi wanatumia mambo kama haya katika sehemu tofauti ambapo wanahitaji watu kuweza kuwasemea.

Lakini mbali kusema kama mimi ni Balozi wa Mnazi Mmoja naweza kuwa ni raia kutoka nchi nyengine, lakini wananialika pengine katika vikao vya bodi katika ajenda ambayo itakuwa nahitajika pale wizara au hospitali inapohitaji mimi nije. Lakini mimi nikiwa kama Balozi nakuwa naisemea Mnazi Mmoja, nawatafutia nyenzo na marafiki, nakuwa nawaunganisha na watu, kimsingi inakuwa haihusiki katika kazi za kila siku au kushiriki katika vikao vya bodi.

Sasa nilitaka kujua waziri, je, atakuwa na mamlaka ya kuchagua mtu ambaye anahisi ataweza kutoa mchango mzuri sio *consultant*, *consultant* ni mshauri, lakini je, kwa mujibu wa sheria kwamba waziri ataamua kumchagua mtu akiwa ni John au Joseph kutoka Marekani kama ni *Professor* wa *Havard* au *Professor* kutoka *University* ya Malasia, au *Professor* kutoka India, au *Professor* kutoka Nairobi hapo Kenya ataruhusiwa kumchagua mtu ili waweze kuunganisha nguvu zao kwa pamoja. Katika kuonesha nguvu hizo hizo je, anaweza kumchagua kuwa Balozi wa Mnazi Mmoja akampa *certificate* yake ili yule mtu aweze kumsaidia kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai, hoja yako mimi pia nimeifahamu, hebu soma kifungu cha 11 cha sheria hii.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, natakiwa nisome au waziri anijibu mimi kama itawezekana…

Mhe. Mwenyekiti: Utaratibu wa bodi, bodi inaweza kuweka utaratibu…

Mhe. Simai Mohammed Said: Mimi nimeshahoji nafasi hiyo, Mwanasheria Mkuu au waziri anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu naomba ukae…

Mhe. Simai Mohamed Said: Haya sawa, sawa ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Hapa tunachokifanya tunatunga sheria, sasa unataka tuweke kipengele cha sheria kitakachomuwezesha waziri kumteua mtu kutoka nje ya nchi, maana yake hata sijaelewa, Mhe. Mwanasheria Mkuu, hebu tusaidie.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wengi watakumbuka kwenye baadhi ya sheria ambazo tunatunga, tunaweka kifungu cha bodi ku-*opt* mtu kuja kuisadia bodi. Anaweza akaja akawa mtaalamu kwenye eneo fulani ambalo linazungumziwa siku hiyo ya kikao cha bodi, lakini mtu huyo anakuwa hana haki ya kupiga kura, yeye anakuja tu anatoa michango yake na anaondoka. Sasa mimi nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, umetuelekeza kwenye kifungu cha 11 kama bodi katika kuweka utaratibu wake hayo ni maeneo ambayo yanaweza sasa yakajipangia yeye wenyewe kulingana na vikao ambavyo vinajadili.

Nikasema kwenye mada hii ambayo leo tunayo basi tutamualika mtu fulani aje atusaidie, kwenye mada fulani tukamualika mtu fulani aje atusaidie. Sasa hiyo ndio maana pana ya kifungu cha 11 ambayo imekusudiwa, sio lazima yale ambayo anayataka Mhe. Simai, yaelezwe humu kimaandishi ayaone, maana pana ya ile ambayo anataka imeshaelezwa kwenye kifungu cha 11 ambacho Mhe. Mwenyekiti, ulimuelekeza Mhe. Simai. Nashukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai, utakuwa unasimama kwa mara ya tatu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante, kwa hiyo nitajieleza ili nifahamike vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Haya.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ni pahala muhimu sana na tunaweza tukamsaidia waziri akapata faida kubwa sana ya nyenzo na fedha, na hili sio jambo la utani. Nchi zetu sasa hivi jirani huko Ulaya wanatumia njia kuweza kuwa *award* familia, kwa mfano familia ya *Rocfeller* kutoka Marekani kama utaamua kuwapa familia ya Gandhi kwamba hawa unawapa ile *certificate* na kuwatambua kwamba hawa ni familia ambao wao ni Mabalozi wazuri wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, unawapa Kitengo cha *INT* wanakuwa wanaki-*maintain* kwa mashine, wana-*maintain* kwa kutia rangi na mambo mengi zaidi ya dola laki tano wanaweza kuwa wanachangia, hii ni heshima inakuwa, hatusemi kwamba wawe ni *body members*.

Sasa katika suala hilo la kumchagua mtu kwamba waziri atakuwa na mamlaka ya kisheria anapoamua yeye mwenyewe ambayo kama atawaalika katika vikao vya bodi *as observers* katika ajenda ambazo wanazitaka, lakini wale watakuwa wana heshima hiyo kama watachagua ni kitu ambacho kinaweza kuleta manufaa na tija na fedha nyingi katika taasisi zetu. Ikiwa Mwanasheria Mkuu anasema kwamba itawezekana mimi nimelipokea na kama waziri atakuwa hafuti sheria atakuwa na mamlaka hiyo pamoja na bodi, mimi naunga mkono naomba mawazo hayo yachukuliwe na yafanyiwe kazi na nitafutahi sana. Naomba Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 5 Kuanzishwa kwa Bodi Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 6 Muda wa bodi
Kifungu 7

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kifungu cha 7(b), ametenda kosa kinyume na maadili au kuwa na tabia isiyokubalika na jamii. Nilizungumza hapa sheria ipo ya maadili ya viongozi, Sheria Nam. 14 ya mwaka 2015, Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia juu ya suala hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku, atakumbuka kwenye ile Sheria ya Maadili tuliyoipitisha hapa kuna orodha ya majina ambayo yametajwa, na kuna watu mle inawezekana hawakutajwa na ndio maana tukaweka kifungu hiki ili tusimuache mtu ambaye atakwenda kinyume na maadili akaenda kwenye sheria ile ikawa hayumo akasema sina pahali sasa pakunikamata. Ndio maana tukakiweka hiki maalum kwa kujua kwamba inawezekana kuna baadhi ya watu kwenye ile Sheria ya Maadili hatukuwataja. Nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hayo ni masikitiko makubwa sana, ikiwa yeye ni Mwanasheria tunafikia sheria mpaka hii hawajaenda kuangalia kitu hiki kama ndicho au sicho, hayo ni masikitiko makubwa…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, amekujibu kwa uhakika kabisa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi nafikiri angeenda kuiangalia hiki kifungu labda tukiache kwanza, mimi katika kumbukumbu zangu naona kama wametajwa watu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Jaku, kwanza kwenye bodi hii Mheshimiwa, kuna wajumbe ambao watakuwa sio

watumishi wa umma, kama sio watumishi wa umma Sheria ya Maadili haiwezi ikawabana, kwa sababu Sheria ya Maadili imeeleza watu ambao inawabana. Sasa sheria hii kama kuna mtu ambaye amekuwa *covered* kwenye sheria ile ya maadili atashughulikiwa kule, kama hakutajwa kifungu hiki pia kitamshughulikia, ndio hoja ambayo nimesema, nimesema kwa uhakika yeye ndio anabahatisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimezungumza Kiswahili fasaha kabisa wala sio Kiingereza…

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee eeh!

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aah! Tusiendelee, ikaangaliwe hii sheria kama ipo au haipo hiki kifungu tukiache kwanza…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, anayekujibu ni Mwanasheria Mkuu na ana uhakika na hicho anachokisema.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nikaja nikamthibitishia mimi, tutafanya nini?

Mhe. Mwenyekiti: Utakuja nayo hiyo hoja humu ndani, naomba tuendelee.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante wakati na mimi nachangia kifungu hiki cha 7, nilisema kama kuna sifa hapa Mjumbe wa Bodi atasita kuwa mjumbe nikaishauri, nikasema hata akifariki pia anakuwa amekosa sifa, na mimi sikupata kuona yale majibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na nimeliandika kwamba Mama yetu Bi. Panya alizungumzia katika hizi sifa moja wapo ni kifo, na ukiangalia sheria nyingi zinakuwa nayo kipengele hiki kimoja cha kifo, yaani ujumbe wake utasita mara tu atakapofariki dunia. Sasa naomba hili nilipokee, nilichukue, nishauriane na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa sababu kwenye sheria nyengine nakumbuka zipo nyingi, nishauriane nae na atawasilisha mezani…

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mheshimiwa, tunakiamua hapa, yaani kama kiingie ni hapa au vyenginevyo tunakiacha ni hapa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ukilitizama lina sura mbili. Moja ni kwamba unatizama hoja ambayo ameitoa Mhe. Panya, kama tuandike kifungu hicho ili inapotokea yule mtu anapofariki tuweze kufanya *replacement*,

ndio maana Mhe. Panya, anatusisitiza tukiandike hicho. Lakini ya pili unapoacha unasema aah, umeacha haya yote lakini haya mliyoyaandika yanapotokea haya ndio mumchague mtu mwengine. Sasa yote yanazungumzika na hata kwenye mswada wa mwanzo hilo neno pia lilikuwepo, kwa hiyo, wala sio tatizo tunalichukua tutalishughulikia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mheshimiwa, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, tunaendelea pamoja na marekebisho, eeh.

Kifungu 7	Kusita kuwa Mjumbe
Kifungu 8	Kazi za Bodi Pamoja na Marekebisho yake

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa tena nafasi. Nilipokuwa nikichangia nilieleza *concern* yangu katika kifungu cha 8 (i), kwanza kifungu cha 8(h) namshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kuweza kutoa ufafanuzi wa wizara kwamba kule alisema wizara itakayoshughulikia masuala ya afya, namshukuru sana.

Lakini kifungu cha 8(i) nilipendekeza kwamba hiki kifungu kisomeke "kupendekeza masharti ya utoaji wa huduma na maslahi ya ajira kwa wafanyakazi wa hospitali ya Mnazi Mmoja", na hayo maneno mengine kwa "kufata Sheria ya Utumishi wa Umma" nilisema yasiingie.

Mhe. Mwenyekiti, najua kuna Sheria ya Utumishi wa Umma, lakini vile vile kuna Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kumekuwa na tatizo kubwa sana hasa katika maslahi, hasa katika kada maalum na utakuta hizi taasisi zinaweka mapendekezo lakini hayazingatiwi, na hii wakati mwengine inasababisha madaktari wetu mabigwa kuondoka nchini kwa sababu ya kubanwa katika maslahi. Sasa nilipendekeza kwamba hili neno "kufata Sheria ya Utumishi wa Umma" liondoke. Kwa hiyo, labda Mhe. Waziri, hebu anisaidie anakubaliana vipi na hoja yangu hii.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, nadhani Mhe. Hamza, anajua hoja yake hii hatuwezi kukubaliana nae, lakini kwa sababu alichangia na kapata *forum* basi lazima asimamie hoja yake. Lakini huu ndio utaratibu ulivyo Mhe. Mwenyekiti, kama kwa sasa hivi Sheria ya Utumishi wa Umma ndio inayolazimisha mambo haya, na haya kwa sababu ya yale yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe, walikuwa wakiyazungumza humu ndani kama inawezekana unakwenda taasisi moja mfanyakazi wa kada fulani na

taasisi nyengine mfanyakazi wa kada fulani wanapishana kwenye kupata mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, wameyazungumza wao Waheshimiwa Wajumbe, sasa kuweka usawa ndio maana unaambiwa uende kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ili wao sasa wanapokwenda na mapendekezo yako wao wanakwambia, aah, hili tunaweza, hii ni Sera ya Serikali haiko hivi, hii haiko hivi, kwa sababu ya kuweka usawa kwa watumishi wote wa umma. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Hamza, na yeye anajua kwamba kwa Sheria ya Utumishi wa Umma ilivyo hatuwezi tukakibadilisha vyenginevyo kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tunatunga sheria hapa lakini tunajua *efficiency* ya sheria hii bado haitokuwa kama vile tunavyoikusudia, na hili Mhe. Mwenyekiti, sisi wenyewe ni mashahidi. Katika maeneo tofauti hii Sheria ya Utumishi wa Umma ipo na Tume ya Utumishi wa Umma ipo, wafanyakazi wanapeleka kilio chao kwa Mhe. Rais kuhusu maslahi yao. Kwa hiyo, ina maana hii tume sitaki kusema kwamba imeshindwa kazi, kwa kweli haitendei haki kada nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nimetaja orodha ya madaktari bingwa waliobakia Mnazi Mmoja, kada karibu 15 ina daktari bingwa mmoja mmoja. Kuna kada nyengine kama mfano ile ya mambo ya kina mama ambayo Mhe. Nadir, mara nyingi alikuwa hapendelei madaktari wanaume kuwahudumia kina mama, walikuwepo wamekimbia mmoja yuko *Aga Khan Hospital* na mmoja amekwenda *African Union* na hii yote inatokana na nini? Bodi zinapopeleka yale mapendekezo ya maslahi hayakubaliwi, sasa leo tunapitisha sheria hii ili kuelekea kwenye rufaa, Mheshimiwa, hii ni ndoto na hii tunajidanganya.

Mhe. Mwenyekiti, haya masuala ya maslahi bodi itapendekeza kwa waziri, waziri na yeye ni mtu ambaye anajua umuhimu wa hili jambo, kama tutakiachia kifungu hiki kubakia kama Sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu suala la maslahi, hapa Mheshimiwa, tutakuwa tunaimba, tutapiga kofi hakuna kitakachofanyika. Mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, haya maneno ya mwisho yaondoke pamoja na kwamba tunajua katika masuala ya uajiri hakuna tatizo, lakini inapokuja suala la maslahi Mhe. Mwenyekiti, hakuna. Kwa hiyo, tusimuachie Mhe. Rais kila siku kutamka, kwenda kutoa maslahi wakati Tume za Utumishi zipo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Hamza, anapenda tukae tuamke ili kuitetea hoja hii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza, atakumbuka kama hoja ya kuwepo kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni hoja ya Kikatiba imeanzishwa na kifungu cha 116 cha Katiba na ikapewa kazi zake. Katika kazi ambayo imepewa ni kupokea mapendekezo kutoka kwa hizi tume nyengine ambazo inazisimamia, hilo ni sharti la kikatiba, kupokea mapendekezo kutoka kwenye hizi tume zote ambazo inazisimamia. Sasa kuna tume ambazo zimetajwa kikatiba, lakini kuna bodi kama hizi ambazo nazo zinafanya kazi kama za kiutumishi nazo zina wajibu wa kupeleka taarifa zao kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Sasa huwezi uka-*avoid* Sheria ya Utumishi wa Umma na huwezi uka-*avoid* kifungu cha 118 cha Katiba kwa sababu ndio msingi wake ulioanzia kule.

Kwa hiyo, sasa utaposema tufute kifungu hiki, maana yake unasema ule msingi mzima wa Katiba ambao umeandikwa ndio uliopelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma nayo tuifute. Sasa Mhe. Hamza, anayosema inawezekana tulipoanza ilikuwa hivyo, lakini sasa hivi naamini Waziri wa Utumishi wa Umma yupo naamini sio tulivyo. Kwa hiyo, hiki Mhe. Mwenyekiti, wala sitoomba tupige kura kwa sababu hoja zetu sisi zina mashiko zaidi kuliko hoja ambayo Mhe. Hamza, anaisimamia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi wala sitofika pahala pakupiga kura, nilikuwa naeleza ile *concern* yangu na Mhe. Mwenyekiti, hebu baadae tafuta katika kumbukumbu zako niliwahi kuleta mapendekezo ya marekebisho ya Katiba na moja katika eneo ambalo lilokuja kuvuruga utaratibu mzima na taasisi nyengine ni suala la Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria Mkuu, ndio maana akasema anajua kwamba hii hoja hawatoikubali na mimi nilikuwa najua kwamba hawatoikubali, lakini nafikiri hii sasa ndio itapelekea kwamba labda yale marekebisho ya Katiba yaje ili hawa mabingwa wetu wasiondoke.

Lakini pamoja na hayo na namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri, anayeshughulikia masuala ya Utumishi katika eneo hili naomba sana bodi ije isikilizwe kwa kuwa kuna hicho kikwazo cha Katiba angalau katika suala zima la maslahi ya madaktari wetu mabingwa ili wale waliondoka warudi, basi aje aisikilize bodi na waziri ili kuweza kuhakikisha kuwarudisha hawa ili mambo yetu yaende vizuri. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti na mimi wakati nachangia kuna mambo yote yameungana haya, kwanza nilizungumza kuhusu habari ya mikataba ya madaktari. Mheshimiwa, unajua Muhimbili imeshakuwa hospitali

ya rufaa, imeshakuwa hospitali ya Taifa, matokeo yake tumeyaona. Madaktari wale wale bingwa wanaenda kufanya kazi nyumbani au kwenye hospitali zao au hospitali za kulipia. Sasa nilimuuliza Mhe. Waziri, kuhusu mikataba ya madaktari hawa, kwa sababu daktari anaambiwa ana uwezo wa kuhimili wagonjwa wangapi, leo anaondoa watu njiani au anakwenda kujichosha tena kwenye hospitali nyengine. Mikataba hii nikamuuliza Mhe. Waziri, je, una mikataba nao vipi hawa madaktari.

Jambo la pili, ni kuhusu habari ya dawa, akasema kwamba ukitaka *glove* sisi tunakupa lakini ikiwa hamna unakwenda ukachukua pale…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan, kifungu hiki ni cha 8…

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ndio, Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Kipengele kipi unachohoji?

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Kipengele kipo hapa Mheshimiwa, hapa kuna kipengele cha kuhakikisha huduma za afya zinatolewa na hospitali ukizingatia vipaumbele vya kutumikia wananchi na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika. Sawa Mheshimiwa?

Mhe. Mwenyekiti: Kipengele kipi?

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Kipengele cha 8(f).

Mhe. Mwenyekiti: Sasa unapendekeza tufanyeje, tukiondoshe, tukizidishe hichi kipengele.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hichi kipengele Mheshimiwa kwa sababu ninahisi kwamba haya matibabu yanakuwa ya kipesa pesa, ifanyiwe marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti: Kiwe vipi?

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, hapa huduma hizi maana yake tunamuhakikishia mwananchi kwamba tutakupatia huduma bora na kila kitu wakati huduma hizi zinakwenda kwa pesa pesa. Hivyo, ningeshauri hapa hichi kihuduma labda iingizwe pesa iwe uhakika, sio kuwa ina maduka ya kuuza nje, sio pawe na madaktari ambao wanaenda hivyo, kwa sababu bila ya pesa hapatakuwa na huduma ya uhakika katika hichi kipengele.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kweli Mhe. Suleiman, hajajieleza vizuri katika hili, lakini katika mchango wake nilimfahamu hapo awali na nikachangia kwamba katika Bodi itakapotekeleza kazi zake kuna hichi kifungu cha mwisho cha (p), kinasema;

"Kutekeleza jambo lolote jengine ambalo ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake au kama itakavyoelekezwa na waziri wa sheria hii".

Kwa hiyo, bodi imepewa uwezo wa kuamua jengine lolote ambalo halimo katika orodha hii, sasa hayo anayosema ya ku-*charge* ama kuto-*charge* yako kwenye kifungu cha 27, kwamba Sera ya Mapinduzi inaendelea kulindwa, wananchi wote hawatakiwi kuchajiwa kwa huduma za afya. Lakini tumeweka kifungu cha 27(2) ili wakati ile hospitali inatumika kama *University Hospital* kwa ajili ya kufundishia na kadhalika, waruhusike ku-*charge* zile *services*, lakini sio ku-*charge* wananchi kwa ajili ya huduma za afya. Sera ile bado haijafutwa, ile ni Sera ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

Kwa hiyo, kwa hoja yako Mheshimiwa, katika kifungu hichi mimi naona tuwaruhusu Bodi wapange watakavyopanga wao na naamini hayo yote yaliyotajwa ndio majukumu makuu ya Bodi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe.Suleiman Sarahan Said: Haya namsikiliza waziri.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa nasemea kifungu baada ya kifungu (p) tuongeze na... wakati nachangia niliongea masuala ya madawa na mali za hospitali. Kama itawezekana basi ilikuwa nashauri kiongezwe kifungu chengine kinachosema kwamba...

Mhe. Mwenyekiti: Tuzidishe (q) baada ya (p).

Mhe. Simai Suleiman Said: Eeh! iongezwe (q), hicho kifungu ninachotaka kiongezwe endapo kama kifungu nambari (i) kitatosheleza basi kitakuwa hakina haja, lakini wacha nikisome halafu Mwanasheria Mkuu atatushauri. Nilikuwa nashauri kwamba kifungu cha (q) kinasema; "kila iwezekanavyo, basi uongozi wa hospitali utasimamia kuhakikisha kwamba kila mali zote za hospitali ya Mnazi Mmoja zitakuwa zina nembo au alama ya hospitali kwa nia njema au kuhakikisha ubadhirifu na wizi au chochote kinachotokezea tunakuwa tunakijuwa".

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mara nyingi binaadamu unapokuta mali ya hospitali mtu anatumia inamfanya ajisikie vibaya, wewe inakuwaje unatumia

mali ya hospitali, unaiibia, imepotea, sasa kwa vile hii hospitali itakuwa na mali nyingi, vitu vingi kutoka mabetshiti, vitanda, madawa, hizi huduma zote ni vizuri za hospitali zikatofautishwa na zile ambazo zilizokuwa nje uraiani ambazo wananchi wananunuwa. Sasa tukisema kwamba tuweke katika kanuni, nahisi itakuwa haijatiliwa mkazo kama hali ilivyo sasa hivi. Sasa mimi ninaona iwekwe kidogo katika sheria hapa ili ule usimamizi wa Bodi utakapoanza na katika *procurement* watakuwa wanasimamia moja kwa moja kuhakikisha kwamba vile vitu vinakuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu baadae mimi naamini katika hiyo hoja ambayo waziri anayoitaka na Mhe. Jaku, alivyozungumza...

Mhe. Mwenyekiti: Jaribu kuwa *brief* kidogo Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante, naamini kwamba ukenda Mnazi Mmoja utakuta wanapewa taula, maji ya moto, unapata hichi, sasa hizi lazima ziwe na nembo.

Mhe. Waziri wa Afya: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii tena na namshukuru Mhe. Simai. Lakini hii ni sheria, sheria haiwezi kubeba kila kitu kuweka nembo kwenye mashuka, mito, halafu ikiibiwa yule mwizi atafanywa nini, kuna vitu vyake vyengine. Naomba sana haya tuliyoyaweka hapa yana-*cover almost everything* na ni mengi kwa kweli, tungeweza haya yote tukayakusanya kwa kifungu kimoja tu, tukasema Bodi itajipangia majukumu yake kwa mujibu wa taratibu zitakazopangwa katika kanuni itakayotumwa na Bodi, tungekuwa tunamaliza kila kitu. Sasa hayo mengine tuwache kanuni, *otherwise,* tutakuwa tuta-*exhaust the whole list*, kanuni itakuwa haina kazi ya kufanya, hayo *the nitty-gritty*, *the detail infomation* naomba zibakie kwenye kanuni, hii ni sheria iwe juu zaidi, ahsante.

Mhe. Simai Mohamed Said: Sawa mimi sina tatizo.

Kifungu 8	Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 9	Vikao vya Bodi
Kifungu 10	Akidi ya Vikao
Kifungu 11	Utaratibu wa Bodi
Kifungu 12	Posho

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninatoa mchango wangu nilipendekeza kitu katika kifungu cha 12, kuna maneno tuongeze, hapa inasema; "wajumbe wa bodi watapaswa kulipwa posho kwa kadri

itakavyowezekana itakavyoamuliwa na waziri". Sasa ninapendekeza kwamba "iwe kwa kushiriana na Menyekiti wa Bodi".

Mhe. Waziri wa Afya: Ni kweli Mhe. Mihayo, alitoa mchango huo na namshukuru kwa mchango wake. Hivi sasa hivi ndani ya Wizara ya Afya kuna Bodi na Bodi kabla hazijaamua lolote wanaleta mapendekezo yao kwa Mhe. Waziri na mimi naweka *sign* kwa mujibu wa bajeti iliyokuwepo na kwa mujibu wa bajeti iliyopangiwa ndio wanalipana maposho yao. Kuna Bodi pamoja na Mabaraza yale zaidi ya tisa ndani ya Wizara ya Afya na huo ndio utaratibu uliokuwa ukitumika. Sioni kwamba hapa waziri anaamua peke yake, imeandikwa lakini haamui waziri peke yake, maisha Bodi wanaweka *recommendation* na hata muda ukimalizika wakati mwengine waziri hajui kwa sababu zinakuwa bodi nyingi, wanaleta zile *recommendation* ni bodi, kwa hiyo, mimi sioni kama kuna tatizo lolote hapo, waziri anashauriana daima na bodi husika.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, lakini kuna maisha baada ya leo na kesho, ipo siku atakuja mtu atajiona kwamba yeye ndiye waziri, atakuwa na mamlaka kuliko mwenyekiti atakayekuwepo. Sasa nashauri kwa umuhimu na kumthamini Mwenyekiti wa Bodi hichi kifungu naomba tukiongezee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mihayo, nafikiri yale maelezo ya Mhe. Waziri, kwamba yale mapendekezo anayoletewa na bodi, *actually* anapoyasaini yale inakuwa ndio kama kafanya waziri ndio inavyokuwa, wao wanaleta mapendekezo lakini yeye akiyakubali tu yale mapendekezo, maana yake aliyefanya vile ni waziri. Kama sisi tunapitisha sheria hii, sisi Baraza la Wawakilishi, lakini sheria inatoka mbali, imetungwa na watu wengi, imeingizwa vitu vingi tu, lakini ikisha kupita hapa hii sheria tuliyotunga ni sisi Baraza la Wawakilishi, sheria imetungwa na Baraza la Wawakilishi, wala sio na Baraza la Mapinduzi, wala sio Kamati ya Makatibu Wakuu, ni Baraza la Wawakilishi, na hiyo nafikiri iko katika mzingira kama hayo. Mhe. Waziri, labda kuna nyongeza.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa, nakushukuru sana umetoa mfano mzuri kweli kweli na mimi naomba nimalizie mfano wako. Sheria ikishatoka Baraza la Wawakilishi lazima Rais akaitie saini, kama hakuitia saini ile sheria itakuwa *not effective*, kwa hiyo, naomba sana tukianza kuongeza hapa baada ya kushauriana, kujadiliana, tunaweza tukatumia maneno mengi sana na tukenda mlolongo mrefu. Waziri tumpeni mamlaka yake ya kuamua, lakini waziri daima anashauriwa, ile saini yake anayoiweka chini ndio maamuzi yanakuwa

ya waziri. Sasa hivi mimi nikishaweka kwenye hii imeandikwa hapa mwisho, imeandikwa Mahmoud Thabit Kombo, Waziri wa Afya katika sheria na mimi ndiye nitakayeweka saini.

Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema imepita kote, sijatunga mimi wala sijakaa mimi peke yangu, yameletwa mambo mbali mbali na mimi nimeingiza ya kwangu, na mimi mengine yangu niliyoyaingiza yamepingwa hivyo hivyo. Kwa hiyo, naomba sana akubali kwamba iamuliwe na Waziri. Najuwa khofu yake kwamba kama waziri atabadilika atakuja kuwa vyenginevyo, sidhani kama litaweza kutokezea jambo kama hilo, ahsante.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri Mhe. Waziri, kamalizia neno zuri sana, kasema sidhani, ina maana lolote linaweza kutokea kwa kauli yake ya neno 'sidhani'. Sasa bado ninarudia pale pale upo umuhimu wa kuongeza kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mihayo, ni mara ya tatu hiyo sasa hivi na bado hujakubaliana na sisi, kwa hiyo, tutalazimika kulihoji Baraza. Kabla hatujahoji nimpe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Mhe.Dkt. Mwinyihaji.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, namuomba Mhe. Waziri, ayaheshimu makubaliano tuliyoyapitisha kwenye kikao na makubaliano hayo tumekubaliana kwamba tuongeze kifungu kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi na yeye alikubali, ndiyo tukapitisha hicho kifungu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, katika karatasi iliyowasilishwa humu Barazani ambayo inaingia kama *official Hansard* hii, ndiyo maana neno 'Taifa' tukalijadili kwa sababu limo humu, neno 'rufaa' tukalijadili kwa sababu limo humu, lakini hili halimo humu. Sasa ningeomba Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, anisaidie mimi binaadamu pia, anioneshe tu humu katika hii orodha nitashukuru sana.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa bahati mbaya sana huyu Katibu wa Kamati alisahau na si hichi tu, tumegunduwa baadhi ya vifungu Katibu wetu hatumlaumu Ramadhani hii alipitikiwa hakuviandika vizuri, kwa hiyo, hata sisi tumeshauri Kamati tukimaliza yale yote na mengine si *substantial,* lakini ni mazuri tu kuwemo. Lakini hili sote wanakamati, kila utakayemsimamisha mmoja atakubali, hivyo ndio tulivyokubaliana na *it doesn't make any difference,* kama waziri kakubali, kuna tatizo gani kusema "kwa kushauriana na mwenyekiti".

Mhe. Mwenyekiti, lakini kama alivyosema mwenyewe siku zote wanashauriana, kwa hiyo, nafikiri hakuna tatizo, kama alivyosema mwenyewe tunashauri. Mimi naomba sana akubali yale makubaliano yetu ya kwenye kamati ayaheshimu. (*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuzungumzia ya kamati, lakini kama ambavyo unavyojua kuna kanuni zinavyotuelekeza kwenye kamati tunapokea ushauri, linaloamua ni Baraza, hizi kanuni ndio zinavyosema, lakini wakati mwengine mara nyingi huwa tunakubaliana na mapendekezo ambayo Waheshimiwa Wajumbe kwenye kamati wanayatoa kwa sababu yanakuwa ni mazuri na yenye msingi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachosema wala sioni kwa nini tuvutane, kwenye jambo ambalo hivi ni vifungu *common* ambayo tunavitunga. Ukitizama sheria zote ambazo tunatunga, *this other common provision* ambazo tunatunga na moja ya jambo ambalo inatakiwa usimamie kunapotunga sheria ni *consistency* kwenye vifungu ambavyo unavitunga. Sasa unapoanza kubadilisha leo umetunga hichi, kesho umetunga hichi, kesho kutwa unatunga hichi, unaondoa ule msingi wa utungaji wa sheria yenyewe. Sasa ndio maana kuna baadhi ya vifungu unakuta *consistently* vinarudia. Vifungu vya Bodi, Mikutano ya Bodi, Uendeshaji wa Bodi, Utaratibu wa Malipo, hivi ni vifungu ambavyo *consistently* vinakuwepo kwenye sheria yote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ningewaomba, ushauri ni mzuri, lakini kwa sababu ya kulinda ile *consistency* yetu ya utungaji wa sheria tukubaliane tuendelee kama tulivyo ili baadae sasa tuje tukubaliane.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Waheshimiwa, kwa sababu kifungu hichi kwanza kilikuwa kimeshahojiwa mara tatu, nimemruhusu Mhe. Dkt.Mwinyi, kwa sababu nilihisi ni Mwenyekiti wa Kamati ambayo inahusiana na hii wizara labda alikuwa na mawazo ya kutaka kubadilisha au vyenginevyo, lakini nilikuwa tayari kwa ajili ya kukihoji hichi kifungu, kwa sababu Mhe. Mihayo, alikuwa hataki kukiachia, aliendelea kukishikilia. Kwa hiyo, sasa natumia nafasi hiyo kuhoji. Kifungu hichi kinakubaliwa?

Wajumbe: Ndiyoo!.

Mwenyekiti: Makubaliano haya bila ya kuzingatia yale marekebisho anayopendekeza Mhe.Mihayo, ndio maana yangu, ndiyo tunaendelea.

Kifungu 13 Kumbukumbu za Vikao

Kifungu 14 Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15 Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16 Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji
Kifungu 17

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kama kuna pahali wanapopata shida wananchi ni hapa, wala sina mashaka nacho kifungu kutoka (a) mpaka (f). Kilio changu kwa huruma kubwa hapa wajumbe niliomba wani-*support* kwa hali na mali na mimi ndiye ninaepata shida sana kwenda Mnazi Mmoja kumtafuta waziri, wakati mwengine anaweza akapokea simu na wakati mwengine asipokee. Dkt. Jamal, unaweza kumpata pengine kalala binaadamu asipokee. Napendekeza kiongezwe kifungu (j) *customer care, twenty four hours*.

Mhe. Mwenyekiti, sababu gani. Daktari anapofanya makosa huna pa kwenda kulalamika, sikilizeni vizuri sana Waheshimiwa Wajumbe, ni kifungu muhimu sana, tena sana, lugha ya matusi unapopata kwa daktari huna pa kwenda kulalamika, umekwenda daktari hayupo, hichi kiwepo *twenty four hours*. Naomba sana kama tuna nia nzuri kweli kweli ya kutumikia wananchi, kama tuna nia mbaya ya kutumikia wananchi, sawa, lakini hapa nitasimamia msimamo wangu mpaka dakika ya mwisho na mpaka pumzi yangu ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, watu wote wamechaguliwa na wananchi, kwa hiyo, huhitaji kusisitiza hivyo. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kama utakumbuka hapa katika hoja hii nilitoa ufafanuzi wa kutosha pale nilipokuwepo, lakini bahati mbaya ukiwa unaendesha *vespa* wakati mwengine upepo inakuwa hata kama una redio huwezi kusikia.(*Makofi*)

Sasa naomba nitoe tena kwa ufupi. Niseme kwamba tulimkubalia Mhe. Jaku, katika kifungu hichi na nilimtaja hapa kama yupo ananisikia, tulitaja kwamba tunamkubalia 17(1)(a) iwe Idara ya Huduma na Tiba, zile huduma ndio zitakuwa huduma pamoja na *customer service department*, huduma kwa wateja, ndio atakapopeleka malalamiko yake, hizo simu anazotupigia mimi na Dkt. Jamal saa nane za usiku zote zitakuwa zinakwenda kule moja kwa moja. Kwa sababu watakuwa wanahusika, wana bodi na mamlaka yao sasa, mamlaka yao kamili kule Mnazi Mmoja. Sasa hili nilishamkubalia lakini ndiyo yale matatizo ya kuendesha bila ya *helmet*, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, muda mwingi ulikuwa humo ndani, maana yake ulikuwa ukiingia na kutoka wakati akijibu Mhe.Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, yote haya yanasababishwa kwa sababu hatujapata pesa za gari, ndio tatizo lote nikawa naendesha *vespa*, ingelikuwa tumeshapata pesa za gari nisingeendesha *vespa*.

Mhe. Mwenyekiti: Naam, sikusikii vizuri Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hii yote Waziri wa Fedha hajatupa fedha za gari, wala nisingeendesha *vespa* mimi, ingelikuwa nishapata pesa za gari ingelikuwa *vespa* nishaiacha zamani.Mhe. Mwenyekiti, hichi kitengo nataka aniambie kitakuwa masaa 24 kwa kufanya kazi? Hapo tumalizane kama kitafanya kazi masaa 24 wala sina mashaka naye mimi.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kitengo hichi hata hivi sasa kipo, kwa sababu hospitali inakuwa na masaa 24, kitengo hichi hata hivi sasa kipo. Mtu wa kwanza kabisa wa kupokea malalamiko ni *customer care* ambayo ni *PR Department* sasa hivi, lakini wa pili ni *Matron* saa 24. *Matron* wa kazini akiondoka, naomba Mhe. Jaku, nimfahamishe ndiyo *regulation* zilizokuwepo sasa hivi, *Matron* wa kazini akiwepo anaacha *Matron* watatu usiku, zile *time* za kazi zikishakwisha anaacha *Matron* watatu usiku na wote wale wana *on call number* zao, namba zao nimeshawahi kuzitoa hapa hapa katika Baraza lako tukufu kusema kwamba hawa wanakwenda kwa *level* hii ya kama kuna tatizo lolote la kuwasilisha matatizo, kuwasilisha maoni, hata mtu kama hawezi ku-*afford* wakati mwengine, hiyo *glove* hawezi ku-*afford* kuna *department* ambayo inashughulikia masuala hayo na namba zao wote nilizisoma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, hapo itakapoundwa bodi hii ndio itaimarika zaidi. Lakini ninaomba nimuahidi kwamba kitengo hicho tutahakikisha kwa ajili ya Mhe. Jaku na nwaanchi wote kipo saa 24, ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana, lakini haya anayozungumza sawa na sitaki kumwambia lugha gani anatumia, lakini hichi kitengo hakipo, mimi nimeshampigia simu kuna wagonjwa wa Kipindupindu, wale madaktari wananifata mimi, Mungu shahidi, hichi kitengo Mhe. Mwenyekiti, hakipo, tuweke *Hansard* sawa, kama utaanza utaanza hichi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 17 Kuanzishwa kwa Idara Pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 18 Uteuzi wa Wakurugenzi wa Idara pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19 Kamati ya Uongozi

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, katika michango yangu nilikuwa na wasiwasi wa kifungu cha 19, nilisema kuna vifungu viwili vya nambari mbili. Vile vile, nikatia wasiwasi wangu kwamba hicho kifungu kilichoandikwa "Mwanasheria wa Hospitali atakuwa Katibu wa Kamati", pengine ilikuwa ni kifungu (f) na kama sio hivyo, maana yake iwe kifungu namba 3, sijapata ufafanuzi. Naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, kwa mtiririko ili uwe mzuri nakubaliana na Mhe. Rashid Makame Shamsi, kwa sababu yeye maoni yake yalikuwa kwenye (b) Wakurugenzi wa Idara, hapa ndivyo ilivyokusudiwa idara zote ambazo zimeundwa kwenye sheria hii, nikatoa ufafanuzi wa Wakurugenzi, Muhasibu Mkuu wa Hospitali, Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu wa Hospitali, lakini katika mtiririko mzuri Mwanasheria huyu tunaomba ibakie kuwa nambari 3. Kwa sababu Mwanasheria huyu ni wa wizara ambaye anatokea katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, inakuwa kama Katibu kajitenga kidogo hayumo, ni *non-voting member*, tukimtia huku itakuwa kama na yeye ni *member*, yaani *voting member*.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani Mheshimiwa alichokuwa anajaribu kurekebisha ni *numbering*.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, iwe nambari tatu(3).

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 19 Kamati ya Uongozi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 Majukumu na Kazi ya Kamati ya Uongozi
Kifungu 21

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nasimama na kifungu cha 21(1), wakati nachangia nilishauri hapa kuna hospitali inaweza kwa mujibu wa masharti na vigezo kuajiri au kuteuwa mfanyakazi au huduma ya mshauri elekezi, au mtaalamu kama itakavyoona inafaa kwa utekelezaji mzuri na majukumu ya hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwa kuangalia kwamba hospitali ni kamati au ni jukumu la watu wengi, uteuzi kama huu mimi ningeshauri ama awenao Rais au

waziri, kitengo hiki kingesahihishwa kidogo kama inawezekana, huyu ambaye anateuwa huyu mtu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu kwa sababu hata kwenye kamati tulikipitia, lakini tukarekebisha 21(2) kama yanavyoonesha marekebisho. Hiki kifungu cha 21 tunataka tumpunguzie hatutaki tumuongezee nae madaraka makubwa sana, kwa sababu waziri tayari kuna vitu vingi anafanya. Hili tuliache kama lilivyo Mheshimiwa, ili bodi na uongozi wake iweze kufanya kazi. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi niliona kwamba waziri ananielekeza kwa majukumu mengi ya Rais kwamba huyu mtu, lakini mimi nilikuwa napendelea sana kwa upande wangu kwa kushauri angekuwa mteuzi yeye waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hapa kwa kuwa imeandikwa hospitali inaweza kwa mujibu wa masharti na vigezo vya kuajiri na kuteuwa mfanyakazi au huduma ya mshauri elekezi, kwa sababu huyu ni mshauri elekezi, ama mtaalamu, tukimuingiza waziri tukamshusha chini huko kwenye wataalamu, hii maana yake nakusudia *consultancy,* labda kuna *negotiation with foreign university* na vitu vya namna hiyo, kwa kweli waziri anakuwa ni mwanasiasa. Mara nyingi na inawezekana ikawa sio *profession* yake, kama mimi sio *profession* yangu *medicine,* tutakuwa tunamleta chini kwenye *technical issues* ambazo hazina haja, tuwaachie. Kwa sababu huyo Mkurugenzi Mkuu lazima awe *technical person,* lazima awe mtu wa *medicine,* tumuachie yeye jukumu hilo ili kuchagua *consultant* ambaye atakaemsaidia katika ushauri wa kitaaluma. Ahsante naomba ibakie hivi hivi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina nia ya kuzuwia kifungu lakini bado natahadharisha, kwa sababu kasoma nusu, majukumu mpaka makubwa na mazuri ya hospitali, hiki ni kitu kikubwa kama kocha katika Timu ya Taifa. Mara nyingi Rais anachukua nguvu yeye au waziri, lakini mimi sizuwii, nilikuwa natoa tahadhari kama anaona waziri inafaa, tuendelee.

Kifungu 21 Wafanyakazi wengine pamoja na...

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti samahani, kuna marekebisho kidogo ambayo yalikuwa *proposed* kwenye kamati.Ukisoma mapendekezo ya kamati kwenye kifungu cha 21(2), mapendekezo yao ni kuongeza maneno "baada ya kupendekezwa na kuthibitishwa na bodi". *Of course,* ni mapendekezo mazuri, lakini sasa ukisoma kifungu cha 8(1)(a), haya ambayo

tayari yamekuwa yamependekezwa ni moja ya kazi ambazo zinafanywa huko na bodi. Sasa mimi ushauri wangu ni kwamba hiki kifungu kibaki kama kilivyo ili kifungu cha 8(a) ambacho tayari kamati walipendekeza tayari kimeshasema hayo kibaki kule kwenye 8(1) na hii 21(2) kibaki kama kilivyo na tusifute Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, pendekezo ni kwamba tukipitishe bila ya marekebisho.

Mwanasheria Mkuu: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, kifungu hiki bila ya marekebisho kinakubaliwa?

Wajumbe: Ndioo!

Sehemu ya Tano
Masharti ya Fedha

Kifungu 22 Fedha za Hospitali
Kifungu 23 Kubakiza Fedha

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, vipi tulikuwa tushakipitisha, haya tukusikie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kutetea hoja yangu ya kuhakikisha kwamba hii sheria tunayoipitisha inaleta ufanisi katika hospitali. Kifungu kinasema Hospitali inaweza kubakiza fedha au kiasi cha fedha kinachopatikana kutokana na malipo ya huduma ilizozitoa kwa kiwango kitakachokubaliwa na waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo la Waziri wa Fedha na Mipango aliyeko sasa hivi, lakini hoja yangu inakuja hapa. Mara nyingi hospitali na kwa sababu hizi fedha sasa hivi zinakusanywa na hospitali na fedha hizi zinakwenda Wizara ya Fedha, matokeo yake yanakuja malalamiko wakati mwengine mpaka jenereta linakosa mafuta. Hiyo nimetoa mfano tu, lakini kimsingi nakusudia kwamba fedha zinakusanywa zinakwenda Wizara ya Fedha, hospitali kuna mambo mengi ya *emergency* yanataka fedha kwa ajili ya kutoa huduma, fedha zile zinakuwa hazipatikani kwa wakati, ndio maana nikapendekeza bado suala zima la yale makusanyo ya fedha yabakie katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kwa kuwa pale kutakuwa kuna Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Bodi na Waziri atakuwa yeye ndiye anayeshauriana sana na hii bodi, ili waweze kukamilisha

haya majukumu ambayo tunayakusudia, *otherwise*, tukiibakisha kama ilivyo Mheshimiwa, bado yatabakia mambo ndio yale yale huku gesi hakuna, fedha zinatakiwa, mgonjwa yuko *ICU* wakati huduma haipo.

Sasa hili nilikuwa naomba fedha hizi zibakie katika hospitali ili waweze kutumia kwa ajili ya kuboresha huduma mbali mbali. Tunajua hospitali mambo yake mengi yanakuwa ni ya *emergency*. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, mimi namfahamu vizuri sana Mhe. Hamza Hassan Juma, na nimemuelewa nini anachokitetea hapa kwa ajili ya huduma nzuri kwa wananchi, wafanyakazi malipo yao, kada zao na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba nimrejeshe tena katika *good governance*. Hospitali inaweza kubakiza fedha kilichopatikana kutokana na malipo ya huduma ilizozitoa hiyo hospitali yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Pana tatizo la Kiswahili pia Mheshimiwa, nafikiri ushaliona.

Mhe. Waziri wa Afya: Nitasoma na *English* kidogo, kwa kiwango kitakachokubaliwa na waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha. Sasa hapa waziri mwenye dhamana hatutarajii kwamba Mnazi Mmoja itakuwa hivi hivi siku zote, siku moja pengine Mnazi Mmoja itatengeneza *sixty billion shillings* kwa mwaka, Mwenyezi Mungu mkubwa. Waziri wa Fedha ana dhamana ya *overall picture* ya *revenue* na *expenditure* ya serikali, yeye ndiye waziri dhamana na ninaamini mimi hata katika *system* yetu ya sasa hivi unaona inatolewa huku inatiwa huku, wakati mwengine kinapohitajika.

Kwa hiyo, wakati itakapozalisha fedha nyingi Mnazi Mmoja kiasi hicho, Waziri wa Fedha kwa kifungu hiki atakuwa na mamlaka ya kuweza kusema tuelekeze huku, lakini sasa hivi kwa hali tuliyo Waziri wa Fedha kwa kifungu hiki pia atakuwa na mamlaka ya kusema hicho chote mlichochukua bakieni nacho na chengine mimi nitakuongezeeni katika kile kifungu cha ruzuku ambacho nilishakitaja hapo awali.

Kwa hiyo, naomba sana tumuachie Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ana picha kamili ya serikali nzima ya *revenue* na *expenditure* na ninaamini atakuwa anapanga kiwango kizuri kilichokubalika. Lakini tuje kwenye ya Kiingereza kidogo, tuisome Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 23 kinasema kwamba:

"The Hospital may retain certain percentage of monies collected from the services rendered upon approval of the Minister responsible for Finance"

Kwa hiyo, kiko *very clear*. Sasa sijui hicho Kiswahili ulichosema Mwenyekiti, lakini mimi naona iko sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Kiswahili changu mimi *actually* sio *content*, yaani sio maudhui ya hiki kifungu ni *syntax error*, pana tatizo la Kiswahili kidogo hapa, "hospitali inaweza kubakiza fedha kilicho..."

Mhe. Waziri wa Afya: "...*retain"* kubakiza, imekusudiwa kiwango cha fedha, kubakiza kiwango cha fedha.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio hicho ambacho ninazungumza, yaani pana marekebisho kidogo hapo. Mhe. Hamza Hassan.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na huduma zinazotolewa hivi sasa na mapungufu yaliyokuwepo si rahisi sana kwamba hospitali ikusanye fedha nyingi sana ambazo zitakuwa hawana matumizi nazo, zikaendelea kubakia kwenye *account* na hilo ndilo lililokuwepo sasa hivi. Fedha nyingi zinakusanywa huduma huku zinasubiri fedha zitoke Wizara ya Fedha na Mipango, fedha zinakawia.

Mhe. Mwenyekiti, unajua kule mwanzo kwenye ile taifa nilikubali iondolewe na ndio maana nikasema basi huko mbele Mhe. Waziri na yeye aje atukubalie. Mhe. Mwenyekiti, hapa tunatengeneza sheria, tunatengeneza sheria ya kuboresha Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuelekea kwenye rufaa. Leo Mhe. Mwenyekiti, kila kitu hakuna, fedha zikiendelea kwenda Wizara ya Fedha halafu ziombwe tutawachosha wale madaktari, huyo Mwenyekiti wa Bodi anaweza akafika pahala akenda, akarudi kwa Mhe. Rais, akamwambia kwa mambo yenyewe yanavyokwenda aa, ingawa hatutegemei kama itakuwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwani hii tukiiachia kutakuwa kuna tatizo gani.Bodi haiwezi ikatumia fedha bila ya *consultation* na Mhe. Waziri, huyo Waziri wa Fedha ni waziri wa serikali, Waziri wa Afya ni waziri wa serikali. Sasa hapa kuna tatizo gani Mhe. Mwenyekiti, hebu kidogo naomba katika hili hii *retention* ya fedha mimi nafikiri iwe 100%. Ingawa kwenye Sheria ya Kiingereza imezungumza vizuri *certain percentage*. Sasa hiyo *certain percentage* mimi nataka iweko *clear,* iwe *hundred percentage retain in the Hospital of Mnazi Mmoja*.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, fedha nyingi ambazo za uendeshaji ukisoma sheria hii zinatoka serikalini, ukisoma kifungu cha 22 ambacho tumepitisha na ndio maana hii tukasema uwe wakala kwa serikali. Kwa sababu bado serikali itakuwa ina mkono mkubwa wa ku-*funds activity* ambazo zinahitajika kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, kama ambavyo Mhe. Waziri wa Afya, amesema na kama ambavyo Mhe. Hamza Hassan, anasema kwamba pamoja na yote hayo lakini pia kutakuwa kuna huduma ambazo zinatolewa na Mnazi Mmoja *Hospital*. Hoja ya Mhe. Hamza, ni kwamba hicho kinachokusanywa basi chote kibaki hapo hapo na Mhe. Hamza Hassan, yeye anajua ni mzoefu, kama Sheria ya *Public Finance* inaeleza kama mapato yote kwanza yaingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Sasa kuna sheria nyengine tunakubaliana tunasema 10% itakuwa *retained*, nyengine tunasema 5% itakuwa *retained*. Sasa mimi ningekubaliana na Mhe. Hamza, kama angeshauri hivyo ili tuanze hivyo kwanza, kuliko hayo ambayo anayotaka kushauri kama 100% ibakie kwenye Mnazi Mmoja *Hospital.* Kwa sababu kwanza hizo huduma zenyewe ambazo zinataka kutolewa hazijulikani zitakuwa ni huduma gani na hicho kiwango hakijulikani kitakuwa ni kiwango cha aina gani. Sasa bado matumizi makubwa ya Hospitali ya Mnazi Mmoja yatabaki kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Sasa mimi nimshauri Mhe. Hamza Hassan, kama yeye anaona hivi kilivyo hakisaidii basi tungekubaliana kwenye *percentage,* akasema basi angalau asilimia tano ya kinachokusanywa kibakie Hospitali ya Mnazi Mmoja kuliko hivi ambavyo anataka Mhe. Hamza. Hivyo, mimi nadhani tungekuwa *moderate*.

Mhe. Mwenyekiti: Anataka asilimia mia moja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, asilimia mia moja kama ambavyo nimesema kwa sababu ya sheria nyengine za fedha hatutoweza, lakini Sheria ya Fedha za Umma inaturuhusu kwamba kiasi fulani tunaweza tukataja kwenye sheria, tuseme basi angalau asilimia tano, asilimia mbili ibaki, lakini kilichobaki lazima kirudi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, yaani nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu Chuo alichosoma ndio hicho hicho nilichosoma mimi. Mhe. Mwenyekiti, amenielewa Mhe. Mwanasheria Mkuu, na ndio ile hoja

yangu niliyokuwa nikijaribu kuitetea, basi mimi nafikiri tukubaliane tu kwamba angalau asilimia 50 ya yale makusanyo yao, kwa sababu hiyo asilimia 50 yenyewe Mhe. Mwenyekiti, kuna *activities* nyingi sana pale. Hii sio taasisi ambayo labda tutasema ni ya uzalishaji, hii ni taasisi ya huduma na huduma nyingi za hospitali zinakuwa ni *emergency*.

Kwa hiyo, mimi ninashauri na kwa kuwa sasa hivi ndio tunajenga kuelekea katika hospitali ya rufaa, basi angalau *50 percentage* wai-*retain* ile *50 percentage* iende Wizara ya Fedha na bado tunashukuru kwamba fedha nyingi zinaendelea kutoka serikalini na kwa sababu kulikuwa hakuna sheria hii, sheria hii tukishaipitisha itaipa nguvu na uwezo Hospitali ya Mnazi Mmoja kuweza kukusanya fedha na kupunguza ile ruzuku inayotoka serikalini kuja katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naamini tukikubaliana asilimia 50 kwa 50, mimi nafikiri madaktari wetu watafanya kazi vizuri na wao watashukuru kwamba dah, leo Waheshimiwa kweli wamefanya kazi ya kutusaidia sana madaktari angalau tuweze kufanya kazi, lakini vile vile kuondokana na haya manung'uniko ya siku zote ya Waheshimiwa, tumekwenda pale hapana, gesi hapana, jenereta haliwaki. Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri tukubaliane katika hiyo asilimia, mimi napendekeza 50 na ninaamini Wajumbe wenzangu wataikubali, maana tukiumwa tunakwenda Mnazi Mmoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Pamoja na hayo makofi naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ili atupe neno.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, tumezisikia hoja za Mhe. Hamza Hassan, lakini kwanza nilitaka kusema tuangalie sera ya nchi yetu, kwanza sera ni huduma za afya bila ya malipo na hiyo toka mwaka 1964, hatutarajii kwamba hospitali hii itatengeneza fedha nyingi sana za kuweza kujiendesha wenyewe. Sasa kwa namna hiyo bado jukumu ni la serikali, bado jukumu ni la Mfuko Mkuu wa Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kuendesha hospitali hii.

Lakini pia tukitizama sera ya fedha nayo iko wazi, huwezi ukamuondolea jukumu waziri anayehusika na masuala ya fedha katika suala lolote la sekta. Hapa pia Mheshimiwa, juzi juzi tumepitisha *Finance Bill* ya mapato na matumizi na jukumu la usimamizi ni la Waziri wa Fedha, lakini hata ukikisoma hiki kifungu cha 24 hapa hapa chini kinasema hivyo, ukikisoma hichi kinasema; "Sheria ya fedha za serikali na sheria nyengine zinazohusiana na mambo ya fedha za serikali zitatumika kwa mambo yote ya fedha za hospitali".

Sasa mimi namshauri sana Mhe. Hamza Hassan Juma, akubaliane na hichi kifungu kama kilivyo na hii *retention* tutawasiliana, mamlaka hayo hapo na jukumu bado nalirudia kwamba jukumu la serikali la kuhakikisha kwamba hospitali ile inaendeshwa vizuri na huduma zinapatikana kwa wananchi, huo ndio wajibu wetu na ndio wajibu wa serikali hii na wakati mwengine zinatoka zaidi ya hiyo asilimia 50 ambayo Mhe. Hamza Hassan Juma, angeipendekeza ikawekwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa, nadhani sasa tunaendelea isipokuwa sasa nitaruhusu marekebisho ya *syntax* lile neno hili amelizidisha Mhe. Waziri, kwa hiyo, nitakihoji hichi kifungu. Mhe. Hamza Hassan Juma, nitakuwa nakupa mara ya nne hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, wala sikusudii kuendelea kuzuia hili fungu isipokuwa tu unajua tatizo tulilokuwa nalo kwamba sio sote tunakuwa sawa sawa. Na hii sheria tukishaipitisha hii leo kuwa Waziri mwema sana Dkt. Khalid Salum Mohamed, kesho atakuja waziri si mwema sana Mhe. Hamza Hassan Juma, Waziri wa Fedha huyo.(*Makofi*)

Sasa hili ndio tatizo, kwa hiyo, kama hatujawaekea kile kiwango cha *percentage* Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hilo tushawahi kusikia hicho kilio tunakwenda sisi pale tunawaambia jamani pesa hatuna. Tunajua kwamba serikali inatoa pesa nyingi sana na kwa sababu ndio wajibu wake. Lakini kwa kuwa tumeshapitisha hii sheria na kuna *certain amount* ambayo tunategemea kwamba zitaingia. Mimi nafikiri hiyo *percentage* kwa kuwa hii Sheria ya Kiingereza imeelekeza *certain percent,* mimi nafikiria hiyo *certain percent* tuweke *clear,* basi *at least* tuweke *certain percent* ya *amount* ya hizo fedha.

Lakini tukisema tuiache hivi hivi tu Mhe. Mwenyekiti, sasa hiyo *retention* yenyewe itakuwa haiko...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, ile *certain percent* mimi nadhani ni vizuri tuiache kama ilivyo kwa sababu inawezekana ni 100%, inaweza kuwa na maana ya 100% . Lakini inawezekana ikawa ina maana ya 10%. Lakini kutokana na hali ilivyo, nadhani tuache i-*hang* ili waweze kuamua sasa kwamba sasa hivi ipo haja, naomba tuendelee.

Kwa hiyo, ni kifungu cha 23 kile pamoja na marekebisho yale Mhe. Waziri, ambayo sasa ameyaleta kinakubaliwa.

Kifungu 24 Kutumika kwa Sheria ya Fedha

Kifungu 25 Kinga pamoja na marekebisho yake

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 25, kuhusu Kinga, hapa kilikuwa kinaeleza Mjumbe wa Bodi, maana yake ni mmoja, mfanyakazi ni mmoja au mtu mwengine yeyote ambaye anatoa huduma hospitali hatoweza kuwajibisha, ingawa ni kuwajipishwa pengine binafsi kwa kitendo, jambo au chochote alichokifanya kwa kuacha kufanya ikiwa alikifanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu yake chini ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hichi kifungu mimi nimeona kwa kisheria kama kinga ya daktari au mjumbe bado haijamkinga. Kwa sababu sijui sheria ipi tunayoenda nayo lakini mimi natizama haya mambo tunayofanya kwenye mahospitali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mgonjwa anakuwa hatibiwi kama hajapata *PF3*, wakati mgonjwa anakuja pale anavuja damu au ana kila kitu chake. Sasa hapa hatujaweka baadhi ya maendeleo, wala hatujaweka kifungu kidogo kwamba mgonjwa hata kama hajapata stakabadhi ya polisi bado anatibiwa. Kwa hiyo, mgonjwa anaweza akatibiwa akafa halafu haijapatikana stakabadhi.

Chengine ni kwamba tumezoea kufanya *operation*, lakini mgonjwa haelekezwi kuweka sahihi katika sehemu yake ya kwamba amekubali kufanyiwa *operation* au daktari gani atamfanyia *operation*...

Mhe. Mwenyekiti: Hii ya pili ni ipi sasa?

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hapana ni hii ambayo imo kinga Mhe. Mwenyekiti, maana yake sasa hivi unaambiwa wende ukafanyiwe *operation*, daktari gani hujui na wala hujaweka sahihi, umekubali au hukukubali. Lakini tunakuja kumkingia kifua kwamba alikuwa afe tu hapana, mimi mwenyewe sikuridhika. Kwa hivyo, kinga hapa ni ya daktari.

Lakini pia nilikuwa nazungumza Mjumbe mmoja wa Bodi. Mhe. Mwenyekiti, naweza kuamua mimi Mjumbe wa Bodi vunja hapa au fanya hapa, Wajumbe wa Bodi angalau watatu na sio mmoja. Kwa hivyo, hapa hichi kifungu kama kiwe na (a) kiongezwe kidogo kwa sababu *PF3* bado tuna sheria kwamba upewe. Lakini pia mgonjwa aweke sahihi ya ugonjwa kupasuliwa. Sio jambo dogo hilo anakwenda kufa, kupasuliwa tumbo mara unasikia daktari katoka mlango wa nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, hii wengine hatumpendi daktari fulani na pia tungepata kipimo cha daktari. Hili Mheshimiwa, lingeangaliwa na waziri kidogo au Mwanasheria Mkuu, maana yake ndio zake hizo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu Mhe. Suleiman Sarahan, ingawa hajenda kwenye ile hoja yenyewe hasa, hajatoa mapendekezo. Lakini kwa kuwa ni mtu wangu wa karibu sana mimi akizungumza namfahamu haraka sana.

La kwanza, ametoa mfano wa *PF3*. Mhe. Mwenyekiti, *PF3* ile ina sheria yake, pale daktari anakuwa analazimika kufuata sheria ile nyengine. Sasa kama kuna marekebisho yoyote sio kwenye sheria hii irekebishwe ile sheria ambayo imeitaja ile *PF3*. Kwa sababu vyenginevyo daktari atadhibitiwa kwa sheria ile *PF3,* kwa sababu daktari keshaambiwa katika mambo haya anaweza kuja mtu mwenye nia njema na akaja mtu mwenye nia mbaya, likaja jambazi limepigwa lenyewe risasi, lakini hana ile *PF3 form,* daktari atakuwa anatibu *criminal* bila ya kujijua anamtibu nani. Ndio maana ile *PF3* ina sheria yake. Kwa sababu marekebisho yale hayahusiani na sheria hii inabidi yarekebishwe kule.

Lakini ametaja mfano mwengine mzuri sana ya kwenda kwenye *operation,* yale ni mambo ambayo yanapangwa katika kanuni. Kwa sababu tusisahau kuna *medical board* ambayo inam-*regulate* daktari na *activities* zake, kuna *Medical council, Nursing council and Midwifery council* ambayo inam-*regulate Nursing* na *Midwifery*, yaani mkunga na muuguzi. Hizo Bodi zina wa-*regulate* na zina kanuni zao, kuna kanuni za maadili, kuna kanuni za kuwachukulia hatua, kuna kununi za nidhamu, kuna kanuni za kumnyanganya leseni daktari na kanuni hiyo aliyoitaja Mhe. Suleiman, iko huko, kuna fomu inaitwa '*consent* fomu' kabla haijaingia *theatre,* na ile fomu sheria hasa watu 3 wanasaini, moja wewe mwenyewe mgonjwa unatakiwa usaini.

Lakini mgonjwa unaweza kuwa hupo katika hali ya hadhiri kutokana na yale maradhi yako anakusainia mtu ambaye ni *next of kin to you,* aidha, mke, mama au baba ambaye yuko chini yake na mtu wa tatu ni shahidi mwengine ambaye anatakiwa kusaini. Sasa zile fomu zinatakiwa zisainiwe, lakini tunachosema hapa kwamba ile fomu imeshasainiwa hata mgonjwa ameshaingizwa *theater* ndani katika meza ile maamuzi yanakuwa juu ya meza na ndio hapo tunataka kumuondoshea, kwa sababu dhima ile ameshapewa kwa kiapo, kwa taaluma yake na kwa sheria, tunataka kumuondeshea dhima nyingine ya kumchukulia hatua kisheria kwa sababu daktari inabidi aamue pale kuokoa maisha ya yule mgonjwa wakati yuko mezani.

Kwa haya aliyoyaeleza Mhe. Suleiman Sarahan, nimeyafahamu lakini itakuwa mengi yanaingia kwenye kanuni hayawezi kuingia kwenye sheria, tutakuwa tunaishusha sheria chini zaidi kuanza kuingia kwenye kanuni. Ahsante, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, hapa kwanza moja ameliacha la huyu mjumbe mmoja wa Bodi. Lakini nasema tena mimi mwenyewe nimeshawahi kufanyiwa *operation* hapa na nimeshawahi kufanyiwa *operation* India.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipotiwa kwenye *theater* daktari wale walionipeleka walinipa mpaka yule anaenipiga sindano akasema *madam* huyu atakupiga hivi, ndio nikanyoosha mkono. Mhe. Mwenyekiti, hapa ukiingia *theater* watu wote wamejifunga kama ninja, wanakwambia kaa upande lete tukupasue. Sasa Mheshimiwa, mimi simkatalii lakini Mwanasheria hawa bwana ndio hawa hawa wanaokaa katika sehemu akakwambia wewe bwana *PF3*.

Mimi natetea kinga kwa daktari kwamba bado hatujamlinda, tunamlinda nje nje anasema kanuni kitu gani. Lakini za wazi kwa nini hatuzitoi, kama yeye amesema *PF3* si kosa lao, serikali si hii, anashitakiwa na serikali gani. Kwa hivyo, kama *PF3* ije baada ya mgonjwa kutibiwa iandikwe kifungu kidogo atatibiwa na *PF3* itafuata, akipasuliwa mgonjwa daktari awepo na amkubali, ndio tunapitisha Mheshimiwa, hapa. Sisi wenyewe ndio tutakaoingia *theater*, sawa Mheshimiwa, mimi nakubali hoja.

Kifungu 25	Kinga pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 26	Kuhaulisha Mali ya Madeni
Kifungu 27	Huduma bila ya Malipo pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 28	Kanuni

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia na kwa kuwa zipo sheria nyingi ambapo mawaziri hawazitungia kanuni na utekelezaji wake unakuwa mzito. Nikamuomba sana Mhe. Waziri, kifungu hichi cha 28 ambacho kinamtaka atunge kanuni namuomba sana. Kwa sababu pana lugha yao hapa ya kisheria wanayoitumia anaweza akatunga au laa.

Kwa hiyo, mimi naomba nikusisitize Mhe. Waziri, kwa sababu huu mswada ni muhimu sana kwetu na utungaji wa kanuni ndio utakaoufanya kuwepesisha hii sheria iweze kutumika vizuri. Sasa kama ulivyokuja mswada huu kwa hati za dharura basi na hizo kanuni ziwe nazo kidharura ili uweze kuzitunga haraka na ziweze kufanyakazi ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana namshukuru sana mama yetu Mhe. Panda Ali, naomba nimthibitishe kwamba *draft* ya kanuni tayari imeshatungwa na imetungwa kutokana na yale masharti ya Afrika Mashariki, *East African Community* na *Medical Education* ambayo ndio Bodi iliyoifanya hii ije chini ya hati hiyo ya dharura. Kwa hiyo, wale katika masharti yao wanataka kanuni ziweko tayari. Kwa hiyo, *draft* imeshatungwa na tunashawasilina na *ishaallah* itawasilishwa baada ya sheria hii.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 28 Kanuni.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wote *back benchers* na *front bench* kwa michango yao mbali mbali ya kuwatetea wananchi wa Zanzibar na ya kujenga.

Mhe. Spika, ilivyokuwa kamati ya kutunga sheria imeupitia mswada wangu wa Wizara ya Afya kifungu kwa kifungu juu ya Hospitali ya Mnazi mmoja na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswad wa Sheria ya Hospitali ya Mnazi mmoja ya Mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Hospital ya Mnazi mmoja ya mwaka 2016. Mswada huo usomwe tena kwa mara ya tatu, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Mswada wa sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapo ndio inakuwa mwisho wa huo utaratibu kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, sheria hiyo sasa itakwenda kukutana na Mhe. Rais, ambaye atahitajika sasa aisaini na baada ya hapo itakuwa ndio imeshapita kuwa sheria ambayo tumeipitisha hivi punde. (*Makofi*)

Kwa hiyo, napenda kutoa pongezi zangu za dhati sana kwa Mhe. Waziri, lakini kwa Waheshimiwa Wajumbe, pia kwa michango mbali mbali na uboreshaji ambao umependekezwa mpaka hapo tulipofikia.

Mswada wa Sheria wa kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kusomwa Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa Sheria Nam. 11 ya mwaka 2009 na kuweka masharti bora na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, ah, iko miwili?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Eeh.

Mhe. Spika: Sawa endelea.

Mswada ya Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, aidha, naomba kusomwa kwa mara ya kwanza Mswada ya Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Elimu, kwa kuwasilisha miswada hiyo miwili kwa kusomwa kwa mara ya kwanza. Sasa namuomba nimwete katibu kwa shughuli inayoendelea.

Mswada wa Sheria na Usimamizi wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia, kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na kuhakikisha uwajibikaji wa kampuni ya maendeleo ya mafuta na kuhakikisha uwajibikaji wa Taasisi za Mafuta na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Muongozo

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa heshima yako nilikuwa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu, atusaidie muongozo kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia masuala ya Ardhi ikiwemo na Nishati.

Lakini mswada tayari tumeshakabidhiwa na tayari umasomwa kwa mara ya kwanza, lakini bado sera hii hatujaiona na utaratibu wetu wa sasa hivi kawaida ile sheria inayotungwa inaongozwa na ile sera husika. Hili Mhe. Spika, nilijaribu kutoa angalizo kipindi kilichopita kwamba, Tanzania Bara wenzetu ile Sera ya Sheria ya Mafuta ilikuja kuleta tatizo kubwa sana kwa sababu ile sera Wabunge walipendekeza wananchi waione ili waweze kutoa mapendekezo yao watakuja kufaidika vipi na hiyo Nishati ya Mafuta na hiyo Gesi itakavyoweza kupatikana. Sasa inawezekana pengine kuna taratibu nyengine ambazo zinazoongoza.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka tu muongozo Mhe. Mwanasheria Mkuu, sasa hii sheria itakuwa inamashiko ya aina gani, wakati ile sera yake bado haijakuwepo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika Mhe. Hamza Hassan Juma, nimesikia muongozo wako, lakini ninadhani ngoja nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu, labda nimsikie kabla sijatoa kauli.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, na ninadhani Mhe. Hamza, anajua sheria inapotungwa ndiyo inakuwa na nguvu ya sheria. Na kilichowasilishwa hapa kusomwa kwa mara ya kwanza ni Mswada wa Sheria, pamoja na kwamba anasema kuna sera lakini sera haizuii kutungwa kwa sheria. Sasa kuletwa kwa Mswada huu na kutokuletwa kwa sera haina maana Baraza hili halina haki ya kujadili na kutunga sheria. Kwa sababu hiyo ndiyo kazi ya Baraza ya Kutunga Sheria.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza, apokee hicho ambacho amepewa kwa sababu kazi ya Kutunga Sheria ndiyo kazi ya Baraza na siyo kazi ya kutunga sera. Sera zinatayarishwa serikalini wala siyo Barazani. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu, labda na mimi niongezee tu kwamba hii Kusomwa kwa Mara ya Kwanza, maana yake Mswada huu utashughulikiwa katika Kikao kinachokuja haina maana kwamba ni kikao hichi ambacho kitashughulika na huu Mswada. Kwa hivyo, tuna muda mwingi humu ndani hapo kabla ya kuja kuwasilishwa na Mhe. Waziri, hoja yake hii. Hivyo, hapo katikati kuna mambo mengi yatajitokeza, Kamati zitakaa na kuna mambo yatafanyika. Kwa hivyo, siku ambayo atakuja kusoma Waziri, ninadhani tutakuwa tumeshafikia pahali ambapo sote tupo katika ukurasa mmoja. Nadhani matatizo kama haya kwa sababu wameshayasikia kabisa serikali, watakuwa wameshaweka sawa.

Na baada ya hapo kabla sijamwita tena Katibu kwa ajili shughuli inayofuata Waheshimiwa, nitoe kabisa tangazo. Munatangaziwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa CCM baada ya kumalizika kwa hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tuna kikao ambacho cha *caucus* cha Wajumbe wote wa CCM wa Baraza.

Baada ya hapo nimwite tena Katibu kwa shughuli inayoendelea.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa mara ya Kwanza)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti yaliyobora kuhusiana na mambo hayo, usomwe kwa mara ya kwanza.

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kufanikiwa vizuri kushiriki na kukamilisha Mkutano huu wa Pili wa Baraza la Tisa la Wawakilishi ulioanza tarehe 18 Mei, 2016, kwa lengo la kujadili Bajeti ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa uwezo wake Mola Mtukufu, kazi zote zilizopangwa katika ratiba ya mkutano huu wa pili tumezikamilisha kwa mafanikio mkubwa.

Mhe. Spika, shukrani maalum nazitoa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu katika hali ya amani na utulivu.Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uwezo, hekima na busara ili aendelee kuiongoza na kuzidi kuiletea maendeleo nchi yetu katika kipindi hiki cha pili cha uongozi wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti na wasaidizi wako wote kwa kukusaidia kuliendesha Baraza hili Tukufu kwa umahiri na umakini mkubwa. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Kudumu za Baraza hili kwa michango, ushauri na maelekezo yao kwa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu la Tisa la Wawakilishi, Mawaziri, na Naibu Mawaziri kwa umahiri wao mkubwa katika kuchangia mijadala na hoja mbali mbali ndani ya Baraza hili. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa mafanikio makubwa.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nachukua pia fursa hii kuelezea kuridhika kwangu na upeo na uelewa mkubwa walionao Waheshimiwa Wawakilishi, kwa jinsi walivyotoa michango ya kujenga na sio ya kubomoa, kushutumiana au kukomoana. Nawapongeza sana kwa uelewa na ukomavu wao kisiasa na jamii kubwa ya Wazanzibari na wengine wanajifunza kwa utendaji wetu vipi kiongozi anapaswa kuwa hasa anapojadili masuala ya wananchi. Katika kuchangia hoja mbali mbali za Serikali, wapo waliochangia kwa hamasa, wapo waliochangia kwa upole, wapo waliochangia kwa jazba na hata kulia, lakini wote hao nia yao ni kuikosoa na kuishauri Serikali ili ifanye kazi zake kwa usahihi zaidi.*(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nimeona dalili ya baadhi yetu kutetea mambo ya kibinafsi kuliko yale ya wananchi walio wengi, hili naomba tuliache, tuwasilishe katika chombo chetu hichi mambo ambayo wananchi yanawagusa na ambayo wametutuma tuje kuyatetea, tupite kwa wananchi tujadiliane nao na mnachokubaliana nao ndicho tukiwasilishe katika Baraza hili Tukufu. Haitokuwa vyema tukaongea vitu ambavyo tukirudi Majimboni kwetu wananchi wakatueleza kuwa yale uliyokuwa unaongea Barazani sio shida zetu au sio tuliyoyapa kipaumbele.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi, wajitahidi kuwatumikia wananchi wao kwa nguvu zao zote na hasa wale walioshinda katika Majimbo ambayo kipindi cha nyuma yakishikiliwa na Wawakilishi wa Chama cha Upinzani, ambao wengi wao hawakuwa wanawaletea maendeleo wananchi wao, ambao wengi wao walihama katika Majimbo yao na kukimbilia mijini. Na baadhi yao kutoka Majimbo ya Pemba walikimbilia na kuhamia Unguja. Wananchi wa Majimbo hayo walikata tamaa na sasa nakuombeni sana mkae na wananchi hao na kuwarejeshea matumaini na pia waweze kuona faida ya kuwa na Wawakilishi kutoka CCM.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nitoe mwito maalum kwa Waheshimiwa Wawakilishi, kutenga muda wa kutosha kuzisoma hotuba za bajeti na miswada inayowasilishwa na michango yetu ikakita katika vitabu au nyaraka zilizowasilishwa kwa kufanya rejea ya maeneo hayo na kushauri nini kifanyike. Baadhi yetu tumeonekana kusikiliza msemaji aliyepita na kurejea yale yale hata kama hayamo katika hotuba inayojadiliwa, si vibaya kurejea au kuzungumza jambo ambalo halikutajwa katika hotuba husika mradi ina nia ya kujenga au kuondoa kero fulani inayowasumbua wananchi wetu hata wageni wanaotembelea nchi yetu.

Mhe. Spika, nimelazimika kutoa ushauri huu baada ya kuona wachache kati yetu wamekuwa wakitoa michango ambayo iko nje ya suala la msingi linazungumzwa au wanauliza kitu ambacho majibu yake yamo katika hotuba inayojadiliwa. Tukisoma kwa makini na kuchangia baada ya kukielewa kilichowasilishwa tutaongeza ufanisi wa shughuli zetu kuokoa muda ambao tungeweza kuutumia kwa shughuli nyengine za Baraza letu Tukufu. Aidha, wananchi wetu wanafuatilia kwa makini sana kinachowasilishwa na michango yetu na nimekuwa nikipokea maoni ya wananchi kuwa baadhi yetu tunatoka sana nje ya mada za msingi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuunda Baraza la Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri lenye watu imara, mahiri, wenye ari ya kufanya kazi na wanaowajibika ipasavyo. Kazi yangu katika Baraza lako Tukufu imekuwa nyepesi kutokana na utendaji wao mzuri. Napenda kuwapongeza Mawaziri hao na Manaibu wao kwa kazi nzuri wanayoifanya Barazani na kwenye Wizara zao.(*Makofi*)

Mhe. Spika, Mawaziri na Naibu Mawaziri wengi wana muda mchache katika ofisi zao, lakini kwa kipindi kifupi sana wameweza kuzielewa kazi zao na changamoto zinazowakabili. Kinachonipa faraja zaidi ni kuwa hoja za Waheshimiwa Wawakilishi, zimeweza kujibiwa kwa usahihi na umakini mkubwa sana, nakupongezeni sana.(*Makofi*)

Mhe.Spika, naomba pia nipongeze mashirikiano ambayo yapo baina ya Waheshimiwa Wawakilishi na Mawaziri, hali inayopelekea kila changamoto inayojitokeza kupatiwa ufumbuzi kwa mashirikiano, huku ndiko kujenga nchi. Hatuwezi kupiga hatua ikiwa hatuna mshikamano na mashirikiano katika ujenzi wa nchi yetu. Siasa chafu kama zinazofanywa na Wapinzani zinalenga kuipaka rangi ya ubaya nchi yetu na viongozi wake zimepitwa na wakati na tusiruhusu sasa siasa uchwara kuenea nchini mwetu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kama nilivyokupongeza hapo awali, naomba niendelee kukupongeza na kutambua usimamizi wako wa chombo hiki kikubwa katika nchi yetu. Wewe mwenyewe binafsi, Naibu wako na Wenyeviti mmefanya kazi kubwa na ya weledi mkubwa sana, kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi, kuna changamoto nyingi ikiwamo kuzielewa Kanuni na Taratibu za Baraza hasa inapotokea mitazamo tofauti juu ya hoja au suala linalojadiliwa. Ninachoweza kusema ni kuwa chombo kimepata manahodha wanaokijua, wanaojua tunakoelekea na changamoto za kufikia tunakokwenda, hongereni sana Mhe. Spika.

TAARIFA YA MAMBO MBALI MBALI:

(i) HALI YA KISIASA

Mhe. Spika, baada ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia Mwenyekiti wake, kufuta matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015 kufuatia kubainika kwa kasoro nyingi ambazo zingeyafanya matokeo hayo kutokuwa ya uhuru na haki, Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Hamad amekuwa akipita maeneo mbali mbali kuwadanganya wananchi hasa wanachama wa chama chake na Jumuiya za Kimataifa kwamba, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, alitoa amri kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchanguzi Zanzibar, Mhe. Jecha Salum Jecha, kufuta matokeo hayo, jambo ambalo sio la kweli, na kauli hiyo ilikuwa kama tusi kwa Dk. Shein, maana amemaanisha kuwa kama Dkt. Kikwete asingemwamuru Mhe. Jecha Salum Jecha, kufuta uchaguzi, Dkt. Shein angekubali kudhulumiwa. Hii ni porojo tu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda ieleweke kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni chombo huru chenye mamlaka na kinafanya kazi zake bila ya kuingiliwa na mtu au chombo kingine chochote. Maamuzi ya kufuta matokeo hayo yalikuwa ni halali baada ya kubainika kwa kasoro nyingi, ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni za uchaguzi hasa Kisiwani Pemba. Tume ya Uchaguzi inafanya kazi zake ili kusimamia haki na kuhakikisha matakwa na ridhaa za wananchi katika kuwachagua viongozi wanaowataka zinatimia bila ghilba na udanganyifu wowote.

(ii) ZIARA ZA MAALIM SEIF SHARIF HAMAD

Mhe. Spika, tokea kumalizika kwa uchaguzi wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016 na CCM kupata ushindi wa kishindo, Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, pamoja na viongozi wengine wa chama hicho wamekuwa wakifanya ziara mbali mbali ndani na nje ya nchi. Serikali imezifuatilia kwa karibu ziara hizo na kubaini kwamba msingi wake ni kutapatapa kwa kiongozi huyu baada ya kushindwa uchaguzi huo wa marejeo. Ziara hizo zimekuwa ni muendelezo wa vitendo vya uchochezi na hujuma, kwani anayoyasema wakati wa ziara hizo yanaongeza chuki na uhasama miongoni mwa wananchi wa Zanzibar. Tunayaona au kuyasikia yanayotokea huko Pemba hivi sasa.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nawaomba wananchi wasibabaishwe na kauli hizo za Katibu Mkuu wa CUF kwani haziwezi hata kidogo kuiteteresha Serikali halali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi iliyowekwa madarakani na wananchi wa Zanzibar

katika uchaguzi wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016. Wala kauli zao hizo haziwezi kututoa kwenye malengo yetu ya kuwaletea wananchi maendeleo.Uchaguzi huo aliukataa yeye mwenyewe na kilichobakia ni kusubiri uchaguzi mwengine hapo mwaka 2020 panapo majaaliwa. Huko nchi za nje nako alisikika akidai kuundwa kwa Serikali ya Mpito ya miezi sita itakayoongozwa na Mzanzibari asiyefungamana na upande wowote wa kisiasa, Zanzibar na baada ya hapo uitishwe Uchaguzi Mkuu utakaosimamiwa na Jumuiya au Taasisi ya Kimataifa. Huu ni upuuzi mwingine kwani jambo hilo haliwezekani kutokea hata siku moja. Tunachojua sisi ni kuwa uchaguzi umekwisha, uchaguzi mwingine hadi 2020. Kabla ya hapo hakuna Serikali ya Mpito wala ya Mpeta. Hapa ni Kazi tu ya kuwatumikia wananchi ya kuzitatua kero zao na kutekeleza ahadi tulizozitoa kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 – 2020.(*Makofi*)

(iii) MATUKIO YA UHALIFU NA HUJUMA

Mhe. Spika, nchi yetu imeshuhudia matukio mbali mbali ya uhalifu na hujuma yanayopangwa na kutekelezwa na baadhi ya wafuasi wa Chama cha Upinzani cha CUF wasioitakia mema nchi yetu, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya viongozi wao ambao wana nia ya kuhatarisha hali ya amani na utulivu uliopo. Matukio hayo yamejitokeza kabla na baada ya uchaguzi wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016, ikiwemo uchomaji moto nyumba, ofisi za CCM na vituo vya afya; wananchi kunyimwa au kubaguliwa kwenye huduma za kijamii; na kukata na kuharibu mikarafuu na mazao mengine, ikiwemo mpunga, muhogo, migomba na vipando vingine.

Mhe. Spika, Serikali inasikitishwa sana na matukio hayo, ambayo sio tu yanaathiri wananchi walengwa, bali pia yanaleta athari kubwa za kimazingira kutokana na uharibifu mkubwa wa miti ya mikarafuu na mazao mengine. Wanaofanya vitendo hivi ni wahujumu uchumi na watakaopatikana ni bora kushitakiwa chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi Zanzibar unaonyesha kwamba Chama cha CUF kimekuwa na mpango wa kuendeleza hujuma hizo katika maeneo mbali mbali, ikiwemo nyumba za Viongozi Waandamizi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi. Kwa mujibu wa uchunguzi huo, vitendo hivi vinatokana na maelekezo ya Chama cha CUF yaliyotolewa na Katibu Mkuu wao. Aidha, upo ushahidi wa kutosha kwamba Katibu Mkuu huyo amekuwa akitoa hotuba za uchochezi kupitia mikutano yake ya ndani aliyoifanya katika maeneo mbali mbali, hasa Kisiwani Pemba. Serikali inakamilisha taratibu za kuwachukulia hatua za kisheria wale wote waliohusika

na vitendo hivyo. Wasije wakailalamikia Serikali kwa hatua itakazochukua. *(Makofi)*

Nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa pole kwa wananchi wa Pemba, kwa madhila waliyoyapata ya kuharibiwa na kuchomewa nyumba zao, kukatiwa vipando vyao mbali mbali na kubaguliwa, serikali iko pamoja nao. Serikali itawashughulikia wahalifu hao vipasavyo. *(Makofi)*

(iv) MARADHI YA KIPINDUPINDU

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kuwa nchi yetu bado imekabiliwa na maradhi ya Kipindupindu katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kuanzia Septemba, 2015 hadi kufikia katikati ya mwezi wa Juni, 2016, jumla ya wagonjwa 4,242 (Unguja 2,608 na Pemba 1,624) walilazwa katika vituo vilivyotengwa vya Unguja na Pemba, na kati ya hao, watu 68 wamefariki dunia (Unguja 49 na Pemba 19 mpaka sasa). Serikali, imeendelea kuchukua hatua mbali mbali za kukabiliana na maradhi haya zikiwemo utoaji wa elimu ya kujikinga na maambukizi ya maradhi hayo. Serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi kutokufanya biashara za vyakula vya maji maji katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mhe. Spika, kutokana na kupungua kwa kasi ya maradhi ya Kipindupindu na kwa kuzingatia mahitaji ya huduma za chakula katika mikahawa, serikali kupitia Wizara ya Afya imeamua kuzifanyia ukaguzi sehemu za kuuzia vyakula na kuruhusu baadhi ya sehemu hizo baada ya kukidhi vigezo vya afya. Nachukua fursa hii kuzitaka sehemu zilizoruhusiwa kutoa huduma ya chakula kuendelea kuweka usafi na kuzingatia masharti ya afya katika sehemu zao, na kwa wale ambao sehemu zao hazijaruhusiwa wahakikishe kuwa sehemu hizo zinakuwa safi ili kukidhi vigezo vya afya.

(v) UTOAJI WA PENSHENI KWA WAZEE

Mhe. Spika, hivi karibuni, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed, kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, alizindua Mpango wa Utoaji wa Pensheni kwa Wazee hapa Zanzibar. Chini ya Mpango huo, Serikali hadi sasa imeorodhesha wazee 21,750 wenye umri wa miaka 70 na kuendelea na kutoa pensheni kwa wazee hao kwa awamu mbili za malipo. Zaidi ya Shilingi Milioni 400 zinatumika kulipia pensheni hizo za wazee kwa kila mwezi. Nachukua fursa hii kukumbusha agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi kwamba, watendaji wanaohusika na pensheni hizo, wawe makini na waadilifu katika kuwabaini, kuwafikia na kuwahudumia wazee hao. Vyenginevyo, serikali haitasita kuwachukulia hatua kali watendaji watakaoharibu mpango huo wa serikali.

(vi) KUWAENDELEZA WAJASIRIAMALI

Mhe. Spika, katika jitahada za kuwaendeleza wajasiriamali, serikali imekifungua rasmi Kituo cha Kulelea na Kukuza Wajasiriamali kilichopo Mbweni. Kituo hiki kimeweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 815 wa Unguja na Pemba, ambao wengi kati yao wameweza kujiajiri kupitia miradi midogo midogo, na hivyo kujiongezea kipato. Nachukua fursa hii, kuwashajihisha vijana wa kike na kiume kujiunga na kukitumia kituo hiki ili kupata taaluma na ujuzi wa uzalishaji na kuendesha biashara kwa faida na tija. Ni mategemo ya serikali kwamba kituo hiki kitakuwa ni msaada mkubwa kwa vijana wetu katika kusaidia kutatua tatizo la ajira.

(vii) USIMAMIZI WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU

Mhe. Spika, upatikanaji wa bidhaa muhimu za chakula, ikiwemo mchele, sukari na unga wa ngano umekuwa wa kuridhisha hapa nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba hadi kufikia Machi 2016, jumla ya tani 72,535 za mchele, tani 16,322 za sukari na tani 29,472 za unga wa ngano zimekidhi mahitaji ya matumizi ya soko la ndani. Mwenendo wa bei za bidhaa hizo uliendelea kuwa ya utulivu (*stable*) kutokana na serikali kuendelea kuchukua hatua za kisera za kusimamia bei za bidhaa muhimu kwa kushirikiana na wafanya biashara. Nachukua fursa hii kutoa shukrani kwa wafanyabiashara kwa kuzingatia maelekezo ya kisera na hali za wananchi katika kutoa huduma hizo za bidhaa muhimu.

(viii) TATIZO LA AJIRA KWA WATOTO

Mhe. Spika, suala la kuwepo kwa ajira kwa watoto hapa Zanzibar bado ni kubwa na serikali inaendelea na jitihada za kulikomesha tatizo hili, ili kuendana na sera na miongozo ya Kimataifa juu ya kuondokana na tatizo hili. Serikali tayari imezisaidia familia masikini 1,500 katika Wilaya zote 11 za Unguja na Pemba ambazo imegundulika kwamba watoto wao wanajishughulisha na kazi mbali mbali za kujipatia kipato. Jumla ya watoto 5,067 kutoka familia hizo ambao walitoroka skuli tayari wamerejeshwa kuendelea na masomo yao badala ya kufanya kazi. Aidha, jumla ya familia 1,065 zimepatiwa sare za skuli kwa

watoto wao pamoja na vifaa vya kuanzishia miradi ya kiuchumi vikiwemo mafriji na mifugo.

Mhe. Spika, kutokana na tatizo hilo la ajira kwa watoto kuwa kubwa, nawasihi wazazi kuacha kabisa kuwatumikisha watoto katika kazi mbali mbali na hasa zile hatarishi kwa kisingizio cha kujiongezea kipato cha familia zao. Bado familia zina jukumu kubwa la kuhakikisha watoto wao wanapata haki zao za msingi, ikiwemo elimu na malezi bora ili kuwajengea mazingira mazuri ya maisha yao ya baadae.

(ix) UDHALILISHAJI WA WANAWAKE, WATOTO NA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji na ukatili kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu bado ni tatizo sugu hapa nchini. Kwa upande mmoja, tatizo hili limekuwa likichangiwa na migogoro ya kifamilia, na kwa upande mwengine linatokana na ucheleweshaji wa taratibu za kushughulikia tuhuma za vitendo vya udhalilishaji na ukatili katika vyombo husika. Nachukua nafasi hii kutoa wito kwa wananchi kujiepusha na migogoro ya kifamilia, na iwapo ikitokea waitatue kupitia vyombo vinavyohusika.

Aidha, navitaka vyombo vyetu vya sheria kuchukua hatua za haraka katika kushughulikia malalamiko na kesi zinazohusu udhalilishaji na ukatilii kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu. Malalamiko makubwa ya wananchi ni kwamba vyombo vya Sheria, havichukui hatua madhubuti za kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia, na wakati mwingine hazishughulikiwi kabisa hata kama ushahidi utakuwa wazi kiasi gani. Naviomba vyombo vya Sheria vichukue hatua za haraka kuwashughulikia wale wote watakaohusika na kesi za aina hii. Kushughulikiwa kesi hizi kwa haraka kutaepusha watu kuchukua sheria mikononi mwao. *(Makofi)*

(x) USHIRIKI WA ZANZIBAR KATIKA JUMUIYA ZA KIKANDA NA KIMATAIFA:

Mhe. Spika, kwa suala la ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha kuwa inawakilishwa vizuri katika mikutano inayoandaliwa na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Mikutano hiyo itawahusisha Maofisa kutoka katika sekta mbali mbali za serikali. Madhumuni ya mikutano hii ni kuiwezesha Zanzibar kunufaika na fursa zinazopatikana kwenye Jumuiya hizo pamoja na kujenga mahusiano mema na nchi wanachama.

(xi) USHIRIKIANO NA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI:

Mhe. Spika, kuhusu suala la ushirikiano wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi au Diaspora, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuwashirikisha Wanadiaspora wa Zanzibar kushiriki maendeleo ya nchi yao. Katika kufanikisha hilo, serikali itahakikisha kuwa Sera ya Diaspora inamalizika na kuanza kutumika. Sera hii itaweka miongozo sahihi na mazingira rafiki yatakayowawezesha Wana-Diaspora wa Zanzibar kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Zanzibar. Aidha, katika mwezi Agosti 2016, serikali itaandaa kongamano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi hapa Zanzibar. *(Makofi)*

(xii) SEKTA YA ARDHI

Mhe. Spika, katika sekta hii, serikali itafanikisha kazi za kutayarisha Hati Miliki 1,350 na Vitambulisho vya Umiliki Ardhi za Eka Tatu 60, kutayarisha Mikataba ya ukodishaji ardhi 130, kuingiza taarifa za ardhi katika mfumo wa komputa sawa na hati za mikataba itakayotayarishwa, kukagua maeneo yote yatakayohitajika kutayarishiwa Mikataba ya Uekezaji na maeneo ya kilimo (Eka Tatu), pamoja na kufanya utambuzi wa maeneo 6,000 kwa Shehia za Unguja na Pemba mijini na vijijini.

Mhe. Spika, vile vile, serikali itaendelea kuhimiza matumizi bora na endelevu ya ardhi na kuendelea kupanga miji midogo ya Zanzibar kwa kupanga matumizi ya ardhi ya miji miwili midogo, mji wa Wete huko (Pemba) na mji wa Makunduchi hapa (Unguja), sambamba na kufanya mapitio ya mpango wa maendeleo ya utalii, katika eneo la Pwani ya Mashariki kutoka Chwaka mpaka Nungwi.

(xiii) MIGOGORO YA ARDHI

Mhe. Spika, bado migogoro ya ardhi imekuwa changamoto kubwa kwa serikali yetu. Hii ni kwa sababu ya wananchi wetu hawataki kuheshimu Sheria ya Ardhi ndiyo maana kila siku migogoro ya ardhi inaibuka. Kuimaliza migogoro hii, naiomba Mahakama ya Ardhi kuzishughulikia kesi za migogoro ya ardhi kwa haraka iwezekanavyo.

(xiv) SEKTA ZA HABARI NA MICHEZO

Mhe. Spika, katika sekta ya habari, serikali imo mbioni kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari kilichopo Kilimani ili kiweze kupokea idadi kubwa ya wanafunzi katika fani ya habari, ambapo Chuo kitaongeza madarasa matano (5) na kutoa fursa kwa wanafunzi wengi kujiunga katika chuo hicho.Ujenzi utakapomalizika, Chuo kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 304 kwa mwaka, ikilinganishwa na idadi ya sasa ya wanafunzi 204 kwa mwaka. Aidha, kutaanzishwa kozi nyengine mpya za masomo zikiwemo Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia (*International Relations & Diplomacy), Language & Interpretation, Language Art of Public Speaking, Graphic Design na Chinese Language & Chinese Culture*. Hivyo, Chuo kitaweza kukuza na kuongeza upatikanaji wa habari kwa ufasaha na kukuza ajira kwa wanahabari.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya michezo, nchi yetu imeshuhudia migogoro mbali mbali hasa katika mpira wa miguu. Migogoro hii inaathiri sana ukuaji wa michezo kwa namna moja ama nyengine nchini. Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa michezo, inaendelea kuchukua hatua za utatuzi wa migogoro hiyo, ili kuendeleza sekta ya michezo na kuleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, serikali imekusudia kujenga na kuviendeleza viwanja mbali mbali vya michezo ili kuwawezesha vijana wetu kupata fursa ya kushiriki na kukuza vipaji vyao vya michezo. Katika kulitekeleza hili, jumla ya viwanja tisa vikiwemo Gombani, Mao-Tse-Tung, Tibirinzi, Nungwi na Matumbaku tayari vimeshapimwa na vinasubiri kuanza kwa ujenzi. Viwanja hivi vikikamilika kujengwa vitasaidia kuimarisha michezo nchini. *(Makofi)*

(xv) SEKTA YA KILIMO

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, serikali itaweka mkazo zaidi katika kuimarisha uzalishaji na tija katika kilimo kwa kushajiisha matumizi ya teknolojia za umwagiliaji maji, kushajiisha ufugaji wa kibiashara wa kuku na ng'ombe wa maziwa, kuimarisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, na katika viwanda vya kusarifu matunda, samaki na mwani pamoja na kuwaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, suala la usimamizi wa rasilimali zetu ni muhimu sana. Serikali itaendelea kupiga vita uvuvi haramu kwa kuimarisha mfumo wa doria pamoja

na kuandaa utaratibu wa kuwapatia wavuvi wadogo wadogo zana bora za uvuvi. Aidha, serikali itaendelea kudhibiti wimbi la uvamizi wa maeneo yote ya kilimo, misitu na mifugo ambayo katika siku za hivi karibuni uvamizi huu umeongezeka sana kwa watu kukata miti ovyo na kujenga katika maeneo yenye rutuba, hasa katika mabonde ya mpunga na katika maeneo ya hifadhi ya misitu na kuchimba mchanga katika mashamba yanayofaa kwa kilimo. Nachukua fursa hii kuwataka wale wote wanaojishughulisha na vitendo hivyo vya kuharibu rasilimali zetu, waache mara moja tabia hiyo, vyenginevyo, serikali itawachukulia hatua za kisheria mara moja. Aidha, serikali itaendelea na utoaji wa miche ya mikarafuu bila ya malipo na kuhakikisha kuwa pembejeo muhimu za kilimo, ikiwemo mbolea, mbegu na madawa ya kuulia magugu yanapatikana kwa wakati na kwa wingi unaohitajika, ili kuweza kuleta mabadiliko ya tija na uzalishaji kwa kilimo cha mpunga.

(xvi) SEKTA YA NYUMBA NA MAKAAZI

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Nyumba na Makaazi, serikali kupitia Shirika la Nyumba la Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji itaendelea kuimarisha huduma bora za makaazi kwa wananchi wote kwa kuendeleza miradi ya kuwapatia wananchi makaazi bora, salama na ya kisasa na yenye gharama nafuu. Matarajio makubwa ya serikali ni kutatua tatizo la makaazi kwa wananchi hapa Zanzibar.

(xvii) UIMARISHAJI WA SEKTA YA ELIMU

Mhe. Spika, katika kuimarisha sekta ya elimu nchini serikali imo katika hatua za kutayarisha mpango mkuu wa miaka mitano 2016 hadi 2020 ambao utakuwa dira ya elimu kwa kipindi hicho katika ngazi za maandalizi, msingi, sekondari na vyuo. Kupitia mpango huo changamoto zote za msingi zinazoikabili sekta ya elimu kama vile, upungufu wa madawati, madarasa, maabara na maktaba pamoja na miundombinu na vifaa vyengine zinapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, suala la mchango wa madawati ya wanafunzi limezungumzwa sana katika vikao hivi vya Baraza lako tukufu. Serikali ilikuwa ikitoa fedha kupitia makusanyo ya Kodi ya Bandari kwa ajili ya kununulia madawati ili kupunguza tatizo la vikalio katika skuli zetu. Mchango huu ulianza kutolewa katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Jumla ya TZS 3,452,662,465.00 zilipatikana kupitia kodi hiyo ya bandari katika kipindi cha miaka minne, na hadi kufikia mwaka 2015/2016, jumla ya Madawati 4,285, Viti 3,706 na Meza 3,704 yalinunuliwa kwa kutumia fedha hizi na kusambazwa katika skuli za Unguja na Pemba na yanatumika kwa ajili ya wanafunzi na walimu wetu.

Niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi, kutumia alau sehemu ndogo ya mifuko yao ya Majimbo kusaidia kupunguza matatizo hayo, hasa upungufu wa madawati kwenye skuli zilizoko ndani ya Majimbo yao.

MAMBO MUHIMU YALIOJITOKEZA BARAZANI

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa pili, Baraza lako tukufu lilikamilisha mambo makuu tisa (9) yafuatayo:-

(a) Kujibu maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

(b) Limepokea na kujadili Hotuba ya Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa 2016/2017.

(c) Limepokea na kujadili Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa fedha 2016/2017.

(d) Limepokea na kujadili Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali na Mashirika.

(e) Limepokea na kujadili Mswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) na Uchaguzi wa Wabunge watano kuliwakilisha Baraza letu tukufu.

(f) Limefanya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza na Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi.

(g) Limepokea, kujadili na kupitisha Hotuba za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara za SMZ kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

(h) Limepokea na kujadili Mswada wa Sheria ya Matumizi.

(i) Limepokea na kujadili Mswada wa Dharura wa Sheria ya kuanzisha Hospitali ya Mnazi Mmoja.
Nia ya sheria hii pamoja na mambo mengine, ni kuipandisha daraja hospitali hii, ili kuzifanya huduma zinazotolewa na hospitali hii kuwa bora zaidi.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu jumla ya maswali ya msingi 85 na maswali ya nyongeza 246 yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta husika. Nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walioiuliza maswali ya msingi na ya nyongeza ambayo yalikuwa na lengo la kudadisi utekelezaji na ufanisi wa shughuli za Serikali. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, kwa kutoa majibu sahihi ambayo yamewajengea uelewa Waheshimiwa Wawakilishi, pamoja na wananchi kwa jumla. Kwa dhati kabisa, napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wapya ambao walijibu maswali katika Baraza hili kwa mara ya kwanza na kujibu vizuri sana kwa umakini na kwa kujiamini.

Mhe. Spika, kuhusiana na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar, Serikali imepanga kutumia Mkakati mpya wa maendeleo ambao unakusudia kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa kuimarisha uchumi endelevu na kuimarisha ubora wa huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya, mazingira endelevu na misingi ya utawala bora.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 maeneo yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar yameainishwa na kufafanuliwa vyema katika hotuba ya Serikali iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. mwanzoni mwa kikao cha kwanza cha Mkutano wa Pili wa Baraza hili la Tisa. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wake mkubwa katika kuendeleza uchumi wetu na kuimarisha huduma za jamii na utawala bora kwa jumla, naomba nichukuwe fursa hii kukumbusha tena maeneo hayo ya kipaumbele tuliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

1. Kuendeleza miundombinu ya msingi ya barabara, bandari, viwanja vya ndege na nishati.
2. Kuendeleza Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (R4P).
3. Kuimarisha huduma za kijamii hasa elimu, afya na maji.
4. Kuimarisha kilimo.
5. Kuimarisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya kati.
6. Kuendeleza Programu za Kukuza Ajira kwa Vijana.
7. Kuongeza juhudi ya kutunza mazingira dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kitaifa na kijamii kwa jumla.
8. Kufanya tafiti katika sekta mbali mbali.
9. Kuimarisha misingi ya utawala bora na sheria.

Mhe. Spika, ni wajibu wa Taasisi zote za Serikali kuhakikisha kuwa mipango na programu zao zinaendana na utekelezaji wa malengo haya makuu ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. Aidha, mipango ya muda wa kati hadi kufikia mwaka 2020 haina budi kuendana na malengo ya Mkakati mpya wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2016 – 2020. Kwa mnasaba huu, Taasisi zote za Serikali ni vyema zikaandaa utaratibu wa haraka wa kufanya mapitio ya mipango mikakati yao *Strategic Plans* ili kuoana na mpango mkuu wa Serikali unaochukua nafasi ya MKUZA II ambao unamalizika muda wake mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2016.

Mhe. Spika, mkutano huu pia umepokea na kujadili na kupitisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Jumla ya fedha TShs: Bilioni 841,477,500 zimepitishwa. Kati ya hizo, TShs: Bilioni 445.6 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na TShs: Bilioni 395.9 kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kuipitisha Bajeti hiyo kwa kauli moja.

Mhe. Spika, ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali na Mashirika imewasilishwa Barazani na itajadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika vikao vijavyo vya Baraza.

Mhe. Spika, mkutano huu pia ulijadili na kupitisha Hotuba za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara zote 13 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Mawaziri watasimamia kwa umakini utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika programu na programu ndogo za Wizara hizo. Aidha, Waheshimiwa Mawaziri, wajitahidi kuzitekeleza ahadi walizozitoa Barazani hapa.

Mhe. Spika, katika mkutano huu Wajumbe pia walipata fursa ya kuwachagua Wajumbe watano wa Baraza hili watakaotuwakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Wajumbe hao waliochaguliwa ni Mheshimiwa Machano Othman Said, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub na Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu. Kwa mara nyengine tena nawapongeza kwa uchaguzi huo na pia nawaomba watuwakilishe vyema katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa Baraza lako Tukufu, Waheshimiwa Wajumbe, walipata fursa ya kujadili mambo mbali mbali muhimu kwa Taifa letu. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na ukusanyaji wa mapato kupitia Halmashauri na Manispaa, kuimarisha ulinzi katika bandari bubu zisizo rasmi, uimarishaji wa Shirika la Utangazaji Zanzibar *ZBC*, utatuzi wa migogoro katika michezo, uvuvi wa bahari kuu, pembejeo za kilimo kwa wakulima, vifaa vya kukabiliana na maafa, uimarishaji wa makaazi ya Viongozi wa Kitaifa na suala la wafanyakazi hewa kwa kutaja machache.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji itahakikisha ukusanyaji wa mapato unaongezeka pamoja na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hayo. Hali hii itaiwezesha Serikali kutekeleza mipango ya maendeleo iliyowekwa katika Halmashauri hizo na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la uimarishaji wa ulinzi katika bandari zisizo rasmi bandari bubu, Serikali inaendelea na mikakati ya kuzitambua na

kuziwekea utaratibu maalum bandari hizo ili kutoa huduma katika hali ya usalama na kusaidia kuchangia upatikanaji wa mapato ya Serikali. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo imekuwa ikifanya doria za mara kwa mara katika maeneo yote ya mwambao wa visiwa vyetu ikiwemo maeneo ya bandari bubu kwa lengo la kuhakikisha maeneo hayo hayatumiki kuendeshea biashara haramu na yanabaki salama.

Mhe. Spika, katika hatua za kukabiliana na maafa nchini, Serikali imeendelea kutekeleza mipango na mikakati mbali mbali inayowezesha kupunguza athari za maafa iwapo yatatokezea. Miongoni mwa hatua muhimu zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuanzisha Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa badala ya Idara ili kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuratibu vizuri zaidi masuala ya kukabiliana na maafa hapa nchini. Aidha, Serikali kupitia Kamisheni hii imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa jamii na kuandaa miongozo ya kujiandaa na kukabiliana na maafa katika ngazi mbali mbali. Serikali itaendelea kuzijengea uwezo wa kitaaluma na kivifaa Taasisi zote zinazohusika na masuala ya kukabiliana na maafa nchini.

Mhe. Spika, katika kuimarisha makaazi ya Viongozi Wakuu pamoja na nyumba za Serikali zilizopo katika maeneo mbali mbali kwa Unguja na Pemba, Serikali inaendelea kuzifanyia matengenezo na kuziwekea vifaa muhimu ili ziweze kutumika kama zilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la wafanyakazi hewa, Serikali inaendelea na uhakiki wa watumishi wote wa umma na itahakikisha wale wote wasiositahiki kuwepo katika orodha ya watumishi wa umma wanatolewa. Aidha, Serikali itawachukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria wale wote watakaobainika kwa namna moja au nyengine kushiriki katika uhalifu huo.

HITIMISHO:

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuuendesha Mkutano huu wa Pili wa Baraza hili la Tisa kwa umahiri na umakini mkubwa. Vile vile, narudia kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa michango yao katika kupitisha bajeti ya Serikali na za Wizara zote katika mazingira ya ushirikiano yenye lengo la kuleta tija na kuimarisha utendaji na uwajibikaji Serikalini.

Mhe. Spika, nawashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na kujibu maswali ya Waheshimiwa Wajumbe kwa ufasaha. Pia, nawashukuru waandishi wa habari na wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi yao nzuri ya kuwapatia taarifa wananchi kuhusu majadiliano ya Baraza katika mkutano huu. Shukrani maalum nazitoa kwa Shirika la Utangazaji Zanzibar *ZBC* kwa kutangaza na kuonesha moja kwa moja *alive* shughuli zote za mkutano huu bila kusita.

Mhe. Spika, mwisho napenda kuvipongeza vyombo vyote vya ulinzi na usalama pamoja na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mchango wao mkubwa katika kudumisha usalama na utulivu uliopo hapa nchini.

Mhe. Spika, zipo kauli zinazosambazwa kupitia mitandao ya kijamii kuwa Serikali itachinja ng'ombe waliowakamata na kuuza nyama kwa bei rahisi ya Shs. 3,000 kwa kilo na kutolewa tahadhari kuwa watu wasinunue nyama hiyo eti siyo halali na ni nyama ya kifo. Napenda kuweka bayana kuwa kauli hizo hazina ukweli wowote. Hakuna ng'ombe yoyote atakayechinjwa na Serikali na kuuzwa Maisara kwa bei rahisi. Huu ni uongo na uzushi mtupu. Vile vile, kuna kauli nyeingine ya kuwazuia watoto wasiende kufurahi Mnazi Mmoja wakati wa Sikukuu eti kutatokea fujo na vurugu. Huu ni uongo mkubwa na uzushi usio na kifani. Serikali inawahakikishia wananchi kuwa hali ya nchi yetu iko salama na utulivu na itabaki hivyo siku zote. Kauli hizo ni propaganda za Wapinzani kutaka kuwahamanisha wananchi wapenda amani. Wananchi wanahakikishiwa kuwa viwanja vyote vya Sikukuu vitakuwa salama.

Mhe. Spika, tukiwa tumo katika kumi la mwisho la Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tunamuomba Mwenyezi Mungu atukubalie swaumu zetu na atujaaliye kumaliza faradhi hii kwa salama. Kwa vile hatutokaa tena katika kikao kama hiki kabla ya kumalizika mwezi Mtukufu wa Ramadhan, nachukua fursa hii kuwatakia Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi wote Sikukuu njema ya Eid-el-Fitri inayotarajiwa hivi karibuni *INSHAALLAH*. *Kuluam wa Antum Bukheir*.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi siku ya Jumatano, tarehe 21 Septemba, 2016 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, kwa hotuba mwanana kabisa ya kufungia Baraza niungane na Waheshimiwa Wajumbe, nami nikupongeze sana, Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha naomba nikupeni tangazo kwamba kutakuwa na semina kesho saa 3.00 Asubuhi ukumbi wa juu, kwa hivyo, mnaombwa mfike kwa wakati saa 3.00.

Waheshimiwa, sasa nachukua nafasi hii niwahoji kwanza, hoja imetolewa na Makamu wa Pili wa Rais na bahati nzuri imeungwa mkono na Mawaziri pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine kwa kusimama, sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja hiyo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe, tusimame kwa ajili ya wimbo wa taifa.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kuahirishwa kwa Mkutano)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa natangaza rasmi kwamba naahirisha shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano tarehe 21 Septemba, 2016 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 10:14 jioni Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 21/9/2016 saa 3.00 asubuhi)